**MTIHANI WA CEKENAS (1)**
*Hati ya kuhitimu Elimu ya Sekondari Nchini Kenya*
**102/1**
**KARATASI YA 1**
**(INSHA)**
**MUDA: 1¾**

***MAAGIZO:***
a) *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima***
b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia*
c) *Kila insha isipungue maneno **mia nne***
d) *Kila insha ina alama 20*

1. **Lazima**
Kumekuwa na visa vya ukosefu wa usalama nchini.
Wewe kama ripota wa gazeti la 'Fahamisha', andika taarifa kuonyesha njia mbalimbali ambazo washikadau wametumia kukabiliana na visa hivi.
2. Andika makala kuonyesha athari mbaya zinazotokana na kutotunza mazingira
3. Andika kisa kitakachodhihirisha ukweli wa methali:
Mwenye kovu usidhani kapoa
4. Andika kisa kitakachoanza kwa maneno yafuatayo
Nilisimama kama ilivyotuamuru sauti nzito ya kutisha. Nilijuta na kujawa na mawazo tele kwa kuhamia nchi nisiyoifahamu…..

---

**MTIHANI WA CEKENAS (1)**
*Hati ya kuhitimu Elimu ya Sekondari Nchini Kenya*
**102/2**
**KARATASI YA 2**
**(LUGHA)**
**MUDA: 2½**

www.freekcsepastpapers.com

1. **UFAHAMU** **(Alama 15)**
*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Nuru aliutazama uso wake kwenye kioo mara ya pili. Machozi yakamtiririka tiriri. Usowe mzima ulisawijika na kumwachia **sijiko**. Mabakamabaka yalipujua ile sura yake ya haiba na jamali ya hapo awali. Fikra zikimnyemelea tena. Hizo zikawa ni kumbukumbu za yaliyompata akiwa kwa shangazi yake wa ule mtaa wa Selea uliobebana na **wanawake kufu yake** huyo shangazi.

Miaka mitatu ilikuwa imepita baada ya kumtoroka adui, mwanamke aliyemwandama kama kupe kwenye mkia wa ng'ombe. Sijui kamkoseani? Hata hivyo, haikuwa nia ya Nuru kupatikana katika lile kasri lililotukuza vituko na vitushi vya kila nui. Ni huko kuishi walikokuheshimu hao wazaziwe. Yaani, mama yake na baba yake.

Safari ya binti wa makamo ya kuibeba mizigo yake na kuhama kwao, ilitukia pindi tu baada ya ajali mbaya ya trela iliyoigonga ile benzi yao. Wakopozi wake wakajilaza usingizi wa gogo usiojua wakati wa kuamka. Binti akaamua liwe na liwalo ale uhamisho. Akatia nanga kwa shangaziye.

Alipokelewa kwa mlahaka mzuri. Jinsi ujuavyo, mgeni siku ya kwanza! Akala akashiba akashukuru. Kumbe, zile shukrani ziliandamwa chini kwa chini na mafundo aliyokuwa nayo yule mwanadamu. Vituko vikaanza. Mara piga deki, mara vikogeshe vitoto, mara uinadhifishe dohani. "Ah! Kazi hii yote miye si

mashine! Natumia damu si petroli!" Kule kuyatamka maneno yale hadharani kukawa ni kujitongea. Alikuwa kajipalia makaa mwenyewe.

Akapangiwa hila. Katili akakitia chuma motoni. "Huyu kisirani leo atakiona na kukitambua cha mtema kuni" Aliyetajwa kuwa kisirani alikuwa usingizini. Chuma kilichopata makali ya moto kilimzindua mtu ndotoni baada ya kuuchunua usowe. Kilio kikamzidia. Akaangua kilio. Akaonewa mbawazi na msamaria mmoja jirani.

Alipotolewa hospitalini, aliapa kutoishi tena na hasidiwe. Akawa hana kani ya kurudi katika lile lindi lenye uhayawani. Waama, dunia rangi rangile. Kumbe ukatili wa namna hii ungalipo? Utu wa mtu uko wapi? Moyo wa ubua umetokomea wapi kiasi cha kuuruhusu **ufisadi kupiga simile na kupishwa na utu**? Ni ibada wazalendo wote wajitoe mhanga dhidi ya nyoyo katili kama hizi zinazohujumu sera za kuishi bila kuisha tu vivi hivi kivoloya alavoya. Mimi nadhani maovu yalimsalia shetani. Kumbe binadamu pia angali katika mikakati ya kumchangiza shetani?

**<u>Maswali</u>**

(a) Nuru alibadilika vipi kutokana na kuishi kwa shangazi yake? (al.2)

(b) Nuru alijipata vipi katika lile kasri lililotukuza vituko na vitushi? (al.2)

(c) Shangazi ya Nuru alikuwa mnafiki. Thibitisha. (al.2)

(d) Nuru alitendewa ukatili gani? (al.2)

(e) "Alikuwa kajipalia makaa mwenyewe." Thibitisha ukweli wa kauli hii kulingana na kifungu. (al.3)

(f) Toa mifano miwili ya matumizi ya 'uhuishaji' katika aya ya kwanza. (al.2)

(g) Eleza maana ya: (al. 3)

(i) wanawake kufu yake

(ii) ufisadi kupiga simile na kupishwa na utu

(iii) sijiko

**2. UFUPISHO** **(Alama 15)**

*Soma taarifa ifuatayo kisha ufupishe taarifa hii kulingana na maswali yanayofuata:*

Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, tumeshuhudia mabadiliko na maendeleo makubwa kuhusu vyombo vya habari nchini Kenya. Hapo awali, redio ndicho chombo cha habari cha kipekee kilichotamalaki kote nchini. Familia nyingi ziliweza kumiliki chombo hiki. Runinga ilikuwa miliki ya wachache, hasa mabwenyenye. Sasa hivi, hata akina yahe nchini na mashambani wanamiliki chombo hiki.

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasiliano kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundisha. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkem kwa mtu wa kila rika. Hali kadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji wa kufundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemichemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo wa vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu na maonevu ya rangi, dini, jinsia, kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya maambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanayowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

www.freekcsepastpapers.com

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa wanafamilia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii ukilinganisha na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake, tajriba ya televisheni huwa ya kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Hali kadhalika, runinga na video aghalabu hueeneza maadili yasiyofaa. Mathalan, baadhi ya vipindi vya televesheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa na kadhalika. Hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya dawa za kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watotowengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaoutumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya waelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Fupisha aya ya **nne** za kwanza kwa maneno 90. (al. 8)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

(b) Kwa maneno 80 eleza masuala yanayoibuliwa na mwandishi kutokana aya ya **sita** hadi ya **kumi.**(al. 7)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

(a) Andika sifa zinazotofautisha sauti zifuatazo: (al. 2)
   (i) /sh/ na /ch/
   (ii) /t/ na /th/

(b) Andika maneno yenye miundo ifuatayo: (al. 2)
   (i) KKI + KKKI
   (ii) I + KI + KI + KKI

(c) Andika maneno yenye miundo ifuatayo: (al. 2)
   i) Kiambishi ngeli (U-ZI, Umoja), wakati ujao, kauli tendwa, kauli tenda
   ii) Wingi (kitenzi), mzizi

(d) Huku ukitoa mifano, andika miundo miwili ya nomino katika ngeli ya U-I. (al. 2)

(e) Kando na nomino ya kitenzi-jina unda aina nyingine mbili mbili za nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo: (al. 2)
   i) konga……………………………………………………………
   ii) fisidi……………………………………………………………

(f) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao:
   i) KN (V + N) + KT (t) + KN (N + S) (al. 1)
   ii) KN (W + RV) + KT (T + RH) (al. 1)

(g) Andika sentensi ifuatayo katika wingi: (al. 2)
   Sehemu ya uga huo ilikarabatiwa kwa ubao na ufito na seremala.

(h) Kanusha sentensi hii (al. 1)
Mchezaji amekuwa akienda uwanjani.

(i) Tunga sentensi ukitumia nomino zenye miundo ifuatayo: (al. 2)
i) Nomino ambata
ii) Nomino milikishi

(j) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. (al. 4)
Gari la Ali lililonunuliwa juzi limepata ajali.

(k) Andika sentensi moja yenye kivumishi cha idadi isiyodhihirika na kielezi cha kiasi. (al. 2)

(l) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya **pamba** na **bamba.** (al. 2)

(m) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi '-li- (al. 2)

(n) Ainisha yambwa katika sentensi hii: (al. 3)
Basi hilo lilibebea wakongwe wengi mizigo iliyoletwa jana.

(o) Andika sentensi ifuatayo katika hali isiyodhihirika. (al. 2)
Viwango vya ujenzi vikiimarishwa, mijengo mingi itakuwa thabiti

(p) Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa:
"Tunaishi katika ulimwengu ambao umebadilika sana siku hizi," mwimbaji alisema. (al. 2)

(q) Andika sentensi hii katika hali ya ukubwa. (al. 2)
Kiti kilichobebwa na wazee kimetengenezewa watoto.

(r) Badilisha sentensi hii iwe katika wakati uliopita hali ya kuendelea. (al. 2)
Walimletea mikebe mingi ajabu.

(s) Shada ni kwa maua ______________________ ni kwa mtama
ilhali umayamaya ni kwa ____________________________ (al. 1)

(t) Rafiki yako ana mazoea ya kutoshukuru kila anapotendewa wema.
Andika methali inayoweza kutumiwa kumwonya dhidi ya tabia hiyo. (al. 1)

## 4. ISIMU JAMII (Alama 10)

Wewe ni Mwakilishi wa Wadi ya Tusongembele. Umepewa nafasi ya kuwasilisha mswada katika Bunge la Kaunti yako. Fafanua sifa **kumi** za lugha utakayotumia.

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA CEKENAS (1)**
*Hati ya kuhitimu Elimu ya Sekondari Nchini Kenya*
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**
**MUDA: SAA: 2.30**

***MAAGIZO:***
*a) Jibu maswali **manne** pekee*
*b) Swali la kwanza ni la lazima*
*c) Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Tamthilia, Riwaya, Ushairi na Hadithi Fupi*
*d) Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja*
*e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**SEHEMU A:**
**FASIHI SIMULIZI**
**LAZIMA**

**1. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

Mimi ni Olichilamgwara
Olichilamgwara mwana mbee wa Ojilong
Ojilong wa Marukatipe
Wazee waliposhindwa
Nilivuka misitu milima na mito
Ni mimi jabali
Kipande cha jifya la mama
Nilipokuwa nalisha mifugo
Nilisikia baragumu inalia
Baragumu ya wito
Mifugo wa mtemi wamechukuliwa
Nikachukua mkuki wangu
Wenye kigumba cha mti
Nikachukua upanga wangu
Wenye makali kama mmweso wa radi
Upanga uliopasua pembe za nyati kwa dhoruba moja
Ndipo nilipofyatuka kasi kama umeme
Kufumba kufumbua nikawakaribia nduli
Kusikia vishindi vyangu wakaanza kubabaika
Kuona kifua changu cha manyoya ya kanga wakatetemeka
Macho yangu makali kama kaa la moto yalipowatazama wakakimbia
Mkuki wangu ulipaa kama umeme
Wote wakalala
Mifugo wakanifuata…
Mko wapi vijana
Mmekuwa kama majivu baada ya moto kuzimika?

**Maswali**

a) Tambua kipera ulichokisoma na udhibitishe jibu lako (al. 2)
b) Tambua sifa za jamii zinazosawiriwa katika utungo huu (al. 2)
c) Kwa kutoa mifano bainisha vipengele vine vya kimtindo vilivyotumiwa na nafsineni (al. 4)
d) Fafanua sifa nne za kipera hiki (al. 4)
e) Eleza mambo manne ambayo mtendaji wa kipera hiki anaweza kufanya ili kufanikisha utendaji wake. (al. 4)
f) Fafanua mikakati ambayo jamii inaweza kutumia ili kuzuia tungo kama hizi kufifia (al. 4)

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU B:**
**TAMTHILIA: BEMBEA YA MAISHA, TIMOTHY AREGE**

**2. "Sima tayari. Ninaanda mchuzi….."**

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)
b) Onyesha umuhimu wa msemewa wa maneno haya (al. 6)
c) Tambua toni katika dondoo hili (al. 2)
d) Eleza changamoto zinazokumba ndoa za kisasa kwa kurejelea tamthilia nzima (al. 8)

3. "Masombo hufungwa kama walau mtu ametia kitu mdomoni. Pamoja na hali ngumu iliyopo, bado hatujafikia pa kukosa mlo wa kimsingi. Ndiyo hatumudu viliwa vya samli lakini hatuwezi kuishi kama kwamba tunazongwa na njaa. Tazama ulivyokonda unaelekea kushindana na ng'onda. Hii nafasi ya ng'onda unaitaka kwa nini?

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)
b) Tambua mbinu mbili za kimtindo zilizomo kwenye dondoo (al. 2)
c) Bainisha sifa nne za msemewa (al. 4)
d) Jadili namna msemaji amechangia katika kuendeleza
i) Ploti (al. 5)
ii) Maudhui (al. 5)

**SEHEMU C:**
**RIWAYA: Chozi la Heri la 4 au la 5**

4. a) …. haya imekuandama tangu usiku ukimtongoza fulani, siku za kuchora ramani ya Afrika kwa vyanda vya miguu hadi sasa? Ama ni hizo mvi unaficha? Naskia ile mid-life crisis ikiwashika wazee ndiyo hivyo,

i) Weka dondoo hili kwenye muktadha wake (al. 4)
ii) Tambua mbinu zozote tatu za kimtindo kwenye dondoo hii (al. 3)
iii) Jadili udhaifu wa msemewa (al. 4)

b) Dhibitisha kauli kwamba 'Kweli jaza ya hisani ni madhila'
Kwa kurejelea wahusika tisa kwenye riwaya ya Chozi la Heri (al. 9)

**RIWAYA: CHOZI LA HERI**

5. "Nashangaa kinachompa kijana kama huyu, na wengine waliofariki jana, ambao wamesomea shahada za uzamili, kujihusisha na unywaji wa pombe haramu!

a) i) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)
ii) Fafanua umuhimu wa msemaji katika dondoo hili (al. 4)
iii) Kando na maudhui ya elimu eleza maudhui mengine mawili katika dondoo hili (al. 2)

b) Eleza jinsi mwandishi alivyofaulu kutumia mbinu zifuatazo katika kuijenga riwaya hii
i) Hadithi ndani ya hadithi (al. 5)
ii) Mbinu rejeshi (al. 5)

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU D: USHAIRI**
**USHAIRI**
**Jibu swali la 6 ay la 7**

**6. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali**
**Said A. Mohamed: Mbele ya Safari**

Ilipoanza safari, ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

Njaa ikawa thabiti, na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati, tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti, dhila na mingi mikiki
Tulijizatiti.

Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari, utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari, juhudi iliyobaki
Tulijizatiti.

Ile ilikuwa ndoto, mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto, sahala 'mmekuwa dhiki
Wagombania kipato, utashi haukatiki
Na kutabakari.

Msafara ukasita, kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita, mlima haupandiki
Basi soe 'kajipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina.

Tukiwa migongo wazi, tukainama kwa shaki
Tukawa'chia ukwezi, kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi, kuteremsha miliki
Wakaitapia.

Wakafikia makazi, ya pumbao na ashiki
Huko wakajibarizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma uliomiliki
Mbele ya safari.

Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema mate, kwa umati halaiki
Imezima nia yote, kiza hakitakasiki
Mbele ya safari.

**MASWALI**

a) Eleza safari inayorejelewa katika shairi hili (al. 2)
b) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa (al. 3)
c) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili ukizingatia: (al. 2)
   i) Mizani
   ii) Vina
d) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari (al. 4)
e) Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita (al. 2)
f) Bainisha aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili (al. 2)
g) Fafanua aina mbili za taswira zinazojitokeza katika shairi hili (al. 2)
h) Kando na kinaya, bainisha vipengele vingine viwili vya kimtindo katika shairi hili (al. 2)
i) Eleza toni ya shairi hili (al. 1)

**7. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali**

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tilichinja ili uwe mwanamume,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu!
Iwapo utatingisa kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu
Ndege zote ziangamie.

www.freekcsepastpapers.com

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,
Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hiii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa.
Iwapo wewe ni mme,
Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri.

**<u>Maswali</u>**

a) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha (al. 2)
b) Tambua anayeimba na anayeimbiwa shairi hili (al. 2)
c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume (al. 2)
d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili (al. 4)
e) Taja shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili (al. 2)
f) Eleza mbinu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiuarudhi (al. 4)
g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili? (al. 4)
   i) Mbari
   ii) Msununu
   iii) Ngariba
   iv) Uvundo

**<u>SEHEMU E:</u>**
**HADITHI FUPI**
**Harubu ya maisha *Paul Nganga Mutua***

"Naja. Nakamilisha shughuli ndogo hapa kisha nianze safari…"

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)
(b) Eleza sifa sita za msemaji wa kauli hii (al. 6)
(c) Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi hii (al. 10)

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU**
**Hati ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari**
**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**

**MAAGIZO**
a) *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima.***
b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
c) *Kila insha isipungue maneno **400**.*

**Lazima**
1. Wewe ni katibu wa mmojawapo wa watu wanaowania nafasi ya uwaziri katika Wizara ya Elimu nchini.Andaa wasifu utakaowasilishwa katika kikao cha usaili.
2. Mahusiano kati ya Afrika na mataifa ya kigeni yana faida nyingi. Jadili
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
4. Andika insha inayoanza kwa maneno haya:
*Sherehe zilinoga kwa shamrashamra kwani tulikuwa tumefua dafu kutokana na ushirikiano wetu...*

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU, 2023**
**Hati ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari**
**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**LUGHA**
**Muda: Saa 2 ½**

**UFAHAMU**
Majuto alihamia mjini Tija na kununua ardhi kubwa na kujenga jumba kubwa lenye vyumba mia moja vya kukodisha na kando yake akajenga jumba lake la kifahari la kuishi na familia yake. Aliipenda sana hali yake mpya. Aliipenda zaidi hewa safi ya utajiri mjini. Aliyapenda mno mandhari mapya. Familia yake ilitabasamu na kuifurahikia sana hali hii nzuri. Majumba yake ya kukodisha yalijaa watu. Kila mwisho wa mwezi alipata milioni moja kutoka kwenye vyumba vyake vya kukodisha. Jambo hili lilimweka katika nafasi nzuri ya kujilimbikizia mali.

Mji wa Tija ulijaa matajiri wenye hela nyingi. Majuto alitamani kuwa na mali zaidi. Alitamani kuwa kama mmoja wa mabwanyenye katika mji wa Tija. Alitamani kuwa kama Mzee Mwinyi ambaye alimiliki magari mengi ya kifahari. Mwinyi alikuwa bilionea. Kila siku Majuto aliwaambia wanawe na mkewe kuwa angetamani sana kuwa kama Mzee Mwinyi na hata kuupiku ukwasi wake. Wao walimhimiza tu na kumwombea utu, uhai na uzima ili azitimize ndoto zake. "Baba, ipo siku utakuwa kama yeye. Work smart na umwombe God. Katika Biblia tunaambiwa kuwa Anna aliomba sana na akapewa mtoi", alisema Kiloo.

Kiloo alipenda sana kutembea mjini na kubugia pombe kwenye baa. Alipenda kujigamba sana mbele ya walevi wenzake. Aliwaeleza jinsi familia yake ilivyo tajiri na matarajio makubwa ya baba yake. Aliwadadavulia kuhusu nia nzuri ya baba yake kuwa bilionea na kumiliki vitu vya thamani kubwa. Walimsikiliza kwa umakini katika ulevi wao. Kumbe walevi huwa makini wakati mwingine!

Siku moja familia ya Majuto ilipata mgeni. Hawakuwa wamemwona mja huyu tangu kuhamia pale. Alikuwa amevalia suti ya samawati, shati jeupe na tai nyekundu. Alipendeza. "Jina langu ni Mweneza. Mimi ni nabii kutoka kijiji cha Mazingara. Roho wa Mungu amenielekeza hapa leo", alisema. Baada kuupata staftahi Mwenezi aliomba kuzungumza na Majuto pembeni.

Majuto alimpeleka Mwenezi katika chumba kimojawapo kwenye kasri lake ili wawe na mazungumzo ya **faragha**. "Roho wa Mungu amenituma kwako Mzee Majuto. Naona unataka sana kuwa na mafanikio makubwa zaidi maishani. Unataka kuwa bilionea. Hilo linawezekana. Ni mapenzi ya Mola kila mtu kufanikiwa kwa kiwango cha juu kulingana na imani yake. Amini na Mungu atatenda. Hata Mzee Mwinyi mimi ndimi nilimsaidia mwaka jana. Sasa yeye ni bilionea. Roho wa Mungu alinituma kwake jinsi alivyonituma kwako hii

leo. Zungumza na familia yako. Nitarejea baada ya siku mbili", alisema Mwenezi. Machozi ya furaha yalimdondoka Majuto na kuulowesha uso wake. Aliiona hiyo kama nafasi bora ya kuwa bilionea.
Familia ya Majuto ilizipokea habari hizo kwa imani kwamba ndoto ya mkuu wa familia hatimaye ingetimia. Fikiri wewe, unatamani kuwa mkwasi wa wakwasi kisha upate njia rahisi na nyoofu ya kulitimiza lengo hilo. Bila shaka utajituma sana. Hata hivyo, Mawazo alikuwa na mawazo tofauti. "Huenda huyu **nsi** anataka kutupunja! Huenda ana lengo la kuiporomosha familia hii. Huenda ana habari **akali** kuihusu familia yetu. Huenda ametumwa kuja kuisambaratisha familia hii," alijisemea.

Baada ya siku mbili Mwenezi alirejea. Uso wa Majuto ulidhihirisha waziwazi furaha aliyokuwa nayo ndani ya moyo wake. Alimweleza Mwenezi kuwa familia yake ilikuwa imeridhia na wangependa kujua Mola alivyoagiza wafanye. "Uza majumba yako yote ya kukodisha, gari lako na jumba lako hili la kifahari. Baada ya hayo leta hela zote niziombee. Zitaongezeka mara mia moja", alisema Mwenezi. Majuto alikubaliana na agizo hilo na kufanya yote aliyoelezwa. Alipata jumla ya milioni mia mbili baada ya kuwekua hela zote alizokuwa amehifadhi katika benki kutokana na kodi ya nyumba. Alijua moyoni na akilini kuwa hizi hela zingekuwa takribani bilioni ishirini baada ya kuombewa. Hatimaye angekuwa bilionea! Majuto alitafuta chumba cha kuishi siku hiyo ya siku pale mjini. Alilipa kodi ya mwezi mmoja katika chumba hicho kama alivyoagizwa na nabii wa Mungu.

Mzee Majuto alimpigia simu Mwenezi kwa furaha kuu na kumweleza kuwa amefanya yote jinsi alivyoagizwa. Nabii alimwambia aziweke pesa zote ndani ya karatasi nyeusi. Baadaye Majuto alimwelekeza nabii walipokuwa wamepanga chumba. Furaha ilijisawiri katika nyuso za wanafamilia. Kila mmoja akiwa na nia ya kuipokea hali yao mpya. Kulingana nao, walikuwa wameuona mkono wa Mungu usioonekana na wengi! "Leo ni leo, asemaye kesho ni mwongo. Walionikashifu watanisifu. Wataziramba nyayo zangu. Kumbe Mungu amekuwa akisikia kilio changu!" Alijisemea Majuto.

Mwenezi alifika katika eneo hilo bila kukawia. Alikuwa amebeba tangi kubwa la lita mia mbili na kumi. "Roho wa Mungu ameniamrisha nije na tangi hili ili nikimaliza kuziombea hela zako niziweke humu ndani. Utalifungua baada ya siku nne na uchukue mabilioni yako. Hata najua zitajaa na nyingine zimwagike humu ndani chumbani", alisema Mwenezi bila kupepesa jicho. Majuto alikubali na kuahidi kuyafuata maagizo yote. "Fungeni macho tuombe. Yafumbeni kabisa ili Mola asikie **sala** zetu," alisema. Baada ya maombi Mwenezi aliondoka na kurejea katika kijiji cha Mazingara.

Siku nne zilipoisha Mzee Majuto, mke wake na wanawe walijawa na furaha sana. "Leo mji mzima utanitambua. Nitanunua ardhi nyingine kubwa, magari mengi ya kifahari na ndege moja ya kuenda safari za mbali", alisema Mzee Majuto. Aliwaongoza wenzake katika kuufungua ule mtungi wenye pesa. Walishangaa sana kupata kuwa ule mtungi ulikuwa na ile karatasi nyeusi waliyoiweka. Walidhani tu zilizomo ni hela walizoweka pekee. Waliifungua kwa wasiwasi mkubwa. Mioyo yao ilidunda kama ngoma. Akili ziliwaduru. Mawazo alikuwa na msongo wa mawazo. Ndani ya karatasi hiyo mlikuwa na vijikaratasi vidogo vya gazeti. Kijikaratasi kimoja kilikuwa kimeandikwa, **AKILI NI MALI**, kingine kikaandikwa, **WEWE NI SAMAKI, MIMI NI BAHARI!**

Mzee Majuto alisema kwa majuto," Kumbe **nimepunjwa!** Eee Mungu wangu. Nionekanie Mola. Nilimwamini mtumishi wako.

www.freekcsepastpapers.com

**<u>Maswali</u>**

1. Yape makala haya kichwa mwafaka. (alama 1)
2. Ni jambo lipi ambalo Majuto alipania sana? (alama 1)
3. Eleza ujumbe unaojitokeza katika kifungu hiki. (alama 3)
4. Kwa nini Majuto alitaka kuwa bilionea? (alama 3)
5. Taja na ufafanue mbinu tatu za lugha zilizotumiwa katika kifungu hiki. (alama 4)
6. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 3)

i. kasri
ii. faragha
iii. akali

**UFUPISHO (ALAMA 15)**

*Soma kifungu kifutacho kisha ujibu maswali yanayofuata.*

Mataifa yanayoendelea yameathirika pakubwa na mabadiliko ya tabianchi. Hali hii imesababisha misimu mirefu ya kiangazi ambayo hatimaye yamesabisha ukame katika mataifa haya. Nchi nyingi pembeni mwa Afrika zenye maeneo kame yameitisha msaada wa dharura kwani jinamizi hili limesabisha maafa si haba. Taswira katika mataifa haya ni ya kutisha. Taarifa katika vyombo vya habari zimeonyesha mamia ya watu waliokufa kwa sababu ya ukosefu wa vyakula. Wengi wamekuwa watoto wachanga na wazee wasiojiweza. Watoto wamekuwa wakikumbwa na utapiamlo, kwani hata wakiambulia chakula hakitakuwa chenye madini mbalimbali yanayohiyajika mwilini. Utapigwa na butwaa vilevile unapoona watu waliokonda na kudhhofika kiafya. Huwa tayari wamefika mwisho na kupoteza matumaini huku wakichungulia kifo, yao imekuwa kusubiri misaada kutoka mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali.

Maji katika nyakati kama hizi za kiangazi huwa nadra kupatikana. Watu wengi hulazimika kutembea kwa kilomita nyingi angalau kupata hata kiasi kidogo cha maji. Hata baada ya kubahatika, hupanga foleni ndefu kwani watu hutegemea sehemu moja kupata maji. Hii ni kwa sababu mito mingi hunyauka na hata visima ambavyo ni vichache pia hunyauka. Maji mengine yanayopatikana huwa machafu. Kwa kuwa wakaazi hawana hiari, huishia kunywa na kuyatumia maji haya nyumbani. Hatima yake ni magonjwa yanatokana na maji machafu. Magonjwa hayo ni vile kama kipindupindu, homa ya matumbo miongoni mwa mengine. Ikumbukwe kuwa, hali katika zahanati za vijijini ni duni. Kando na haya, zahanati ni chache na zilizotengana mithili ya ardhi na mbingu. Watu wengi huaga dunia katika harakati za kutafuta huduma za matibabu ama hata kwa kukosa huduma hizo kabisa. Maelfu ya mifugo pia wamekuwa wakifa nyakati za kiangazi. Hii ni kwa kukosa lishe na pia maji. Hasara hii inatokea huku wenyeji wakikosa chakula. Mifugo wanaosalia huwa wamekondeana kama wamiliki wao. Hata kuuza ni balaa. Hali hii imekuwa si hali kwa muda sasa. Ni muhimu jambo hili liangaziwe kwa lengo la kupata suluhu ya kudumu.

Baada ya miezi mingi ya kiangazi, mvua inazuka kwa fujo. Maeneo yaleyale yanaripoti mafuriko. Msaada wa kibinadamu unaanza kuitishwa tena. Vifo vya watu na mifugo vinaanza kushuhudiwa. Maji yaliyokuwa nadra sasa yanapatikana kwa wingi kupita kiasi. Je, serikali za nchi hizi zina mipango madhubuti? Kuitisha misaada nyakati zote mbili hushangaza. Ni muhimu kuzingatia ujenzi wa mabwawa. Huu utakusanya maji yote ambayo yangesabisha maafa na kuhifadhi kwa minajili ya kutumika nyakati za kiangazi. Isitoshe, maji yayo hayo yanaweza kunyunyiziwa mimea na hivyo kuchangia pakubwa katika uzalishaji wa vyakula. Bila shaka, vifo vinavyotokana na uhaba wa vyakula vitapunguzwa na hatimaye kuzikwa katika kaburi la sahau.

Kuchimba visima vingi na kueneza nguvu za umeme pia kutaimarisha uwepo wa maji ya kunywesha mifugo na kutumika katika shughuli za nyumbani. Ni muhimu kumfundisha mtu kuvua samaki kuliko kumpa samaki kila wakati. Wananchi wafundishwe njia mwafaka za kuendeleza kilimo chenye kipato kikubwa. Huku kutawafanya kuzalisha kiwango kikubwa cha chakula. Kando na kuwafundisha ni kuwahimiza watu walio katika maeneo kame kupanda mimea inayoweza kustahimili angalau muda mrefu wa kiangazi ili isinyauke haraka. Serikali pia ziangazie upya bei ya pembejeo. Mbolea na mbegu zimekuwa bei ghali katika siku za hivi majuzi. Gharama hii imewavunja moyo wakulima wa maeneo ya nyanda za juu na yenye mashamba yenye uwezo wa kuzalisha vyakula vya kulisha maeneno mengine. Kwa sababu hii, kumekuwa hata na uhaba wa vyakula katika maghala ya serikali.

Kichwa kibaya cha ufisadi hakijakosa kupata mgao wake wa lawama katika suala hili pana la ukame na mabadiliko ya tabianchi. Viongozi wenye ushawishi serikalini wameishia kufuja pesa zinazotengewa ujenzi wa mabwawa, upunguzaji wa bei ya pembejeo na hata usambazaji wazo. Ni lazima umma na serikali ijizatiti katika vita dhidi ya ufisadi ili kuweza kuukomesha. Serikali pia iweze kuimarisha miundo msingi katika maeneno mbalimbali kwani hali duni ya miundo msingi imechangia. Barabara duni zimezuia usambazaji wa pembejeo na mavuno mashambani huku watu wakikosa chakula kicho hicho baadaye.

Ni lazima wafugaji wapate kuelewa kuwa mifugo wengi bila mipango ni hasara. Waweze kuwa na mifugo wanaoweza kuwashughulikia ili kupunguza hasara za vifo vyao wakati wa kiangazi. Wafugaji na serikali pia washirikiane kuanzisha au kuimarisha bima ya mifugo ili wafugaji wapate fidia wakati mgumu wa kiangazi na ukame. Kando na hilo, watafiti waimarisha mbegu ya mifugo wanaozaliwa kwani hili litaimarisha kipato chao. Kwa kweli, suala la madhara ya mabadiliko ya tabianchi linaweza kukabiliwa kwa kupanda miti mingi. Serikali na wananchi wapande miti katika mashamba ya serikali na ya watu binafsi. Wabinafsi wenye tabia ya kukata miti misituni ovyoovyo, hata katika chemichemi ya mito lazima wakomeshwe kwa kukabiliwa kisheria. Sheria zilizomo zitiwe shime ili kufanikisha vita hivi. Serikali, wananchi, mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali, miungano ya kimaeneo, kibara na kimataifa ikivalia njuga mabadiliko ya tabianchi na madhara yake, tutakuwa na sababu ya kutabasamu.

www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Fupisha aya za kwanza kwa maneno 80-90. (Alama 6,1 utiririko)
Matayarisho / Nakala safi

b) Eleza hatua za kukabiliana na madhara ya ukame na mabadiliko ya tabia nchi kwa maneno 100-110. (Alama 9,1 utiririko)
Matayarisho / Nakala safi

**MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Andika tofauti mojamoja kati ya sauti zifuatazo. (alama 2)
(i) /ny/ na /y/
(ii) /g/ na /gh/
b) Kwa kupigia mstari, onyesha panapotokea **shadda** katika maneno haya. (alama 1)
(i) majaka
(ii) paramamba
c) Onyesha mofimu katika neno lifuatalo. (alama 2)
awaye
d) Tenganisha silabi katika maneno yafuatayo (alama 2)
(i) kinena
(ii) masizi
e) Tumia neno **'zuri'** katika sentensi kama:
(i) kiwakilishi (alama 1)
(ii) kivumishi (alama 1)
f) Kutokana na mzizi **'-baya'** unda: (alama 1)
(i) nomino
(ii) kivumishi
g) Ainisha **virai** katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Wale wengine wataenda Moyale kwa ndege.
h) Andika kinyume cha sentensi hii kwa kuzingatia maneno yaliyopigiwa mstari (alama 1)
Punde tu <u>alipojibu</u> swali hilo Tunai <u>alitoka</u> darasani.
i) Andika katika wakati ujao hali ya kuendelea (alama 1)
Neema alimlipia Asna karo.
j) Andika miundo yoyote miwili ya nomino katika ngeli ya U-I (alama 2)
k) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo wingi (alama 2)
Debe hilo litasafirishwa pamoja na nyundo hiyo.
l) Ainisha **vitenzi** katika sentensi hizi:
(i) Paka alikuwa anamla panya. (alama 1)
(ii) Simba alikuwa mtini. (alama 1)
m) Andika katika usemi halisi. (alama 2)
Mwenyekiti alisema kuwa wangetoa nyongeza ya mshahara mwaka ambao ungefuata.
n) Tumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 1)
Omanyala aliwaona <u>waimbaji wengi sana</u>.
o) Jibu kulingana na maagizo:
(i) Mwalimu <u>aliwashauri</u> watahiniwa <u>wajibidiishe</u> masomoni.
(Geuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa nomino) (alama 2)
(ii) <u>Naam</u>, amepigwa <u>sana</u>. (Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari) (alama 2)
(ii) Wanafunzi wote walisoma maswali kwa makini. (Bainisha kiima na chagizo) (alama 2)
(iv) Ingawa hakuanza vizuri, alimaliza vizuri. (Ainisha vishazi) (alama 2)
p) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali (alama 4)
Mkutano utakaofanyika wiki ijayo utahudhuriwa na wanajopo wengi sana.
q) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo (alama 3)
Nuru alimnywesha babu yake uji mtamu kwa kikombe.
r) Tunga sentensi kubainisha matumizi yafuatayo ya kiambishi 'ki' (alama 2)
(i) Kuonyesha namna tendo lilivyofanyika
(ii) Kama kitenzi kishirikishi kipungufu
s) Alama ya kitone hutumiwa mwishoni mwa sentensi. Tunga sentensi moja kuonyesha matumizi mengine ya alama ya kitone (alama 1)

www.freekcsepastpapers.com

**ISIMU JAMII (alama 10)**

a) Eleza **kaida** zozote tatu za lugha (alama 3)

b) "Hapana ni kifaduro!" Alibisha mwingine…Maana ninasikia kupumua kunamtatiza…anapumua kama mgonjwa wa kifua.

(i) Tambua sajili ya makala haya na uthibitishe (alama 1)

(ii) Tambua mbinu tatu za kimtindo kifunguni. (alama 3)

(iii) Tambua sifa ambazo zingetumika kwenye sajili hii. (alama 3)

---

**MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU, 2023**

**Hati ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari**

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

**FASIHI**

Muda: Saa 2 ½

**Maagizo**

*(a) Jibu maswali **manne** pekee.*

*(b) Swali la **kwanza** ni la **lazima**.*

*(c) Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu **nne** zilizobaki; yaani: Tamthilia, Riwaya, Ushairi na Fasihi Simulizi.*

*(d) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.*

**SEHEMU A: HADITHI FUPI**

**YUSSUF SHOKA HAMAD:** ***Mzimu wa Kipwerere***

**1. Lazima**

…akikiomba radhi kile kitawi cha mti kilichonasa kwenye kazu yake ya rangi ya udongo iliyoficha kiwingu cha nongo kwa kukosa kuoshwa tangu ainunue! Nikauacha mpambano ule kati ya mzimu na mwenye dhamana ya mzimu ambao sina shaka ulidumu hadi asubuhi pale wanakijiji walipofika kushuhudia siri nzito iliyomezwa na mzimu ule waliokuwa wakiogopa na kuamini kiasi cha kuabudu kwa unyenyekevu na uchaji uliotukuka!

(a) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)

(b) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. (alama 4)

(c) Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo. (alama 4)

(d) Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha 'mwenye dhamana ya mizimu' na wenzake kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa Kipwerere kiasi cha kuabudu kwa unyenyekevu na uchaji uliotukuka. (alama 8)

**SEHEMU B: TAMTHILIA**

**T. AREGE:** ***Bembea ya Maisha***

***Jibu swali la 2 au la 3***

**2. (a)** 'Hizo juu-chini chini-juu ndizo utamu wake. Ni kama maisha kwa jumla. Yana pandashuka ndiyo lakini pandashuka hizo ndizo hutupa kuridhika hatimaye tunapozishinda.'

Thibitisha kuwa maisha yamejaa pandashuka ukirejelea tamthilia: *Bembea ya Maisha* (alama 10)

(b) 'Umenirudisha nyuma kweli katika siku zile za ujana wangu. Asubuhi niko skuli majira ya alfajiri…''

i. Eleza mbinu ya kimtindo inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

ii. Fafanua mifano mingine minane (8) ya matumizi ya mbinu hii katika tamthilia (alama 8)

**3.** "Mwenyewe ona ulivyokonda kama ng'onda!"

(i) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

(ii) Tambua mbinu **mbili** za lugha katika dondoo hili. (alama 4)

(iii) Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya. (alama 6)

(iv) Fafanua umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (alama 6)

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU C: RIWAYA**

**A. MATEI:** ***Chozi la Heri***

***Jibu swali la 4 au la 5***

**4** a) Hakiki mtindo wa mtunzi katika kifungu kifwatacho: (alama 8)

"Suala la polisi na wanajeshi kutatua mizozo midogo midogo kwa makeke na bunduki ni jambo ambalo limeanza kupitwa na wakati; ni sawa na kumwua chawa kwa fimbo! Raia wanahitaji zaidi ushauri badala ya vipigo. Kutatua tofauti zetu kwa vita ni kama kufukuta moto zaidi, na amani tuliyoazimia kupata haipatikani. Vilio vya raia kuhusu kile wanachokiiita *extra judicial killings* vimehanikiza kote. Huenda tusiwe wahusika katika visa hivi. Hata hivyo, ni vyema kutahadhari kabla ya hatari. Wakati mwengine, ndugu zangu amani haiji kwa ncha ya upanga!"

b) "Mwandishi amewasawiri vijana kuwa na nyoyo zilizoshiba wema." Dhihirisha ukweli wa kauli iliyosisitizwa kwa hoja 12 toshelevu. (alama 12)

**5.** "... jua langu li karibu kuchwa... sasa muda umefika. Hutakuwa na lawama duniani hata ahera iwapo utafunga akidi."

"... Hata mimi nimeliwazia jambo hili kwa muda. Hata hivyo, moyo wangu umekuwa yabisi, hisia zangu zimekufa ganzi."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Msemaji wa kauli 'hutakuwa na lawama duniani hata ahera' kando na kuwa msalihina, ana wasifu gani mwingine kwa mujibu wa dondoo hili? (alama 4)

(c) Jadili jinsi suala la uozo linavyojitokeza kwenye Jumuiya ya Chozi la Heri. (alama 12)

**SEHEMU D: USHAIRI**

***Jibu swali la 6 au la 7***

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Ndugu zangu waadhama, leo nawaulizia
Mlo Embu na Giriama, wote mpate sikia
Wazima hata vilema, rai zenu nanuia
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?
Miezi tisa tamima, tumbo lake nakalia
Kwa uwezo wa Karima, mama akajizalia
Ni mdogo sijasema, shida zangu ajulia
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

Mate kwake nimetema, mama hakunichukia,
Tumbo langu likiuma, kinyesi namtupia
Chakula hakuninyima, na dawa ya malaria
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?
Ni mtu mwenye huruma, tena wa kuvumilia
Hasa uwe ni yatima, baba amejifilia
Akufanyia huruma, mradi kutimizia
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?
Japo nimpe heshima, sioni kama murua
Wema wake nikipima, mbali bado huzidia
Kanipa nyingi huduma, nini nitamlipia?
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?
Nikimpa **darahima**, naona sijatimia
Unga viazi na nyama, sioni kama fidia
Zawadi zote kipima, ya kumpa sijajua
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?
Kwa heshima yake mama, kwaheri nawapungia
Naondoka himahima, swali langu nawachia
Nenda keti huko nyuma, jibu lenu nangojea
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

(Wallah Bin Wallah, *Malenga wa Ziwa Kuu*)

www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)

b) Andika bahari zinazojitokeza katika shairi kwa kurejelea:

i. vina (alama 1)

ii. vipande (alama 1)

iii. mishororo (alama 1)

c) Kwa kutolea mifano, onyesha mbinu alizotumia mshairi kuzingatia arudhi. (alama 3)

d) Tambua nafsineni katika shairi hili. (alama 1)

e) Bainisha mbinu zozote **mbili** za kimtindo katika shairi hili. (alama 2)

f) Andika ubeti wa **tatu** kwa lugha nathari (alama 4)

g) Tambua toni ya shairi hili (alama 1)

h) Andika maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi (alama 2)

(i) darahima

(ii) fidia

**7.** ***Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali***

Azali machozi yalilowesha mashavu yangu
Michirizi yakafanya na mitaro kuchimba
Chini yakadondoka na mchanga kulowesha
Utamu wake wa chumvi chumvi niliulamba
Nikapata hamaniko kuliondoa pasi kufahamu
Wakati mwingine yalichochea usingizi nikapata amani
Wakati huo yalikuwa ni maji tu
Maji, maji yaliyokolea chumvi.

Leo hii katika makako haya
Bado ninalia kama mtoto mdogo
Aliyenyimwa haki yake
Ingawa hutokea kwa tukizi
Nalia bado ndiyo ela si kwa sauti tena
Hulia kubwa ninapofika na kuliziba langu koo
Fundp hilo chungu huyafungua Masika
Ya mvua isiyofanya mawingu mazito meusi.

Hadi leo nimelia vilio vingi
Vipo niliapo nikiwa na wandani
Huku tukimenyana na vikombe viloshiba chai
Vipo niliapo nikiwa pweke
Nikizongwa na upweke wa chumba changu
Vilio vya kimnya visivyotaka kuhaniwa
Ni hivi vilio vya upweke
Ambavyo vyanituma shairi kuandika
Hivi vinavyotoka chini moyoni
Kwenye kiini cha chembe cha moyo.

Nimetambua kuwa matozi haya hatakauki
Lau yakapanguswa kwa kitambaa laini cheupe.
Michirizi yake hukauka lakini chemichemi zake hazikauki.
Chozi hili lina nguvu zinazozidi kiangazi

Halichi umri
Halichi cheo
Halichi jinsia
Halichi dini
Halichi uwezo
Chozi hili humea katika bonde la wetu unyonge
Chozi hili huvunja kingo za heshima na staha
Chozi hili huyeyuka kutoka kitovu cha utu

www.freekcsepastpapers.com

Chozi hili halikauki au likiwa, lina siha bado
Chozi hili ni daraja kati ya mawili yasiyoonekana kwa macho
Chozi hili lina nguvu kuliko silaha

Chozi hili litakauka
Pale moyo utakapokauka
Na mkono kuzipa
Hadithi zisizotangazwa za hakina Phili.

**Maswali**

a) Hili ni shairi la aina gani? Tetea jibu lako. (alama 3)
b) Chozi halibagui. Kwa mujibu wa shairi hili, eleza ukweli wa kauli hii. (alama 3)
c) Eleza aina za urudiaji katika shairi hili. (alama 3)
d) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 1)
e) Mtunzi wa shairi hili amefaulu kutumia uhuru wake. Fafanua. (alama 2)
f) Jadili matumizi ya aina zifuatazo za mistari katika shairi hili. (alama 2)
   i) mishata
   ii) kifu
g) Eleza aina zozote **tatu** za taswira katika shairi hili. (alama 3)
h) Kwa mujibu wa shairi hili, ni muhimu kulia. Tetea ukweli wa usemi huu huku ukitolea mifano maridhawa. (alama 1)
i) Eleza matumizi ya vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili: (alama 2)
   i) chuku
   ii) tasfida

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8. Mababu zetu walituriithisha heshima, utu, utamaduni wa amani, imani na upendo. Tunatambua nia yao njema ya kuona jamii ikiishi kwa utulivu, umoja, mshikamano na uelewano. Leo hii nyuso zetu zimesawijika. Nyuso zimeinama kwa matokeo mabaya ya kitendo cha ubinafsi, unyama na ukatili cha mmoja wetu. Kama jamii, kama watu wa ukoo wa Shani wa Miramba, tunajitenga na ila hii. Tunamkana Kaliko wa Ndaya. Damu yake si yetu. Tunakemea na kulaani kitendo chake cha ubakaji. Tunalaani umaluuni huu kwa kinywa kipana. Mababu zetu wamemkataa. Mungu wetu mwenye kutaka heri kwa waja wote atuepushe adhabu na ghadhabu yake. Tunaomba dua kwako Mungu wa Mlima mkuu uliovikwa kofia ya theluji na kutukuka. Yalinde mashamba yetu tupate mazao mazuri; ila iliyoingia kwetu isije na kiangazi. Mawindo ya usasi wetu yasitupotelee kutokana na kasoro hii. Tunaomba mito yetu isikauke tusikose kitoweo humo na maji kwa mifugo wetu. Bariki ukoo wetu mtukuka. Tubaki imara kama mwamba. Ukoo wetu ni nyota siku zote. Ndiyo ni nyota! Ukoo wa Shani wa Miramba udumu milele!

a) Bainisha kipera cha utungo huu na utoe ushahidi wako. (alama 2)
b) Taja sifa zozote tano za kipera hiki. (alama 5)
c) Kipera hiki kina nafasi gani kwa jamii? (alama 5)
d) Mwasilishaji wa kipera hiki anahitajika kuwa wasifu upi ili kukifanikisha? Fafanua kwa hoja tano. (alama 5)
e) Jamii inayohusishwa kifunguni inajiendelezaji kiuchumi? (alama 3)

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU, 2023**
**Hati ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari**
**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**LUGHA**

**UFAHAMU**

1. Yape Makala haya kichwa mwafaka. (alama 1)
**Tamaa ya Majuto/Majuto/Majuto ni mjukuu**

2. Ni jambo lipi ambalo Majuto alipania sana? (alama 1)
**i. Majuto alitamani kuwa Tajiri Zaidi.**
**ii. Alipania kuwa na mali Kama mzee Mwinyi.**

3. Eleza ujumbe unaojitokeza katika kifungu hiki. (alama 3)
**i. Baadhi ya watu wanahadaika kutokana na tamaa ya mali na hivyo kupoteza mali nyingi.**
**ii. Watu kama vile Mwenezi wanatumia udanganyifu ili kujinufaisha na kujitumia jina la Mungu ili waaminiwe.**
**iii. Baadhi ya wahubiri wanatumia ujanja ili kujitajirisha.**

4. Kwa nini Majuto alitaka kuwa bilionea? (alama 3)
Ili mji mzima umtambue
**i. Anunue ardhi nyingine kubwa.**
**ii. Anunue magari mengi ya kifahari.**
**iii. Anunue ndege moja ya Kwenda safari za mbali.**

5. Taja na ufafanue mbinu tatu za lugha zilizotumiwa katika kifungu hiki. (alama 4)
**i. <u>nidaa</u>-kumbe nimepunjwa!**
**ii. <u>tashihisi</u> -leo mji mzima utanitambua**
**iii. <u>majazi</u>-Mwinyi (Tajiri), Majuto-alijuta kwa kumwamini Mwenezi.**
**iv. <u>methali</u> -leo ni leo, asemaye kesho ni mwongo.**
**v. kuchanganya ndimi-work smart na umwombe Mungu.**

6. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu. (alama 3)
i. kasri -**Jumba kubwa la kifahari.**
ii. faragha- **fiche, chemba**
iii. akali- **chache**

**MUHTASARI/UFUPISHO**

**a) Fupisha aya za kwanza kwa maneno 90-100. (Alama 6,1utiririko)**
i) Mataifa yanayoendelea yameathirika pakubwa na mabadiliko ya tabianchi na madhara ukame.
ii) Nchi nyingi pembeni mwa Afrika zenye maeneo kame yameitisha msaada wa dharura.
iii) Mamia ya watu wamekufa kwa sababu ya ukosefu wa vyakula.
iv) Watu pia wamedhoofika kiafya kwa sababu ya uhaba wa vyakula.
v) Kiangazi kimesababisha uhaba wa maji.
vi) Watu wanalazimika kutembea kilomita nyingi angalau kupata hata kiasi kidogo cha maji.
vii) Maji mengine yanayopatikana huwa machafu na hivyo kusababisha magonjwa.
viii) Watu wanaaga dunia kwa kukosa huduma za matibabu.
ix) Mifugo wengi hufa kwa kukosa maji na vyakula kwa sababu ya ukame.

b) Eleza hatua za kukabiliana na madhara ya ukame na mabadiliko ya tabianchi. **(Alama 9,1 utiririko)**
**NJIA YA KUKABILIANA YA MADHARA YA MABADILIKO YA TABIA NCHI NA UKAME.**
i) ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya unyunyiziaji wa maji
ii) uchimbaji wa visima
iii) kupunguza bei ya pembejeo na mbolea
iv) wananchi wafundishwe njia mwafaka za kuendeleza kilimo chenye kipato kikubwa cha chakula.
v) wakulima wahimizwe kupanda mimea inayoweza kustahimili angalau muda mrefu wa kiangazi
vi) ufisadi ukabiliwe vikali

www.freekcsepastpapers.com

vii) lazima wafugaji wafuge mifugo wanaoweza kuwashughulikia ili kupunguza hasara
viii) wafugaji na serikali washirikiane kuanzisha au kuimarisha bima ya mifugo ili wafugaji wapate fidia wakati mgumu wa kiangazi.
ix) serikali na wananchi wapande miti katika mashamba ya serikali na ya watu binafsi.
x) ukataji wa miti ukomeshwe kwa kuwachukulia hatua za kisheria wanaohusika.

**MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)**

a) (i) /ny/ ni king'ong'o ilhali /y/ ni kiyeyusho/nusu irabu (alama 1)
(ii) /g/ ni kipasuo ilhali /gh/ ni kikwamizo. (alama 1)

b) (i) ma-<u>ja</u>-ka (½)
(ii) pa-ra-<u>ma</u>-mba (½)

c) a-nafsi (½)
w-mzizi(½)
a-kiishio(½)
ye-kirejeshi(½)

d) (i) ki-ne-na (alama 1)
(ii) ma-si-zi (alama 1)

e) (i) <u>Zuri</u> limenunuliwa. (alama 1)
(ii) Gari <u>zuri</u> limenunuliwa. (alama 1)

f) (i) ubaya(½)
(ii) mbaya/kibaya/vibaya/baya(½)

g) wale wengine- kirai nomino (alama 1)
wataenda Moyale- kirai kitenzi (alama 1)
kwa ndege- kirai kihusishi
(mtahiniwa aandike virai vyovyote viwili, kila kimoja alama moja)

h) punde tu <u>alipouliza</u> swali hilo Tunai <u>aliingia</u> darasani. (alama 1)

i) Neema atakuwa anamlipia Asna karo. (alama 1)
AU
Neema atakuwa akimlipia Asna karo.

j) (i) M-MI: mkoba-mikoba, mkate-mikate, mti-miti, mto-mito
(ii) MW-MI: mwiba-miba, mwaka-miaka, mwezi-miezi
(iii) MU-MI: muwa-miwa, muundi-miundi, muundo-miundo
(iv) MO-MI: moyo-mioyo-moto-mioto
Miundo yoyote miwili, kila muundo pamoja na mfano ni alama moja.

k) Videbe hivyo vitasafirishwa pamoja na vijundo hivyo. (alama 2)

l) (i) alikuwa-kitenzi kisaidizi(½)
anamla- kitenzi kikuu(½)
(ii) alikuwa-kitenzi kishirikishi kikamilifu (alama 1)

m) "Tutatoa nyongeza ya mshahara mwaka ujao," Mwenyekiti alisema. (alama 2)

n) Omanyala aliona <u>kikoa cha waimbaji</u>. (alama 1)

o) (i) Mwalimu aliwapa <u>ushauri</u> watahiniwa watie <u>bidii</u> masomoni. (alama 2)
(ii) naam-kihisishi cha kuitikia (alama 1)
sana-kielezi cha namna halisi (alama 1)
(iii) kiima-wanafunzi wote (alama 1)
chagizo-kwa makini (alama 1)
(iv) kishazi huru-Alimaliza vizuri. (alama 1)
kishazi kitegemezi- ingawa hakuanza vizuri (alama 1)

p)

| S | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KN | | KT | | | | |
| N | S̄ | T | H | N | V | E |
| Mkutano | utakaofanyika wiki ijayo | utahudhuriwa | na | wanajopo | wengi | Sana. |

q) (i) shamirisho kipozi-uji mtamu (alama 1)
(ii) shamirisho kitondo-babu yake (alama 1)
(iii) shamirisho ala-kikombe (alama 1)

www.freekcsepastpapers.com

r) (i) Tetu alikula kifisi (alama 1)
(ii) Kisu ki mezani. (alama 1)

s) Sentensi ya mtahiniwa idhihirishe moja kati ya matumizi haya: (alama 1)

i. kuandika maneno kwa kifupi- S.L.P (sanduku la posta)
ii. kuandika tarehe- 30.6.2023
iii. kutenganisha shilingi na senti- 200.50 (shilingi mia mbili na senti hamsini)
iv. kuonyesha nambari za desimali

**ISIMU JAMII (alama 10)**

**a) Eleza kaida tatu za Lugha. (alama 3)**

(i) Cheo cha mtu-Madaraka ya mtu huchangia msamiati wa kutumia.Waajiri hutumia lugha ya kuamuru ilhali waajiriwa hutumia Lugha ya upole na adabu

(ii) Umri-Vijana wana namna ya kutumia lugha inayojihusisha na mitindo mipya tofauti na wazee wanaotumia msamiati wenye hekima na ushauri.

(iii) Uhusiano-Kuna mahusiano ya aina nyingi kwa mfano mtoto atatumia lugha kwa njia tofauti katika kuwasiliana na wazazi wake tofauti na vile atazungumza na watoto wa rika lake.

(iv) Hali ya mtu-Mgonjwa atazungumza kwa upole wakati Melvin atazungumza kiholela bila kuchagua maneno

(v) Utabaka-Watu wa tabaka la juu wanapenda kuchagua maneno ya kifahari ilhali watu wa tabaka la chini hutumia maneno ya kawaida.

(vi) Mazingira-Lugha hutegemea mazingira ya wazungumzaji kama vile mahakamani,nyumbani, sokoni, kanisani na kadhalika

(vii) Jinsia-Unyenyekevu hujitokeza katika mazungumzo ya wanawake na ambayo ni tofauti na ya wanaume. Lugha ya wanaume huwa na fujo, kiburi na hali ya kutojali sana. Wanawake watajikita katika mapambo ilhali wanaume watajikita katika siasa na kandanda

zozote 3×1=3

**b) "Hapana ni kifaduro!"Alibisha mwingine...Maana nikasikia kupumua kunamtatiza... anapumua kama mgonjwa wa kifua.**

(i) Tambua sajili ya makala haya na udhibitishe (alama 1)
Sajili ya hospitalini-kupumua kunamtatiza anapumua kama mgonjwa wa kifua
(ataje na athibitishe 1×1=1)

(i) Tambua mbinu za kimtindo kifunguni (alama 3)
(i) nidaa-"Hapana ni kifaduro!"
(ii) mdokezo- Alibisha mwingine...
(iii) tashbihi-anapumua kama mgonjwa wa kifua
3×1=3

(iii) Tambua sifa ambazo zingetumika kwenye sajili hii (alama 3)

(i) Lugha ya kudadisi-Daktari anapouliza maswali
(ii) Lugha ya upole na unyenyekevu-Mgonjwa
(iii) Utohozi hutumika
(iv) Lugha yenye huzuni na hofu
(v) Hutumia sentensi fupi fupi Kwa urahisi wa maelewano
zozote 3×1= 3

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA MWIGO GATUNDU KUSINI**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA KWANZA**
**INSHA**
**Muda: Saa 1¾**

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA**
*(a)* Andika insha **mbili**.
*(b)* Insha ya kwanza ni ya **lazima**.
*(c)* Chagua insha moja nyingine kutokana na hizo tatu zilizobakia.
*(d)* Kila insha isipungue maneno **400**.
*(e)* Kila insha ina alama 20.

**1.** Wewe ni mkurugenzi wa masuala ya Elimu katika kata ya Gatundu. Umeambiwa na wizara ya Elimu kuandika ripoti kuhusu sababu za kudorora kwa matokeo ya mitihani katika eneo hilo. Andika **ripoti** yako
**2.** Wewe ni meneja wa shirika la Tangazo. Andika **memo** kwa wafanyikazi wako ambao wamekuwa wakilalamikia hali ngumu ya uchumi. Kwenye memo yako onyesha athari za hali ngumu ya maisha
**3.** Andika kisa kinachodhihirisha maana ya methali: **Usitukane wakunga na uzazi ungalipo.**
**4.** Tunga kisa kitakachomalizia kwa maneno **............niliapa kutoshiriki katika vita vya kikabila tena.**

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA MWIGO GATUNDU KUSINI**
**KISWAHILI**
**102/2**
**KARATASI YA PILI**
**LUGHA**
**MUDA: SAA 2½**
**MAAGIZO**
- Jibu maswali yote.

1. **UFAHAMU ( ALAMA 15 )**
***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Lugha ya Kiswahili ndio lugha muhimu katika eneo lote la Afrika Mashariki na Kati. Hii ni kwa sababu lugha hii ina nafasi ya kipekee katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Katika nchi hizi, Kiswahili ni lugha ya taifa. Pia, wananchi wengi wa Afrika Mashariki wanaelewa na huitumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao, hivyo kuipa lugha hii nafasi ya kipekee katika mambo muhimu kama utamaduni, siasa, na uchumi.

Wataalamu wengi wa masuala ya utamaduni wanakubaliana kwamba kwa kiasi kikubwa, lugha ni kielelezo cha utamaduni. Ukweli huo hujidhihirisha katika lugha yenyewe. Ukichunguza kwa makini lugha yoyote, utagundua kwamba ina vipengele mbalimbali vya utamaduni wa wasemaji wa lugha hiyo ambavyo vinajitokeza ndani mwake.

Vilevile, nafasi iliyonayo Kiswahili katika masuala ya siasa ni jambo lisilohitaji kupigiwa ngoma. Tangu enzi za wakoloni, lugha ya Kiswahili ilitumika kama chombo muhimu cha kuunganisha watu na kuleta umoja. Harakati nyingi ziliendeshwa kwa Kiswahili. Kwa kuwa Kiswahili ndio lugha itumiwayo na watu wengi katika Afrika Mashariki kuleta uelewano, basi ndio lugha wanasiasa hutumia katika mikutano yao.

Aidha, Kiswahili ndio lugha pekee ambayo inazungumzwa zaidi dhidi ya lugha nyingine katika maeneo ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini ambapo zipo lugha nyingine.

Katika ukuaji wa uchumi, Kiswahili ni muhimu vilevile. Lugha ambayo inafahamika kwa watu wengi ndio ifaayo kutumiwa katika mawasiliano ya kibiashara. Tangu zamani, wananchi wa Afrika Mashariki wamekuwa wakiitumia lugha hii katika shughuli zao za kibiashara.Kiswahili kingemwezesha Mkenya kwenda Tanzania, hata vijijini, akaendesha shughuli zake za kibiashara bila taabu ya kutafuta mkalimani.

Hali hii pia inajiakisi katika jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Malawi, Ngazi ja (Comoro ), Burundi na Rwanda.

Siku hizi, Kiswahili kinatumika katika idhaa za nchi nyingi za ulimwengu kama vile Uchina, Afrika Kusini, Urusi, Ujapani, Ujerumani, India na nyingine ambapo Kiswahili kimepewa nafasi. Aidha, vyuo vikuu mashuhuri duniani kama vya nchini Marekani, Uingereza, Ujapani, Korea, Urusi, Uchina na kwingine sasa vinafundisha Kiswahili. Isisahaulike kuwa Kiswahili ni lugha mojawapo rasmi ya Umoja wa Afrika.

Kwa jumla, Kiswahili kinaendelea kukua kila kukicha. Kilichobaki ni kwa wakereketwa wa Kiswahili kuendelea kukieneza na kukipangia mikakati mingi inayoweza kusaidia kukiendeleza ili kiweze kusambaa kwa mapana na marefu.

***Maswali***

(a) Kwa nini mwandishi anasema kuwa nafasi ya Kiswahili katika siasa "haifai kupigiwa ngoma"? (alama 3 )

(b) Kuna ithibati gani kuonyesha kuwa Kiswahili sasa kimekuwa lugha ya kimataifa. (alama 3 )

(c ) Unafikiri Kiswahili kina umuhimu gani? (alama 5 )

(d) Eleza (alama 4 )

(i) Lugha ya taifa

(ii) Lugha rasmi

**2. UFUPISHO ( ALAMA 15)**

***Soma taarifa kisha ujibu maswali yanayofuata kutegemea maagizo.***

Dunia sasa imegeuka ikilinganishwa na vile ilivyokuwa zamani. Siku hizi, jambo linapotokea popote duniani, linajulikana kwingineko kwa haraka. Hali hii imeathiri jinsi mabadiliko yanavyotokea na kuifumania jamii. Sasa, mwanafunzi anaweza kufanya maamuzi kwa haraka na kubadilisha mawazo na hivyo kufikia maamuzi hata kupitia kwa baruapepe. Hata hivyo, wakereketwa wengine wanadai kuwa hali hii imechangia pakubwa "kudhoofika" kwa tabia ya usomaji.

Katika burudani, mambo sasa ni tofauti. Zamani watu wakiwa na njia finyu za kujiburudisha lakini siku hizi zimejaa tele. Mja anaweza kuchagua kujiburudisha akiwa nyumbani kwake katika chumba cha kulala kupitia kwa mtandao. Wengi wanasema kuwa hali hii imesaidia kuwepo burudani aipendayo mtu kwa sababu ya kuwepo uteuzi. Lakini pia kuna shutuma. Hali hii inasemekana kurahisisha kasumba ya kikoloni kupitia kwa uigizwaji wa tamaduni za kigeni ikiwemo lugha.

Jamii nyingi siku hizi zimebadilisha mawazo yao na utendaji katika jamii kwa sababu ya utandaridhi. Watu wamebadilisha fikra kuhusu masuala na dhana potovu, hali ambayo imebadilisha hali ya maisha katika jamii. Dhana kama usawa wa kijinsia na mawazo ya kisasa limekuwa jambo la kawaida. Watetezi wa masuala ya kiasili wanasema kuwa hali iliyozuka imedhoofisha utamaduni wa Kiafrika, kustaarabisha watu na kuchangia kusambaratika kwa familia kutokana na kuongezeka kwa visa vya kuvunjika kwa ndoa.

Kuwepo kwa mtandao kumefanya mambo kuwa rahisi kwa njia nyingi. Lakini hali hiyo pia imechangia kuwepo kwa hali ya kuchanganyikiwa hasa miongoni mwa vijana wasioweza kujiamulia kuhusu wanayoyaona na kuyasikia. Baadhi ya watafiti pia wanasema kuwa hali hii imechangia kuwepo kwa uvivu kwa sababu ya runinga.

Kwa sababu hii pia, mabadiliko makubwa yanaendelea kutokea katika masomo huku ujanja mwingi na kutozingatiwa kwa maadili ukishuhudiwa.

(a) Eleza faida zinazotokana na mabadiliko yaliyoko katika jamii.
(Maneno 30 – 40 ) (alama 6 mtiririko 1 )
Nakala chafu/Nakala safi

(b) Ni matatizo gani yanayoambatanishwa na mjo wa hali ya sasa ?
(Maneno 40 – 50 ) ( alama 6 mtiririko 2)
Nakala chafu/Nakala safi

www.freekcsepastpapers.com

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

a) Andika neno lenye mtindo ufuatao (al. 2)
Kipasuo kwamizo si ghuna cha kaakaa gumu, irabu ya chini kati, kipasuo si ghuna cha kaakaa laini, irabu ya mbele juu

b) Huku ukitoa mifano, eleza maana ya sauti mwambatano (al.2)

c) Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu (al.2)
Mkurugenzi anawaamuru wafanyakazi katika kampuni yake.

d) Eleza matumizi ya viambishi vilivyopigwa mstari (al.2)
Mtahiniwa ali<u>ji</u>suta baada ya kupata alama tano <u>kwa</u> ishirini

e) Andika sentensi zifuatazo kwa kuzingatia maagizo kwenye mabano

i) Vitabu vilipopotea muktubi alikuwa na wasiwasi (Aanza kwa kupotea............) (al. 1)

ii) Mchoraji <u>alichora</u> picha hiyo vizuri <u>akawafurahisha</u> watalii
(Geuza maneno yaliyopigwa mstari kuwa nomino) (al.2)

f) Bainisha ngeli za nomino zifuatazo (al.2)

i) Karatasi__________________________________________________________

ii) Mbatata__________________________________________________________

g) Andika kwa wingi (al.2)
Ukwato uo huo ulimsaidia kutambua kondoo wake

h) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao (al.2)
nomino ya kitenzi jina, kivumishi kionyeshi cha wastani, kivumishi cha pekee cha kutobakiza, kitenzi halisi

i) Tunga sentensi kutumia kiunganishi cha kutofautisha (al.1)

j) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo (al.2)
Wanafunzi wa kingereza wataenda Msambweni ijumaa

k) Andika katika usemi halisi (al.3)
Mkufunzi alishangaa na kutaka kujua kama Awiti ndiye aliyekuwa amemwibia Njoroge siku iliyotangulia

l) Kanusha sentensi ifuatayo (al.1 )
Wanasiasa wameenda bungeni kujadili mswada.

m) Tunga sentensi zenye miundo ifuatayo (al 2)

i) Kishazi tegemezi ambacho ni kivumishi.

i) Kirai kihusishi ambacho ni kielezi cha mahali.

n) Andika katika hali ya udogo wingi (al.2)
Fahali huyu aligonga ndoo hiyo

o) Akifisha sentensi ifuatayo (al.2)
jihadhari akasema kulei uamuzi wako unaweza kukuathiri vibaya

p) Eleza matumizi ya neno **wale** katika sentensi (al.2)
Mashemeji wale waliambiwa wale kabla ya sherehe kuanza

q) Andika sentensi ifuatayo kuanzia na yambiwa (al.1)
Mbunge wa Tononokeni aliwajengea watu hospitali sita mwaka uliopita

r) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mishale (al.2)
Wale wandanganyifu walikuwa wanasumbua wenyeji

s) Tunga sentensi kudhirisha dhamira ya (al.2)

i) Rai

ii) Hisi

t) Mama ni kwa nina akali ni kwa ............................ na dua ni kwa ................. (al.2)

u ) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kutendesha (al. 1)
Mama amemfanya mtoto alie

**ISIMU JAMII**

Karibu Bw. Ngatia. Fungua kinywa utapewa painkillers. Umeze mara tatu kisha utang'olewa meno mengine ambayo yanakusumbua. Urudi tena kuoshwa zaidi.

a) Bainisha sajili ya makala haya kwa kutoa mfano kutoka kwenye makala (al.2)

b) Fafanua sifa zinazojitokeza na zingejitokeza katika makala haya (al.8)

www.freekcsepastpapers.com

**<u>MTIHANI WA MWIGO WA GATUNDU KUSINI</u>**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**
**Muda:2½**

***<u>MAAGIZO:</u>***

1. *Jibu maswali **MANNE** pekee*
2. *Swali la kwanza ni la **LAZIMA***
3. *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani : Tamthilia, Riwaya, Ushairi na HadithiFupi*
4. *Usijibu maswali <u>mawili</u> kutoka sehemu moja*
5. *Majibu yote <u>lazima</u> yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**<u>SEHEMU A:</u>**
**<u>FASIHI SIMULIZI</u>**
**<u>LAZIMA</u>**

1. **<u>Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali</u>**

Mimi ni Olichilamgwara
Olichilamgwara mwanambee wa Ojilong
Ojilong wa Marukatipe
Wazee waliposhindwa
Nilivuka misitu milima na mito
Ni mimi jabali
Kipande cha jifya la mama
Nilipokuwa nalisha mifugo
Nilisikia baragumu inalia
Baragumu ya wito
Mifugo wa mtemi wamechukuliwa
Nikachukua mkuki wangu
Wenye kigumba cha mti
Nikachukua upanga wangu
Wenye makali kama mmweso waradi
Upanga uliopasua pembe za nyati kwa dhoruba moja
Ndipo nilipofyatuka kasi kama umeme
Kufumba kufumbua nikawakaribia nduli
Kusikia vishindi vyangu wakaanza kubabaika
Kuona kifua changu cha kanga wakatetemeka
Macho yangu makali kama kaa la moto yalipowatazama wakakimbia
Mkuki wangu ulipaa kama umeme
Wote wakalala
Mifugo wakanifuata…
Mko wapi vijana
Mmekuwa kama majivu baada ya moto kuzimika?

<u>Maswali</u>

a) Tambua kipera ulichokisoma na uthibitishe jibu lako (al. 2)
b) Tambua shughuli za jamii zinazosawiriwa katika utungo huu (al. 2)
c) Kwa kutoa mifano bainisha vipengele vinne vya kimtindo vilivyotumiwa na nafsineni (al. 4)
d) Fafanua sifa nne za kipera hiki (al. 4)
e) Eleza mambo manne ambayo mtendaji wa kipera hiki anaweza kufanya ili kufanikisha utendaji wake. (al. 4)
f) Fafanua mikakati ambayo jamii inaweza kutumia ili kuzuia tungo kama hizi kufifia (al. 4)

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU B:**
**TAMTHILIA: BEMBEA YA MAISHA, TIMOTHY AREGE**

2. “Sima tayari. Ninaandaa mchuzi…..”

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)
b) Onyesha umuhimu wa msemewa wa maneno haya (al. 6)
c) Tambua toni katika dondoo hili (al. 2)
d) Eleza changamoto zinazokumba ndoa za kisasa kwa kurejelea tamthilia nzima (al. 8)

3. “Masombo hufungwa kama walau mtu ametia kitu mdomoni. Pamoja na hali ngumu iliyopo, bado hatujafikia pa kukosa mlo wa kimsingi. Ndiyo hatumudu viliwa vya samli lakini hatuwezi kuishi kana kwamba tunazongwa na njaa. Tazama ulivyokonda unaelekea kushindana na ng’onda. Hii nafasi ya ng’onda unaitaka kwa nini?

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)
b) Tambua mbinu mbili za kimtindo zilizomo kwenye dondoo hili. (al. 2)
c) Bainisha sifa nne za msemewa (al. 4)
d) Jadili namna msemaji amechangia katika kuendeleza
i) Ploti (al. 5)
ii) Maudhui
e) Kwa kurejelea Tamthilia ya Bembea ya Maisha, jadili maudhui ya ukengeushi (alama 5)

**SEHEMU YA C: CHOZI LA HERI (Assumpta K.Matei)**
**Jibu swali la 6 au 7**

6. “<u>Amani iwe nanyi.</u>’’
“Iwe pia nawe.’’

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Onyesha kinyume kinachojitokeza katika kauli iliyopigiwa mstari kwa kurejelea riwaya nzima. (alama 16)

**AU**

7. Vijana ni mhimili katika jamii. “Tetea kauli hii kwa kurejelea Riwaya ya Chozi la Heri. (alama 20)

**SEHEMU D: USHAIRI**
**Jibu swali la 6 au la 7**

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali
Said A. Mohamed: Mbeleya Safari

Ilipoanza safari, ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

Njaa ikawa thabiti, na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati, tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti, dhila na mingi mikiki
Tulijizatiti.

Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari, utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari, juhudi iliyobaki
Tulijizatiti.

Ile ilikuwa ndoto, mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto, sahala ‘mmekuwa dhiki
Wagombania kipato, utashi haukatiki
Na kutabakari.

www.freekcsepastpapers.com

Msafara ukasita, kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita, mlima haupandiki
Basi soe 'kajipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina.

Tukiwa migongo wazi, tukainama kwa shaki
Tukawa'chia ukwezi, kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi, kuteremsha miliki
Wakaitapia.

Wakafikia makazi, ya pumbao na ashiki
Huko wakajibarizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma uliomiliki
Mbele ya safari.

Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema mate, kwa umati halaiki
Imezima nia yote, kiza hakitakasiki
Mbele ya safari.

**MASWALI**

a) Eleza safari inayorejelewa katika shairi hili (al. 2)
b) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa (al. 3)
c) Taja na ueleze Bahari mbili za shairi hili ukizingatia: (al. 2)
i) Kibwagizo
ii) Vina
d) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya tutumbi (al. 4)
e) Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita. (al. 2)
f) Bainisha aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili (al. 2)
g) Fafanua aina mbili za taswira zinazojitokeza katika shairi hili (al. 2)
h) Kando na kinaya, bainisha vipengele vingine viwili vya kimtindo katika shairi hili (al. 2)
i) Eleza toni ya shairi hili (al. 1)

**AU**

7. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tilichinja ili uwe mwanamume,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu!
Iwapo utatingisa kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu
Ndege zote ziangamie.

www.freekcsepastpapers.com

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,
Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa.
Iwapo wewe ni mme,
Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri.

<u>Maswali</u>

a) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha (al. 2)
b) Tambua anayeimba na anayeimbiwa shairi hili (al. 2)
c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume (al. 2)
d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili (al. 4)
e) Taja shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili (al. 2)
f) Eleza mbinu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi (al. 4)
g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili? (al. 4)
i) Mbari
ii) Msununu
iii) Ngariba

**SEHEMU E: HADITHI FUPI.**

6. *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi nyingine*.

Hata hivyo, alionekana kama mwanamke wa umri wa makamo. Shida na madhila aliyopitia yalimkomaza kiakili na kimwili. Majukumu aliyotwikwa katika boma la mjomba wake yaliifanya ngozi yake kuota kea na makunyanzi. Dunia iliamua kumnywesha shubiri pindi tu alipozaliwa. Mamake Nyaboke alimzaa akiwa mwanafunzi wa kidato cha pili.Pindi tu alipojifungua, Nyaboke alikatiza masomo yake akaanza kazi ya ulezi, kazi ni kulea mwana! Wazazi wake walikata tamaa ya kupata maisha mazuri kwa sababu binti walimtegemea kusoma hadi chuo kikuu alikomea kidato cha pili. Janadume lililofaa kuitwa babake Sabina lilimkana Nyaboke mchana kweupe. Sabina akaelekea kukosa malezi ya baba mzazi tangu hapo.

a) Fafanua mbinu za kimtindo katika kifungu hiki. (al. 12)
b) Fafanua maudhui ya malezi yanavyojitokeza katika hadithi hii. (al. 8)

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA SUKELLEMO**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**MUDA: SAA 1¾**

***MAAGIZO***

*a)* *Andika insha* ***mbili****. Insha ya* ***kwanza*** *ni ya* ***lazima.***
*b)* *Kisha chagua insha nyingine* ***moja*** *kati ya hizo tatu zilizobakia.*
*c)* *Kila insha isipungue maneno* ***400****.*
*d)* *Kila insha ina alama* ***20****.*
*e)* *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

1. Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa na Waziri wa Elimu kuchunguza njia mbalimbali za udanganyifu katika mitihani ya kitaifa. Andika ***kumbukumbu*** za mkutano uliofanyika kuwasilisha uchunguzi huo.
2. Serikali ndiyo ya kulaumiwa kutokana na kupanda kwa gharama ya maisha nchini Kenya. Jadili.
3. Andika kisa kitachodhihirisha maana ya methali ifuatayo: **Mchuma janga hula na wa kwao**
4. Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo.
   Mahakama ilikuwa imejaa furifuri. Jamaa na marafiki walikuwepo. Nilisimama kizimbani. Mashahidi walikuwa wamekamilisha kutoa ushahidi wao. Jaji aliinua uso wake akaniangalia kwa ukali kisha…

---

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA SUKELLEMO**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**LUGHA**
**MUDA: SAA 2½**

**1. UFAHAMU (Alama 15)**
**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu.

Msingi mkuu wa uainishaji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na Jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na Jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya kipindi cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mahali mwa kazi, washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii wanaoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila kuhajiri, uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini.

Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghosi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani.

Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia ya aina hii kama ya mpito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususan pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na uhusiano wa 'chembe chembe.' Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachoshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzako. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia na kadhalika.

Mahusiano ya aina ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisiasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiwa, ameibiwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusiana vipi na Jamaa zetu, marafiki zetu majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

**Maswali**

(a) Taja kigezo cha kuzungumzia mahusiano. (al. 1)
(b) Eleza imani ya watu kuhusu mahusiano ya watu. (al. 1)
(c) Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. (al. 2)
(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. (al. 4)
(e) Taja sifa kuu za mahusiano ya muda mfupi. (al. 2)
(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (al. 2)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (al. 3)

a. inasigana
b. yameghoshi
c. vighairi

**2. UFUPISHO (Alama 15)**

***Soma kifungu kisha ujibu maswali***

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekekana kusema kuwa uchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea wenzo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti kuyaendesha, kuyatawala na kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ambaye ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanaweza kuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha maarifa mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu mmoja huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza

www.freekcsepastpapers.com

kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu hawezi kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo mzito wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia za ishara au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishwa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa kwa mfano, kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambamba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana. Kwa mfano, neno ‘mwerevu’ huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa ‘mjinga’, mjanja’, mjanga’, ‘hodari’ na kadhalika.

Maarifa huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu, ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kudhibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapo mfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe, ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za uenezaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

(a) Fupisha aya ya pili na ya tatu kwa maneno 55-60. (al. 6)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

(b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane kwa maneno 100 - 110. (alama 8, 1 mtiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

(a) Andika maneno yenye miundo ifuatayo. (al. 2)

i. Kizuiwa ghuna cha midomo, kiyeyusho cha midomoni, irabu ya kati chini, kilainisho ambacho wakati wa kutamka hewa hutambaa kinywani na irabu ya kati nyuma.

ii. Nazali ya ufizi, kipasuo ghuna cha kaakaa laini, irabu ya nyuma juu, kimadende cha ufizini na irabu ya mbele juu.

(b)

(i) Eleza maana ya sauti mwambatano. (al. 1)

(ii) Andika mfano mmoja wa sauti mwambatano inayotamkiwa ufizini. (al. 1)

(c) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika wakati uliopita, hali isiyodhihirika. (al. 1)
Mkurugenzi anawaamuru wafanyikazi katika kampuni yake.

(d) Andika neno lenye mofimu zifuatazo. (al. 3)
Nafsi ya tatu wingi, njeo, kielezi cha namna kinachojengwa kwa silabi moja, yambwa, kauli tenda. (al. 3)

(e) Tunga sentensi moja yenye mpangilio ufuatao wa maneno: (al. 2)
Nomino ya kitenzi jina, kivumishi cha kuashiria cha wastani, kivumishi cha pekee chenye dhana ya bila kusaza, na kitenzi halisi.

(f) Andika ukubwa wa sentensi ifuatayo katika hali ya ukanusho. (al. 1)
Mbwa wenye ukali walimfukuza mtoto.

(g) Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kuwa kitendo kilifanikiwa kutokana na kufanikiwa kwa kitendo kingine. (al. 1)

(h) Andika katika wingi. (al. 1)
Ukwato uo huo ulimsaidia kutambua kondoo wake.

(i) Andika sentensi hii upya ukianza na yambiwa. (al.1)
Mbunge wa Mtondo aliwajengea watu wake hospitali sita mwaka uliopita.

www.freekcsepastpapers.com

(j) Andika sentensi zenye vipashio vifuatavyo. (al. 3)

i. Yambwa tendwa ambayo ni kirai nomino

ii. Kishazi tegemezi ambacho ni chagizo ya wakati

iii. Kirai kihusishi ambacho ni kielezi cha mahali.

(k) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo ukizingatia maneno yaliyopigigwa mstari. (al. 1)

Mvua ilinyesha wageni walipofika.

(l) Eleza matumizi ya kiambishi na neno lililopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo. (al. 2)

Mtahiniwa alijisuta baada ya kupata alama tano kwa ishirini.

(m) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. (al. 3)

Yalijaa yakamwagika.

(n) Onyesha miundo yoyote miwili ya ngeli ya KI-VI. (al. 2)

(o) Andika katika usemi halisi. (al. 3)

Mkufunzi alishangaa na kutaka kujua kama Awiti ndiye aliyekuwa amemwibia mwenzake siku iliyotangulia.

(p) Andika sentensi yenye muundo ufuatao. (al. 2)

$KN - (\overline{S}) + KT\ [(Ts + Ts + T + RE(E+E)]$

(q) Nyambua vitenzi hivi katika kauli ambayo hutoa dhana ya kinyume bila kubainisha mtendaji. (al. 2)

i. fuma

ii. shona

(r) Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi cha Kibantu na kihusishi cha mtenda. (al. 2)

(s) Ainisha sentensi ifuatayo kiuamilifu. (al. 1)

Jibu maswali yote katika sentensi hii.

(t) Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha maneno yaliyopigiwa mstari kuwa nomino. (al. 3)

Mchoraji alichora picha hiyo vizuri akawafurahisha watalii.

(u) Mama ni kwa nina na akali ni kwa …………….. na dua ni kwa ………………… (al. 2)

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

Wewe ni wakili katika kesi ya jinai inayoendelea katika Mahakama ya Haki na Uwajibikaji. Hata hivyo, umegundua kuwa hadhira haijamakinika kukusikiliza. Fafanua sifa za lugha utakayotumia ili hadhira imakinike. (alama 10)

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA SUKELLEMO**
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**
**MUDA: SAA: 2.30**

**Maagizo**
a) Jibu maswali manne pekee
**b)** Swali la **kwanza** ni la **lazima.**
**c)** Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki (**hadithi fupi,tamthilia riwaya na fasihi simulizi)**
d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

SEHEMU A: **USHAIRI**
**1. LAZIMA**

Naikumbuka,
siku nilipofika kijijini
na kumkuta nyanya kaketi chini ya,
mgunga unaolekeana na machweo,
akisaga ugoro wake
na
kuyaangalia machweo,
akiwasikiliza nyuni waliokuwa,
wakiimba kwa msisimko
kuyaomboleza matanga ya
magharibi.
Naikumbuka kauli yake,
'itakuwa lini nasi kuomboleza
Kifo cha dhiki?

Naikumbuka sauti ya
mama alipokuwa akiwinga
bundi aliyekuwa akiimba
mbolezi kuucheka umaskini
kuudhihaki uwezo duni wa wanakijiji.
Naikumbuka sauti ya mama
Na swali lake:
'Lini nasi tutawaimbia watutesao
mbolezi za bundi?

Naikumbuka siku niliposikika,
kilio alichokilia ndugu;
kidole ki lipokatwa na mashine
ya kutengenezea karatasi
Sauti yake akilalamika,
kutolipwa fidia na chozi,
la kufutwa kazi kwa kutozalisha,kama kabla.
Ndio na swali lake:
'Lini itakatwa mirija ya
wanyonyaji wafanyao watu mashine?

Naukumbuka ukwenzi,
alioupiga falahi na mkulima,
aliyepokea pesa ukufi kwa,
mazao yaliyomlaza nje na kumvunja,
mgongo akalala hoi,
nayakumbuka machozi yake ,

www.freekcsepastpapers.com

yaliyotiririka na kumkamua
nguvu akitoa lawama zilizotoka kwa shida
nililisikia swali lake:
'Lini jasho la upanzi na mavuno
litawafaidi wachomwa na jua?'

(a) "Shairi hili linakatisha tamaa.'' Thibitisha kauli hii kwa mifano mitatu kutoka kwenye shairi. **(alama 3)**
(b) Fafanua umuhimu wa aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 2)**
(c) Bainisha nafsineni katika shairi hili. **(alama 2)**
(d) Jadili umuhimu wa maswali ya balagha katika shairi hili. **(alama 2)**
(e) Tambua toni ya shairi hili. **(alama 1)**
(f) Bainisha na uoneshe umuhimu wa mistari ifuatayo katika shairi hili.
(i) Mistari kifu **(alama 2)**
(ii) Mistari mishata **(alama 2)**
(g) Bainisha aina mbili za taswira zinazojitokeza katika shairi hili. **(alama 2)**
(h) Fafanua muundo wa shairi hili . **(alama 4)**

SEHEMU YA B
**HADITHI FUPI**
**Jibu swali la 2 au 3**
**2. D.W .LUTOMIA : *Msiba wa kujitakia***
**Wetu ni wetu, hata akiwa mbaya …ni wetu.hatuna budi kuchagua yeye. Lisilobudi hubidi.**
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
(b) Fafanua vipengele vya kimtindo katika dondoo hii. **(alama 4)**
(c) Hiari ya maamuzi ya wahusika mbalimbali yamewaletea madhila anuwai.jadili. **(alama 12)**

AU
3. **YUSSUF SHOKA HAMAD: *Mzimu wa Kipwerere***
**"Mbali na vitisho vya aina hii, mzimu wa kipwerere ulikuwa na miiko yake"**
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
(b) Fafanua sifa za msemaji wa maneno haya. **(alama 4)**
(c) Jadili miiko ya mzimu wa kipwerere kwa mujibu wa hadithi. **(alama 4)**
(d) Dondoa vitisho vinavyorejelewa kwa mujibu wa hadithi. **(alama 8)**

SEHEMU YA C. **BEMBEA YA MAISHA (Timothy M.Arege)**
**Jibu swali la 4 au 5**
**4 "Lakini nilivyosema, mungu hamwachi mja wake.."**
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
(b) Tambua sifa tatu za msemewa. **(alama 3)**
(c) Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kukuza vipengele vifuatavyo.
(i) Ploti **(alama 4)**
(ii) Maudhui **(alama 4)**
(d) Kwa kurejelea tamthilia nzima eleza ukweli wa kauli "mungu hamwachi mja wake". **(alama 5)**

AU
(5) **Ukilazwa tayari unakuwa umeonja seli.Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema. Amri na vitisho kama askari.Unashindwa kama uuguze moyo ama ugonjwa.Katika wodi hewa iliyojaaa harufu ya dawa imezagaa, vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura.Yaani hali nzima haikupi matumaini ya kutoka ukiwa bora.matumaini yanadidimia. Tumaini lako unaliweka katika sala.**
(a) Tambua toni mbili katika kifungu hiki **(alama 2)**
(b) Tambua aina moja ya taswira katika dondoo hili **(alama 2)**
(c) Kando na taswira chambua vipengele vingine vya kimtindo **(alama 6)**
(d) Fafanua namna mandhari ya dondoo hili yalivyochangia kujenga tamthilia ya bembea ya maisha **(alama 10)**

www.freekcsepastpapers.com

SEHEMU YA .D

**CHOZI LA HERI (Assumpta K.Matei)**

**Jibu swali la 6 au 7**

6. "**<u>Amani iwe nanyi.</u>**"
**"Iwe pia nawe."**

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b) Onyesha kinyume kinachojotokeza katika kauli iliyopigiwa mstari kwa kuwarejelea wanaolengwa na maneno haya. **(alama 16)**

AU

7. **"Wanawake ni viumbe wa kushangaza sana.Ya nini kuilea mimba kisha kuja kutupa matokeo?"**

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b) Eleza umuhimu wa anayeambiwa maneno haya kuijenga riwaya hii. **(alama 4)**

(c) Kwa kurejelea riwaya hii ,onyesha mchango wa wanawake katika kuzoroteka kwa Maisha yao **(alama 12)**

SEHEMU YA E

**FASIHI SIMULIZI**

Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali

Heri ujue mapema
Nasaba yetu haina woga
Woga haumei kwetu, humea kwa kina mamaku.
Tulichinja jogoo na fahali ili uwe mwanaume.

Ah! kisu cha ngariba ni kikali ajabu.
Iwapo utatikisa kichwacho.
Uhamie kwa wasotabiri,
Ama tukwite njeku.
Mpwangu kumbuka hili,
Wananume wa mlango wetu
Si waoga kwa kisu
Wao hukatwa mchana hadi usiku
Wala hawalalamiki.

Siku nilipokatwa
Nilisimama tisti
Nikacheka ngariba kwa tashtiti
Halikunitoka chozi.

Iwapo utapepesa kope
Wasichana wa kwetu na wa mbali
Wote watakucheka
Ubaki ukinuna.

Sembe umepokea
Na supu ya makongoro ukabugia
Sema unachotaka
Usije kunitia aibu

**Maswali**

(a) Taja na uthibitishe shughuli zozote za jamii ya wimbo huu. **(alama 4)**

(b) Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anawaimbia nani? **(alama 2)**

(c) Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha. **(alama 2)**

(d) Mwimbaji wa wimbo huu ana taasubi ya kiume .Thibitisha kauli hii. **(alama 2)**

(e) Eleza wajibu wa nyimbo katika jamii. **(alama 6)**

(f) Ijapokuwa nyimbo ni nzuri, zina ubaya wake.Thibitisha kauli hii . **(alama 4)**

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA MECS**
***Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya***
**102/1**
**KISWAHILI**
**Insha**
**Karatasi ya 1**
**Muda: SAA 1¾**

**MAAGIZO:**
- *Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya **lazima**.*
- *Kisha chagua insha **moja** nyingine kutoka hizo **tatu** zilizobaki.*
- *Kila insha isipungue Maneno **400**.*
- *Kila insha ina alama **20**.*

1. **SWALI LA LAZIMA.**
Shuleni mwenu kumekuwa na visa vingi vya matumizi ya mihadarati. Wewe ni katibu wa chama kilichobuniwa kuchunguza sababu za wanafunzi wengi kutumia mihadarati- Chama cha Wapekuzi.
Andika kumbukumbu za mkutano ulizoandika kuhusu sababu za vijana wengi kutumia mihadarati nchini.
2. Teknolojia ya kisasa ni kama sarafu yenye sura mbili; ina faida na hasara. Jadili.
3. Tunga kisa kitakachooana na methali ifuatayo;
Asante ya punda ni mateke.
4. Andika kisa kitakachomalizia kwa maneno yafuatayo;
...nilipozinduka kutoka usingizini, nilijipata bado nikiwa katika hali yangu ya umaskini hohehahe. Kumbe ilikuwa ni ndoto!

---

**MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA MECS**
***Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya***
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
**Lugha.**
**Muda: Saa 2 ½**

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**
***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Zamani wanadamu wa kwanza ambao ni mababu wa vizazi vingi vilivyopita waliishi duniani. Habari kuhusu maisha na maumbile yao haikujulikana kwa hakika kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kuandika. Lakini mara kwa mara shughuli za wanaakiolojia kama Louis Leakey na wengine hugundua mifupa yao ardhini na michoro yao katika mapango. Wataalamu hawa hufukua mafuvu, vyombo na silaha zao za zamani. Kwa kuchuguza vitu hivi tunaweza kubahatisha viumbe hawa walivyokuwa na jinsi walivyoishi.

Moja ya mambo yanayofahamika sasa ni kuwa wanadamu hawa wa awali walifanana na sokwe. Aidha, walitembea kwa kupinda mgongo kama kibiongo. Chakula na uhai wao ulitegemea kukusanya matunda, kokwe, majani ya miti na mayai ya ndege. Vilevile, walitegemea wanyama wadogo, kufukua mizizi na kubambua magamba ya miti **walipokabwa** na njaa.

Maisha yao yalikuwa ya hatari. Walikuwa wakiwindwa na wanyama wakubwa. Hii ni kwa sababu mwanzoni hawakuwa na silaha za **kujihami**. Hivyo iliwabidi kujificha katika miti na vilima kuepuka uvamizi. Lakini usalama wao ulitegemea kwa kiasi kikubwa kudura za Mungu au pengine miungu.

Kwa taratibu wanadamu hawa walijifunza kutengeneza silaha. Walianza kwa kutumia fimbo nene zenye ncha au mawe ya kutupia. Baadaye walichonga mawe ili kufanya kuwa visu, nyundo au vigumba vya mikuki. Hatimaye, walivigomoa au kupasua vipande vya mawe na kuvitumia kama mishale. Hapa ndipo walipoanza kuwinda wanyama wakubwa mithili ya swara, nguruwe, nyati na ngiri. Pia waliweza kutumia mikuki kudunga samaki majini.

www.freekcsepastpapers.com

Mababu zetu hawakuwa na nyumba. Kwanza walikuwa wakijisitiri kwa kukaa chini ya vivuli vya miti au kujenga vibanda vya matawi na majani ya miti. Hawakuweza kuingia mapangoni asilani kwa kuchelea wanyamapori wakali kama chatu, simba na mamba waliokaa humo. Kwa bahati, siku moja mmoja wao aligundua moto alipokuwa akipekecha vijiti. Kabla ya ugunduzi huu, wao pia hawakujua kazi ya moto na walikuwa wakiogopa na kukimbia moto jinsi wafanyavyo wanyama wa mbugani mpaka leo.

Ujuzi wao wa kutumia moto ulileta mabadiliko makubwa. Baada ya hapo waliweza kukaa mapangoni na kukoka mioto milangoni mwa mapango ili kuwaogofya adui. Hali kadhalika, waliweza kuota moto, kumulikia **maskani** yao mapya na kuchoma nyama badala ya kuila mbichi.

Wanadamu wa awali hawakuwa na mavazi. Waliwezaje kuzuia baridi? Inadhaniwa kwamba nywele nyingi walizokuwa nazo kwenye mwili zilisaidia kuwapa joto. Uvaaji wa nguo ulianza walipoanza kutumia ngozi kutoka kwa wanyama waliowawinda. Walizisafisha ngozi kwa kuzipaa kwa kombe za mawe na kuzianika juani. Zilipokauka walizifunga na kuzishikanisha kwa mifupa au mikanda ya ngozi.

Wanadamu hawa hawakuweza hata kuongea. Waliwasiliana kwa kupiga mayowe, kutoa milio au kuguruma jinsi wafanyavyo wanyama. Polepole walianza kutumia sauti na baada ya muda walipanga sauti kuibua mfumo wa maneno yenye maana za kipekee. Umilisi wa kutumia lugha uliwawezesha kupiga hatua kubwa kimaendeleo. Lugha pamoja na matumizi ya moto na silaha viliwarahisishia maisha na kuwawezesha kupata muda wa kupumzika mapangoni jioni wakiota moto. Kutokana na hali hii waliweza kutekeleza jambo moja kuu waliloturithisha. Walitupokeza Sanaa. Kutoka kwao tulirithi fasihi simulizi na kupata nakshi za michoro yao kwenye mapango. Michoro hii inapatikana katika mapango hata leo hii nchini Ufaransa, Uhispania, Afrika Kusini na hata Afrika Mashariki.

www.freekcsepastpapers.com

**<u>Maswali</u>**

a) Msemo "Kudura za Mungu au pengine miungu" inadhihirisha hali gani ya wanadamu wa kwanza. (alama 2)

b) Kwa nini wanadamu hawakuishi mapangoni mwanzoni? (alama 1)

c) Fafanua mambo **matano** yaliyomwezesha mwanadamu wa kwanza kupiga hatua kimaendeleo. (alama 5)

d) Taja sifa zilizotofautisha wanadamu wa awali na wa siku hizi? (alama 2)

e) Eleza maana ya? (alama 3)

i) walipokabwa ........................................

ii) kujihami ........................................

iii) maskani ........................................

**2. UFUPISHO** **( ALAMA 15)**

Uwazaji tunduizi ni tendo ambalo huhusisha matumizi ya akili. Uwazaji huu umekitwa kwenye matumizi ya michakato kama makini, upangiliaji, uteuzi na tathmini. Hata hivyo, uwazaji huu si mchakato mwepesi bali ni mchakato changamano.

Mchakato wa uwazaji tunduizi unahusisha stadi na mikabala tofauti. Mathalan, kuweza kutambua na kubainisha misimamo ya watu wengine, hoja wanazozua na uamuzi waliofikia kutathmini au kupima ushahidi uliopo ili kubainisha mitazamo tofauti. Vilevile, uwazaji tunduizi hushirikisha kupima hoja za upinzani na ushahidi uliopo kwa njia ya haki pamoja na kutambua yaliyofichwa au ukweli uliofunikwa na taswira ya juu juu. Hali kadhalika, uwazaji tunduizi hujumisha kutambua mbinu zinazotumiwa kufikia misimamo fulani kwa mvuto zaidi na kwa matumizi ya mbinu za kishawishi. Aidha, uwazaji huu huhitaji kutathmini masuala kwa mtindo ulio wazi, kufikia uamuzi kama hoja zinazotumiwa zina mashiko au zinakubalika kuwa nzuri. Zaidi ya hayo, uwazaji tunduizi unahusisha kuwasilisha mtazamo kwa njia yenye uwazaji mzuri na inayoshawishi.

Uwazaji tunduizi una manufaa anuwai. Mosi, unasaidia kujenga makini ya utendaji. Pili, hupevusha uwezo wa usomaji kwa kuufanya usomaji huo uwe na malengo wazi. Fauka ya hayo unamsaidia mtumiaji kutambua hoja kuu katika matini au ujumbe fulani ya kuzongwazongwa na hoja duni za pembeni. Uwazaji huu unasaidia kuuchonga uwezo wa kuikabili au kuiitikia hali fulani na kukuza stadi za uchanganuzi. Mwanadamu huwa mtu tofauti na bora anapoujenga na kuuimarisha uwazaji tunduizi wake.

***<u>Maswali</u>***

a) Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi, fupisha aya mbili za mwanzo. (maneno 70-80) (alama 8, 1 utiririko)

***Matayarisho /*** **Jibu**

b) Andika kwa muhtasari mambo muhimu katika aya ya tatu. (maneno 35-40) (alama 5, 1 ya utiririko)

**Matayarisho / Jibu**

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Tofautisha sauti zifuatazo. (alama 2)
i) /ny/ na /m/
ii) /a/ na /u/

b) Andika neno lenye muundo ufuatao wa silabi. (alama 1)
K-KKI

c) Ainisha nomino katika sentensi hii.
Kuuza sukari kwa Rehema kulimfanya awe na utajiri. (alama 2)

d) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika hali yakinishi.
Mtoto hakupatiwa chakula wala nguo. (alama 1)

e) Kwa kutoa mifano, ainisha aina mbili za mofimu. (alama 2)

f) Andika katika hali ya ukubwa wingi. (alama 2)
Mwanamke alibeba kiti chake.

g) Ainisha yambwa katika sentensi hii. (alama 3)
Mtoto alipikiwa chakula kizuri kwa mwiko.

h) Tunga sentensi yenye kivumishi cha pekee chenye dhana ya kutojali. (alama 2)

i) Kwa kutunga **moja** sentensi tofautisha kati ya vitate hivi. (alama 2)
Mzazi na msasi.

j) Eleza maana ya kiambishi **"ji"** katika sentensi hii.
Mcheza**ji** ali**ji**kata kwa kisu. (ala1)

k) Taja ngeli za nomino zifuatazo. (alama 1)
Kiwete
Maji

l) Tunga sentensi ukitumia neno **vile** kama **kitenzi** na **kivumishi**. (alama 2)

m) Ainisha virai tofauti katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Mwalimu yule mzuri sana alikuja darasani mapema sana.

n) Onyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo; (alama 2)
i) kibainishi
ii) vifungo

o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. (alama 4)
Kitabu kilichonunuliwa ni hiki.

p) Sahihisha kwa njia mbili tofauti. (alama 2)
Mwanafunzi alifika katika nyumbani

q) Eleza maana ya nahau **kula mwata**. (alama 1)

r) Tambulisha hali katika sentensi hii. (alama 1)
Mtoto acheza.

s) Andika kulingana na maagizo. (alama 2)
Mtoto alipoenda Mombasa alijawa na furaha. (anza kwa: Kwenda…)

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

a) Umeteuliwa Kama mtangazaji wa mashindano ya michezo baina ya shule katika eneo gatuzi ndogo lenu. Eleza sifa tano za lugha utakayotumia. (alama 5)

b) Jadili mambo matano yanayoathiri matumizi ya lugha katika jamii. (alama 5)

www.freekcsepastpapers.com

**<u>MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA MECS</u>**
***<u>Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya</u>***
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**

***MAAGIZO:***
a) Jibu maswali **manne** pekee.
b) Swali la **kwanza** ni la **lazima.**
c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.
d) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili

**SEHEMU A: SWALI LA LAZIMA (ALAMA 20)**
**1. USHAIRI**
**<u>UTU NI NINI?</u>**
Utu na ubinadamu, ni kama yai na kuku
Utu ni ile nidhamu, *mola aliyokhuluku,*
Ubinadamu ni damu, ya utu wa kila siku,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Ye yote mwanaadamu, ana asili ya utu,
Ya'ni kwenye yake damu, hakikosi hiki kitu,
Utu sifa maalumu, ya mtu kuitwa mtu,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu ni kiumbe hai, tunacho chaonekana
Utu kamwe haudai, tabia ya kujivuna,
Utu ni ule uhai, ushikao uungwana,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu huweza pimika, kwa hisia ya akili,
Huweza kuhifadhika, kulingana na *fadhili,*
*Utu huweza pendeka, palipo na maadili*
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu unayo aibu, na *tabia ya muhali*,
Utu huenda na jibu, la Imani na ukweli,
Utu huiona tabu, tabia ya ujahili,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Filosofia ya utu, inapinga ubinafsi,
Utu hautaki kitu, cha upeke wa nafsi,
Utu hauna kiatu, cheupe au cheusi,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Utu wa kweli kwa *mja*, ni wenzake kuwajali,
Utu huiona haja, ya kujua watu hali,
Utu ni kuwa pamoja, kwenye shida mbalimbali,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Utu ni ubinaadamu, udugu na wenzi wako,
Utu wote waheshimu, kwa nidhamu na kicheko,
Utu ona mwanadamu, sijitenge peke yako,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

www.freekcsepastpapers.com

Ingawaje tu dhaifu, katika ubinafsi,
Utu kweli nausifu, ubinadamu halisi,
Utu ni sifa tukufu, iletayo kila *nemsi*,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

a) Tambua aina ya shairi hii kwa kutolea ithibati. (alama 2)
b) Taja sifa tano za mtu mwenye utu kulingana na shairi. (alama 5)
c) Tambua mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwa na mshairi. (alama 2)
d) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 3)
i) vipande
ii) vina
iii) mpangilio wa maneno
e) Tambua nafsineni katika shairi. (alama 1)
f) Tambua mbinu tatu alizotumia mshairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)
g) Andika ubeti wa saba kwa lugha nathari. (alama 4)

**SEHEMU B: RIWAYA,**
**A Matei: Chozi la Heri**
**Jibu swali la 2 au la 3**

2. Jadili mchango wa wazazi na walezi katika kusambaratisha familia katika riwaya ya Chozi la Heri (alama 20)

***Au***

3 Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua...Mawingu yaliyoshiba yakataka kutapika yanagooka, yanakaribiana, kupigana busu na kusababisha mwanguko wa matone mazito ya mvua; matone yanayoanguka kwenye ngozi laini zą wanangu wakembe... ubavuni mwangu amelala maskini mke wangu... Sijui kama inahalisi kumwita mke wangu.... Siye, siye, siye-e-e-e. Tazama uso wake ulivyovamiwa na majeraha kikwi... Amevimba na kuvimbiana kama dongo la unga ngano baada ya kutiwa hamira. Lakini yeye hana la hamira!

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Jadili aina ***nne*** za taswira katika dondoo hili (alama 4)
c) Bainisha vipengele vingine **vinne** vya kimtindo katika dondoo hili (alama 4)
d) Bainisha toni ya dondoo hili. (alama 2)
e) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili (alama 6)

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU C. TAMTHILIA**
**T. Arege: Bembea ya Maisha**
**Jibu swali la 4 au la 5**

4. "... wakati mwingine mwindaji huwa mwindwa. Hata kijijini wanaishi watu . Watu hao hawakumbwi na dhiki kiasi hiki. Ya nini kung'ang'ana kuyatafuta maisha kama kwamba hayapiti? Maisha ni mshumaa uso mkesha! Ukijiachia sana peupe hata upepo unaweza kuuzima kabla ya kulika hadi nchani."

**Maswali**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama. 4)
b) Bainisha toni katika kauli hili (alama. 2)
c) Eleza vipengele **vinne** vya kimtindo alivyotumia msemaji kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. (alama. 4)
d) Eleza umuhimu wa msemaji katika kuendeleza ploti ya tamthilia hii. (alama 10)

***Au***

5. (a) Fafanua umuhimu wa mazungumzo kati ya Luka, Beni na Yona katika kujenga tamthilia ya "Bembea ya Maisha" (alama 10)
(b) "Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa michezo.Huungwa na mchezo kuanza tena." Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutolea mifano mwafaka tamthiliani. (alama. 10)

**SEHEMU YA D**

**Hadithi Fupi – Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine – Dw Lutomia**

***Jibu swali la 6 au la 7***

***Kifo cha Suluhu***

6. Mume wangu, hebu zivute fikra zako miaka kumi na mitano iliyopita tulipoingia katika mkataba wa ndoa. Kwa nini unataka kujitia hamnazo kuhusu ahadi ulizozitoa? Umesahau namna tulivyohangaika, tukachekwa na watu, tukakosa hata marafiki na hatimaye tukabandikwa majina ya ajabu? Umesahau, mume wangu? Umesahau namna kazi yako ya kuuza makaa ilivyofika hatima ya ghafla baada ya serikali kupiga marufuku ukataji wa miti katika eneo la Dafrao? Naomba ukumbuke. Ninaamini huenda umesahau! Ama cheo chako cha ubunge ulichokipata kwa mbinu nizijuazo mimi kimekulevya na kukufanya uisahau familia yako?

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 5)

b) Fafanua mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. (alama 6)

c) Tambua toni iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)

d) Fafanua umuhimu wa ujumbe alitoa mnenaji wa maneno haya. Tumia hoja nane. (alama 8)

**Au**

7. **“Wewe mke sampuli gani usiyetaka kumuunga mkono mmeo?”**
Kwa kurejelea hadithi hii na nyingine zifuatazo, jadili changamoto anazopitia mnenewa pamoja na wahusika wa jinsia yake. (alama 20)

***Ahadi ni deni.***

***Hadithi ya Nipe nafasi***

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

**8. Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali**

Hapo zamani za kale, Nyani na Mamba walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Watoto wao walipendana na kufaana kama ndugu wa toka nitoke. Familia ya Mamba aliishi mtoni nayo ya Nyani aliishi katika msitu uliokuwa maili thelathini kutoka mtoni. Kila mara marafiki hawa walitembeleana na kusaidiana kwa hali na mali. Kwa vile Mamba alikuwa mvuvi msahuhuri, aliweza kumwauni Nyani na aila yake kwa samaki wa aina mbalimbali. Nyani naye alimpelekea Mamba matunda na nafaka kutoka shambani mwake.

Urafiki wao ulikita mizizi na kunawiri Zaidi wakati Mamba alipokuja kwa Nyani kumposea mwanawe binti. Ukwe uliutilia viungo uhusiano wa Nyani na Mamba wakawa wanagandana kama kupe na mkia wa Ng’ombe. Wakatenda mengi pamoja. Wakazungumza ya kupwa na ya kujaa. Hakuna hata mmoja wao aliyeutilia shaka uaminifu wa mwenzake. Wake zao nao walifuata kaida ya maji kufuata mkondo. Walikuwa masahibu wa chanda na pete.

Msimu mmoja wa mapukutiko ulishuhudia mabadiliko ya kudumu katika maisha ya Nyani na Mamba. Wakati huo, bahari ilichafuka si haba. Kazi ya Mamba ya uvuvi ikaanza kukabiliwa na majabali ya kila aina. Kila mara Mamba alipokwenda uvuvini, alirudi akichekelewa na nyavu zake. Hakuambulia chochote. Njaa ilianza kubisha hodi katika familia ya Mamba. Hali hii ilitishia kuutia ufa urafiki kati ya Mamba na Nyani. Mamba alivamiwa na pepo ambaye hata yeye alishindwa kumfahamu. Kila mara alipomwona. Nyani au watoto wake alitamani kumdakia na kumla mzima mzima. Kadiri aalivyojaribu kujiasa dhidi ya fikira hii mbovu ndivyo moyo wake ulivyoendelea kumshauri, “Una njaa bwana, familia yako itaangamia. Je huoni rafiki yako na familia yake wanaweza kuwa kitoweo? Utaendelea kula wishwa hadi lini? Mbona huyo Nyani ambaye anajiita rafiki yako sasa amekata guu humu? Mbona haji tena kukutazama? Hata karafuu alizokuwa akikuletea ameacha kuleta. “Mamba akaanza kumshuku rafiki yake na akasadiki kuwa Nyani alikuwa mla naye tu.

Usiku mmoja baada ya kula mate na kujilaza kitandani mwake akihesabu nyota, wazo lilimjia. Alikata shauri kumlaghai rafiki yake wa miaka mingi ilia pate kujiokoa yeye na familia yake kutoka katika

www.freekcsepastpapers.com

kinamasi cha njaa. Asubuhi yake alikwenda kwa Nyani akiwa amejinamia kwa jitimai. Alisema, "Rafiki yangu, jana tulipoagana nilipata tanzia. Mjumbe kutoka kijijini aliniarifu kuwa baba yangu ni mgonjwa mahututi. Alisema kwamba baba ananitaka nyumbani upesi," Habari hizi zilimtia Nyani majonzi makuu. Alimwahidi Mamba kwamba wangeandamana pamoja. Kwa vile Nyani hangeweza kutembea majini, ilibidi abebwe na Mamba. Alipatwa na kichefuchefu na manyezi kila alipotazama bahari iliyojitandaza mbele yao kwa mbwembwe. Hata hivyo, Mamba alimhakikishia kuwa wangefika salama. Naye kwa Imani iliyotokana na urafiki na mazoea ya miaka mingi, alitulia.

Safari ilikuwa ndefu na yenye machovu yaliyomfanya Nyani kulala mgongoni mwa Mamba. Walipofika kwenye vina vya maji, Mamba aliamua kumpasulia mbarika Nyani. "Rafiki yangu, nimekuwa nikidhani wewe ni rafiki wa dhati, kumbe uzuri wako wa mkakasi? Mimi na wanangu tumetafunwa na njaa kwa miezi kadha sasa huku maghala yako yakishiba na kutapika chakula. Hujadiriki hata siku moja kuja kujua kama nimepata hata senti moja ya kusagia mkunguni. Jana usiku nilipokuwa nikiwazia hali yangu, nilioteshwa katika ndoto kwamba kama ningepata moyo wako na kuula, basi hali ya uhitaji ingeniishia. Moyo wangu unaniuma sana kukufanyia tendo hili, hata hivyo lisilo budi hutendwa."

Nyani alipigwa na butwaa nusura moyo wenyewe ujikabidhi kwa Mamba. Hata hivyo, akili yake nyepesi ilifanya kazi. Alimwambia Mamba,"Ndugu yangu, pole sana ikiwa umekuwa unadhani sikujali. Kwa kweli, hata ungeniomba moyo wangu siku hizo ningekupa tu. Unajua tena sisi Nyani, Tumbili na Kima tuna mioyo mingi. Hata hivyo, nasikitika kuwa Mungu alituambia kuwa daima mioyo yetu itakaa mitini. Basi ndugu mpenzi, badala ya kuendelea na safari hii, turudi pale mtini nikupe moyo wangu pamoja na mitatu ya wanangu kusudi uwalishe wanao na mkeo."

Mamba akaingia mtegoni. Wakarudi hadi ufuoni. Kwa vile Mamba hakuweza kutoka majini, alibaki ufuoni akimngojea rafiki yake amletee mioyo.

Mamba alitunga macho yake kwenye ujia alioufuata Nyani akiomba pasitokee lolote la kumcheleweshа Nyani. Matumbo yalimnguruma kwa njaa. Roho ikampapa kwa tumaini. Alingoja, akongoja, akangoja... wiki, mwezi, mwaka... Nyani hakurudi. Mamba akajua amepwaguliwa na Nyani. Akaapa kumtafuta kwa udi na ambari. Huo ukawa mwisho wa urafiki kati ya Nyani na Mamba.

***Hadithi yangu inaishia hapo.***

**Maswali**

a) Tambua kipera cha utungo huu. Thibitisha. (alama 2)

b) Tambua mbinu **sita** kimtindo alizotumia mtambaji wa utungo huu. (alama 6)

c) Umepewa jukumu la kutamba ngano hii. Fafanua mambo **matano** muhimu utakayozingatia ili kufanikisha uwasilishaji wako. (alama 5)

d) Fafanua umuhimu wa ngano hii katika jamii. (alama 3)

e) Kwa kutoa hoja **nne** jadili umuhimu wa maneno yaliyokolezwa rangi katika utambaji wa ngano kama hizi. (alama 4)

www.freekcsepastpapers.com

**TATHMINI YA PAMOJA YA MOKASA**
**102/1**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
**INSHA**
**MUDA: SAA 1¾**

***MAAGIZO:***

a) *Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima****.*
b) *Kisha chagua insha nyingine* ***moja*** *kati ya hizo tatu zilizobakia.*
c) *Kila insha isipungue maneno* ***400****.*
d) *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

1. **LAZIMA**
Wewe ni Mkuu wa Utumishi wa Umma na katibu wa Baraza la Mawaziri katika Gatuzi la Matopeni. Utendakazi na mienendo ya baadhi ya mawaziri hauridhishi. Waandikie Arifa/Memo ukiwaonya dhidi ya jambo hili.
2. Wewe ni msomaji wa Gazeti la Tujuzane. Andika barua kwa mhariri ukitoa maoni yako kuhusu namna mabadiliko ya hali ya anga yanavyoathiri maisha ya wananchi.
3. Tunga kisa kinachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
'Subira huvuta heri. '
4. Andika insha itakayomalizika kwa :
……….. aliangalia nyuma alikotoka lakini hakuona chochote, macho yaliingia kiwi. Ukweli ulikuwa umejiandika kila mahali alikoangaza.

---

www.freekcsepastpapers.com

**TATHMINI YA PAMOJA YA MOKASA**
**102/2**
**Kiswahili**
**KARATASI YA 2**
**Lugha**
**MUDA: SAA 2½**

**1. UFAHAMU (alama 15)**
**Soma makala yafuatayo kwa makini kisa ujibu maswali yanayofuata.**

'Hamjambo wananchi? Ni fursa kubwa kwangu kusimama hapa kwa niaba ya wachukuzi, makuli, wakulima, waashi, masonara na wengine wote wanaokandamizwa ili kufaamishana kwamba tumeamidi kugoma kuanzia kesho kutwa. Madhila yanayotusakama hayaitaji mtaalamu ili kutuchambulia. Watoto wetu wamebaki nyumbani tangu kufunuliwa kwa shule kwa sababu ya kukosa kutimiza mahitaji ya kimsingi kwa ajili ya masomo yao. Aina haja kukumbushana kuhusu adha za wenye nyumba kwa sababu ya kulimbikiziwa kodi pasi na kujali maslahi ya wapangaji. Si hanikizo la uvundo, si mrundiko wa taka, si maji taka **yaliyovavagaa**, si ukuukuu wa majengo na rangi zinazoning'inia, si maji ya kubahatisha ilmuradi hali si hali hapa. Malalamishi yetu ama yanaangukia masikio yenye nta au yaliyozibwa kwa komango. Mwisho wa mwezi hawachelewi kunyoosha mkono kudai kodi. Alfajiri unasikia **mgongo** mlangoni mradi mwezi umeisha; hawajali kwamba hujalipwa na una kibaba cha kuikimu aila yako. Milungula waliyolishwa wakuu wa kutetea maslahi ya wapangaji katika wizara ya nyumba ilifanya kazi yake barabara – hawajali, bali ukubali yote yasemwayo na wenye nyumba. Ni dhahiri kwamba tumetekwa kikamilifu – **mbele simba, mgongoni fisi'**.

Bahati alitongoa hoja zake akisikizwa kwa makini na wenzake, kisha akaendelea:

'Kule mashambani wakulima wanalazimishwa kupeleka mifugo yao kupigwa sindano maalum eti kuzuia magonjwa ambayo hawaambiwa. Ni wazi kwetu kwamba mifugo wakipigwa sindano watakufa. Hapana anayejua faida ya ng'ombe kupigwa sindano maana ng'ombe wetu wamekuwa wakiumbwa na kjiponea bila hiyo chanjo yao. Wanataka wawapige ng'ombe sindano tu ikiwa watakufa au kupona, si hoja kwao. Tumejifunza kutoka kwa majirani zetu kwamba upigaji sindano ng'ombe umeteketeza ng'ombe. Ni lazima wafugaji wachukue tahadhari katika jambo kama hili kabla ya kuharibikiwa kabisa. Kumbuka wakati ule walipotaka kujenga uwanja wa ndege waliwafurusha wakulima kutoka katika ardhi yao na

kuvunja nyumba zao. Madai yao yalikuwa kwamba wenye ardhi walipewa fidia. Hatujui ndege zinazoruka na kutua zina maslahi gani kwetu kama sio zile kelele za kuudhi masikio na kubughudhi usingizi wa wanetu?'

Mzee Gae, licha ya umri wake, alitafakari mtimani mwake kuhusu mawazo fyongo ya namna hii yaliyomdondoka Bahati kutoka kinywani bila simile. Labda kuhusu yale malalamishi ya kwanza kulikuwa na nafuu ya kukubaliana nayo lakini haya ya chanjo na uwanja wa ndege yalikuwa na taksiri hasa. Lau yangetoka kinywani mwa mzee kama yeye, msamaha ungeweza kufikiriwa. Mzee hangeweza kutabiri kama miaka iendeleavyo ndivyo binadamu anaimarika au anasambaratika kimawazo. Akiwa angali mawazoni hivi, Simali hivi, naye akadakiza usemi wa Bahati kwa hotuba yake fupi:

' Heri waache tulime mashamba yetu, ndege zibaki huko huko angani au kule zitokako!'

Stahamala za Mzee Gae zikafika mwisho sasa akaja juu kwa ukakamavu wa ghafla na kuanza …

'Simali unasahau jambo moja. Mgala muue lakini haki yake usimhini. Angatua unayoikejeli imetufaa si haba. Lile gonjwa sugu liliplipuka na kuzua taharuki, madaktari na wauguzi walifikishwa hapa haraka kwa ndege kupitia angatua hiyo. Vyakula vya msaada kwa walioathirika na njaa iliyozuka miaka mitano iliyopita, vilisafirishwa haraka kwa sababu ya kuwepo kwa miundomsingi huu. Wakati wa mafuriko yam waka jana daraja la kutuunganisha na mji mkuu lilisombwa na maji ikawa vigumu kupata mahitaji ya kila siku. Kama sio uwanja huu, nusura yetu ingetoka wapi? Mwanao aliyekuwa mtahiniwa wa mwaka jana hapa petu anaelewa jinsi uwanja huu ulivyomfaa yeye na watahiniwa wenzake vinginevyo katarasi za mitihani zingebaki huko huko kashani. Mengi yaliyowezeshwa na kuwepo kwa uwanja huu yanaonekana sio nuruni tu bali hata penye giza totoro. Ni kweli kwamba kujengwa kwa uwanja huu kulitatiza malisho na uzalishaji wa mazao ya kilimo lakini kama ilivyo ada shughuli huvunja nyngine. Binadamu yu mbioni kufanya uvumbuzi usiku na mchana ili maisha yake nay a vizazi vya usoni yawe bora zaidi. Anapovumbua kitu kilicho bora kuliko kile alicho nacho, hana budi kuvunja ili kujenga! Si lazima mbegu izikwe ndipo imee?

'Ni kweli kwamba amani haipatikani ila kwa ncha ya upanga. Hata hivyo, amani ijayo kwa njia hii ina gharama kubwa na huwaachia majeraha mengi wahusika kisha makovu yake hudumu milele. Majuto na chuki hukalia viti vya mioyo ya wahusika bila kubanduka. Makuruhu tunayokumbana nayo jinsi Bahati alivyochmbua mwanzoni yanadhihirika na kupinga kuwepo kwake ni hujuma kwa jamii yetu. Lakini katika ulimwengu wa sasa, kunazo mbinu mbadala za kuyasuluhisha. Ulimwengu mzima umesheheni visa vya mizozo baina ya jamii mbalimbali lakini wangwana hufanya vikao vya kimataifa kama njia ya kukumbatia umuhimu wa mashauriano mahali pa kushika zana za vita. Kumbuka hata sasa kuna zana bora sana za kivita zilizobuniwa lakini hakuna taifa lililo na haraka ya kuzitumia kero zinapozuka. Mgomo hautasuluhisha migogoro yetu vyema. Heri tung'ang'anie mazungumzo kwa kuwatuma wajumbe wetu kwa wakuu wetu. Hata hivyo, wajumbe **wasijihasiri** kwa kupinga swala la chanjo ya ng'ombe dhihi ya maradhi ya miguu na midomo ambayo yamefagia mifugo katika taifa jirani. Maneno hayo!'

Akatamatisha Mzee Gae na kuketi akitazamwa kwa meno na Bahati na Simali na wote waliokuwa pale. Avuliwapo nguo, muungwana huchutama.

***Maswali***

a) … "**tumetekwa kikamilifu – mbele simba, mgongo fisi**". Kwa kuzingatia hali ya wapangaji, rejelea mifano **minne** kuthibitisha ufaafu wa kauli hii. (alama 4)

b) Kwa mifano **miwili** kwenye makala, thibitisha kinaya katika hotuba ya Bahati au kinachotokea mashambani. (alama 2)

c) 'Mgala muue lakini haki yake usimhini'. Kwa kurejelea kifungu, thibitisha kauli hii kwa hoja **nne**. (alama 4)

d) Thibitisha kwamba walimwengu wa sasa wanatawaliwa na hekima zaidi ya nguvu katika kusuluhisha migogoro. (alama 2)

e) Andika visawe vya maneno haya: (alama 3)

(i) Tumeamidi …………………………………………………………………………..

(ii) Yaliyovavagaa …………………………………………………………………………

(iii) Walijihasiri …………………………………………………………………………

www.freekcsepastpapers.com

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

*Soma kifungu kifutacho kisha ujibu maswali yanayofuata*

Mataifa yanayoendelea yameathirika pakubwa na mabadiliko ya tabianchi. Hali hii imesababisha misimu mirefu ya kiangazi ambayo hatimaye yamesabisha ukame katika mataifa haya. Nchi nyingi pembeni mwa Afrika zenye maeneo kame yameitisha msaada wa dharura kwani jinamizi hili limesabisha maafa si haba. Taswira katika mataifa haya ni ya kutisha. Taarifa katika vyombo vya habari zimeonyesha mamia ya watu waliokufa kwa sababu ya ukosefu wa vyakula. Wengi wamekuwa watoto wachanga na wazee wasiojiweza. Watoto wamekuwa wakikumbwa na utapiamlo, kwani hata wakiambulia chakula hakitakuwa chenye madini mbalimbali yanayohiyajika mwilini. Utapigwa na butwaa vilevile unapoona watu waliokonda na kudhhofika kiafya. Huwa tayari wamefika mwisho na kupoteza matumaini huku wakichungulia kifo,yao imekuwa kusubiri misaada kutoka mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali.

Maji katika nyakati kama hizi za kiangazi huwa nadra kupatikana. Watu wengi hulazimika kutembea kwa kilomita nyingi angalau kupata hata kiasi kidogo cha maji. Hata baada ya kubahatika, hupanga foleni ndefu kwani watu hutegemea sehemu moja kupata maji. Hii ni kwa sababu mito mingi hunyauka na hata visima ambavyo ni vichache pia hunyauka. Maji mengine yanayopatikana huwa machafu. Kwa kuwa wakaazi hawana hiari, huishia kunywa na kuyatumia maji haya nyumbani. Hatima yake ni magonjwa yanatokana na maji machafu. Magonjwa hayo ni vile kama kipindupindu,homa ya matumbo miongoni mwa mengine. Ikumbukwe kuwa,hali katika zahanati za vijijini ni duni. Kando na haya, zahanati ni chache na zilizotengana mithili ya ardhi na mbingu. Watu wengi huaga dunia katika harakati za kutafuta huduma za matibabu ama hata kwa kukosa huduma hizo kabisa. Maelfu ya mifugo pia wamekuwa wakifa nyakati za kiangazi. Hii ni kwa kukosa lishe na pia maji. Hasara hii inatokea huku wenyeji wakikosa chakula. Mifugo wanaosalia huwa wamekondeana kama wamiliki wao. Hata kuuza ni balaa. Hali hii imekuwa si hali kwa muda sasa. Ni muhimu jambo hili liangaziwe kwa lengo la kupata suluhu ya kudumu.

Baada ya miezi mingi ya kiangazi, mvua inazuka kwa fujo. Maeneo yaleyale yanaripoti mafuriko. Msaada wa kibinadamu unaanza kuitishwa tena. Vifo vya watu na mifugo vinaanza kushuhudiwa. Maji yaliyokuwa nadra sasa yanapatikana kwa wingi kupita kiasi. Je, serikali za nchi hizi zina mipango madhubuti? Kuitisha misaada nyakati zote mbili hushangaza. Ni muhimu kuzingatia ujenzi wa mabwawa. Huu utakusanya maji yote ambayo yangesabisha maafa na kuhifadhi kwa minajili ya kutumika nyakati za kiangazi. Isitoshe, maji yayo hayo yanaweza kunyunyiziwa mimea na hivyo kuchangia pakubwa katika uzalishaji wa vyakula. Bila shaka, vifo vinavyotokana na uhaba wa vyakula vitapunguzwa na hatimaye kuzikwa katika kaburi la sahau.

Kuchimba visima vingi na kueneza nguvu za umeme pia kutaimarisha uwepo wa maji ya kunywesha mifugo na kutumika katika shughuli za nyumbani. Ni muhimu kumfundisha mtu kuvua samaki kuliko kumpa samaki kila wakati. Wananchi wafundishwe njia mwafaka za kuendeleza kilimo chenye kipato kikubwa. Huku kutawafanya kuzalisha kiwango kikubwa cha chakula. Kando na kuwafundisha ni kuwahimiza watu walio katika maeneo kame kupanda mimea inayoweza kustahimili angalau muda mrefu wa kiangazi ili isinyauke haraka. Serikali pia ziangazie upya bei ya pembejeo. Mbolea na mbegu zimekuwa bei ghali katika siku za hivi majuzi. Gharama hii imewavunja moyo wakulima wa maeneo ya nyanda za juu na yenye mashamba yenye uwezo wa kuzalisha vyakula vya kulisha maeneno mengine. Kwa sababu hii,kumekuwa hata na uhaba wa vyakula katika maghala ya serikali.

Kichwa kibaya cha ufisadi hakijakosa kupata mgao wake wa lawama katika suala hili pana la ukame na mabadiliko ya tabianchi. Viongozi wenye ushawishi serikalini wameishia kufuja pesa zinazotengewa ujenzi wa mabwawa, upunguzaji wa bei ya pembejeo na hata usambazaji wazo. Ni lazima umma na serikali ijizatiti katika vita dhidi ya ufisadi ili kuweza kuukomesha. Serikali pia iweze kuimarisha miundo msingi katika maeneno mbalimbali kwani hali duni ya miundo msingi imechangia. Barabara duni zimezuia usambazaji wa pembejeo na mavuno mashambani huku watu wakikosa chakula kicho hicho baadaye.

Ni lazima wafugaji wapate kuelewa kuwa mifugo wengi bila mipango ni hasara. Waweze kuwa na mifugo wanaoweza kuwashughulikia ili kupunguza hasara za vifo vyao wakati wa kiangazi. Wafugaji na serikali pia washirikiane kuanzisha au kuimarisha bima ya mifugo ili wafugaji wapate fidia wakati mgumu wa kiangazi na ukame. Kando na hilo, watafiti waimarisha mbegu ya mifugo wanaozaliwa kwani hili litaimarisha kipato chao. Kwa kweli, suala la madhara ya mabadiliko ya tabianchi linaweza kukabiliwa kwa kupanda miti mingi. Serikali na wananchi wapande miti katika mashamba ya serikali na ya watu binafsi. Wabinafsi wenye tabia ya kukata miti misituni ovyoovyo, hata katika chemichemi ya mito lazima wakomeshwe kwa kukabiliwa kisheria. Sheria zilizomo zitiwe shime ili kufanikisha vita hivi. Serikali, wananchi, mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali, miungano ya kimaeneo, kibara na kimataifa ikivalia njuga mabadiliko ya tabianchi na madhara yake, tutakuwa na sababu ya kutabasamu.

www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Fupisha aya za kwanza kwa maneno 80-90. (Alama 6,1 utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

b) Eleza hatua za kukabiliana na madhara ya ukame na mabadiliko ya tabia nchi kwa maneno 100-110 . (Alama 9,1 utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

**3. LUGHA (alama 40)**

a) Andika neno lenye sifa zifuatazo: Kipasuo kwamizo hafifu cha kaakaa gumu, irabu ya chini kati, kipasuo hafifu cha kaakaa laini, irabu ya mbele juu. (al. 2)

b) Dhihirisha dhima ya viambishi katika kitenzi **ukupigao**. (al. 2)

c) Itunge sentensi sahihi ukitumia kihusishi kimoja cha mtendaji. (al. 1)

d) Lugha ukamilishwa kwa ushirika wa vijenzi vyake vidogo vidogo. Vitaje. (al. 2)

e) Tumia neno maudhui katika sentensi ili kudhihirisha upatanisho wa kisarufi. (al. 2)

f) Tunga sentensi kudhihirisha wakati ujao hali timilifu. (al. 2)

g) Akifisha kifungu kifwatacho: nimekuwa nikisisitiza umoja wa afrika daniel moi 1924 2020 (al. 4)

h) Geuza katika usemi halisi: Askari jela alimuuliza kendi kama alidhani hapo ni kwao. Alimwamuru aende kwake mara moja. (al. 2)

i) Bainisha maana mbili ya sentensi hii: Umu alimwandikisha mkewe. (al. 2)

j) Changanua kwa matawi: Watu ambao wana mali hawatoi zaka zao. (al. 4)

k) Eleza matumizi ya neno wale katika sentensi hii: Wale walioiba ni mabanati wale ambao waliambiwa wale kabla ya kitendo hicho. (al. 3)

l) Bainisha aina ya yambwa na chagizo katika sentensi: Binti yake Kimani aliozwa Luka kwa harusi mwezi uliopita. (al. 2)

m) Ainisha virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo: Yule mtiifu atatuzwa kesho jioni na mwalimu mkuu (al. 2)

n) Amrisha kwa kutumia kitenzi **nywa** katika nafsi ya pili (al. 1)

o) Tunga sentensi moja kuonyesha maana mbili za neno chupa (al. 2)

p) Tumia neno sembuse katika hali kanushi kutunga sentensi (al. 2)

q) Neno sema ni kitenzi, libadili liwe kielezi kwa kutungia sentensi. (al. 2)

r) Andika katika ukubwa wingi: Kitoto hiki kinalia kwa sababu hakijala mkate. (al. 2)

s) Tunasema ng'ang'ana kukutu, vunjika ………………..pelekwa ……………. (al. 1)

**ISIMU JAMII (alama 10)**

a) Eleza sifa zozote **tano** zinazotambulisha sajili ya mazungumzo. (alama 5)

b) Andika sifa tano za kimtindo utakazotumia ukipata fursa ya kutangaza mchezo wa kandanda shuleni. (alama 5)

www.freekcsepastpapers.com

**<u>TATHMINI YA PAMOJA YA MOKASA</u>**
**<u>102/3</u>**
**<u>KISWAHILI</u>**
**<u>KARATASI YA 3</u>**
**<u>FASIHI</u>**
**<u>MUDA: SAA 2½</u>**

**Maagizo**

*a)* *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
*b)* *Swali la kwanza ni la* ***lazima.***
***c)*** *Chagua mengine matatu kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:* ***Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Ushairi.***
d) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka katika sehemu moja.*

**SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI**

**1. Lazima**

**Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**

Zimepita siku ayami
Siku chungu tangu giza lipotanda
Wakati lipotazama kwa kiwewe na shauku
Pumzisho kipania, roho kupigania
Ziraili alipokakamaa aushiyo kufakamia.

Nilikwita kwa sauti
Ela mpenzi hukunitika
Machoyo litunga mbele
Kumkabili huyu nduli
Nikabaki kunyongonya
Jaala kitumainia,
Mtima kijiinamia
Hatima kungojea.

Ya mwisho lipopumua,
Alfajiri ya kiza kuu
Nalidhani wanichezea,
Mizaha yako kawaida
Lijaribu kupulizia
Hewa toka langu pafu,
Tumaini kiniambia pumzi zangu takuhuisha
Sikujua hizo likuwa juhudi za mfa maji muhebi.

Macho libaki kutunduiya, tabasamuyo kitaraji
Kumbe mwenzangu kaniacha!
Ukiwa ulinivaa, ukungu ukatwandama
Pa kuegemea sikujua fundo chungu linisakama
Tabibu alipoingia na kutangaza rasmi mauko.

Ilikuwa kana kwamba ndo jana lipofunga nikahi,
Kumbukizi zilinijia kwa chozi teletele
Japo kifo ni faradhi ndwele hino halieleweki
Ama jicho la hasidi,
Limekuangaza jamani?
Koja hili ninalokuwekea,
Kando ya kasri hili la shakawa
Ni hakikisho toka kwangu, nitatamba sana njia
Kutafuta alotwendea kinyume kutupoka,
Mauko kutuleteya.

www.freekcsepastpapers.com

a) (i) Ainisha utungo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. (alama 1)
(ii) Andika sababu **tatu** kuthibitisha jibu lako la a (i). (alama 3)
b) Bainisha sifa **mbili** za jamii inayosawiriwa wa utungo huu. (alama 2)
c) Fafanua vipengele **vinne** vya kimtindo ambavyo vimetumiwa kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. (alama 4)
d) Tungo za aina hii zinaendelea kufifia katika jamii yako. Fafanua hoja **tano** utakazotumia kuishawishi jamii yako kukinga dhidi ya hali hii. (alama 5)
e) Unanuia kutumia mbinu ya kushiriki kufanya utafiti kuhusu tungo za aina hii. Eleza sababu **tano** za kuchagua mbinu hii. (alama 5)

**SEHEMU YA B: RIWAYA**
**Assumpta Matei: Chozi la Heri**
**Jibu swali la 2 au la 3**

2. … alijua kwamba msimamo wake huu ungempalia makaa. Lakini alihiari kupoteza riziki yake ili kuyaokoa maisha ya wanyonge wasio na hatia.
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Fafanua sifa za anayerejelewa katika dondoo. (alama 4)
(c) Huku ukirejelea wahusika riwayani, thibitisha kuwa hiari ya wahusika inawafanya kujipalia makaa. (alama 12)

3. … kisha ninaanza kumsimulia yaliyojiri kana kwamba ni mgeni wa hali hii. Ninajua kwamba simsimulii … bali pia Mamia ya Wahafidhina ambao huenda hawajaishuhudia hali hii.
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Eleza umuhimu wa usimulizi wa msemaji katika kujenga riwaya ya ***Chozi la Heri.*** (alama16)

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA**
**Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Maradhi! Madhila yake hayasemeki. Yakimla mtu humthakilisha. Humwacha hoi hana mbele wala nyuma.Yakitaka huzichezea dawa mwajificho. Dawa zikiingilia huku, maradhi hutokezea pale hali pesa zinakwenda, shughuli zinasimama ... Dunia ina mitihani tosha lakini panapo maradhi sugu, uzito wake haumithiliki."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Bainisha mbinu **nne** za kimtindo zilizotumiwa kwenye dondoo. (alama 4)
(c) Huku ukirejelea hadithi, eleza sifa **sita** za msemaji wa kauli hii. (alama 12)

5. **Sara:** Nilipopata harufu ya mahamri nilijua bila shaka kwamba baba yako ameingia jikoni.
**Neema:** Mama sijaona baba akipika hivi karibuni.
Kwa kurejelea nukuu zilizotolewa hapa juu, fafanua usasa na utamaduni vilivyosawiriwa tamthiliani. Kila upande utawe na hoja kumi kumi. (alama 20)

**SEHEMU YA E: HADITHI FUPI**
**Rachel Wangari: Fadhila za Punda**
6. "Nisikuone tena ofisini mwangu, mwanamke wewe. Kuja kuniaibisha, wapinzani wangu waseme nimeshindwa kumdhibiti mke wangu, sembuse kaunti nzima!"
a) Bainisha muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza toni katika muktadha huu. (alama 2)
c) Asasi ya ndoa imo hatarini. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea mandhari ya dondoo hili. (alama 4)
d) Jadili namna mbinu zifuatazo zilivyotumiwa na mwandishi wa hadithi **Msiba wa Kujitakia**. (alama 10)
(i) Kinaya
(ii) Mbinu rejeshi

**Clara Momanyi: Mapambazuko ya Machweo**
7. "…umeniita tukae hapa kando ya barabara kwa nini lakini?
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Eleza sifa zozote **nne** za Mzee Makucha. (alama 4)

www.freekcsepastpapers.com

c) Fafanua changamoto zinazowakumba msemaji na msemewa pamoja na wenzao katika hadithi hii ya **Mapambazuko ya Machweo**". (alama 6)

d) Jadili visababishi vyovyote **sita** vya matatizo yanayowakumba wahusika katika hadithi ya **Harubu ya Maisha**. (alama 6)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

8. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Soma waliosoma, masomo wa zama soma,
Soma hata wangasoma, wasome na kusosoma,
Soma mwisho watasoma, kusoma kuyosoma,
Soma somato msoma, wasoma wambe kusoma.
Soma ya leo msoma, soma siwache wasoma,
Soma akiliyo choma, kisomo cha waliosoma,
Soma hata wangasoma, mizomo haitachoma
Soma somato msoma, wasoma wambe kasoma.

Soma ja samaki shoma, kusoma kuno kushoma,
Soma wa jana mshoma, bado kitu hajashoma,
Soma kuno ndo kusoma, kushoma bila kuchoma,
Soma somato msoma, wasoma wambe kasoma.

Soma waseme wasoma, ya kwamba hawajasoma,
Soma wakusome soma, mbwa wapi yuno msoma?
Soma wakisoma soma, washindwe yako kusoma,
Soma somato msoma, wasoma wambe kasoma.

Soma ya kusomea soma, yasosomwa pia soma,
Soma masomo kuchoma, masomo yaseme 'soma'!
Soma siwe ja mzoma, kuzoma siyo kusoma,
Soma somato msoma, wasoma wambe kasoma.

Soma walimwengu soma, visomo vyao kusoma,
Soma kusomoa soma, kushomashoma kusoma,
Soma kusoma msoma, kisichosomwa kusoma,
Soma somato msoma, wasoma wambe kasoma.

Soma hata ungasoma, jua bado hujasoma,
Soma kuna walosoma, kwao utakuwa joma,
Soma msomaji soma, hakuna tama kusoma,
Soma somato msoma, wasoma wambe kasoma.
**(Hamisi Babusa)**

www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Eleza mbinu alizotumia mshairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 2)
b) Fafanua bahari katika shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: (alama 3)
i) Idadi ya vipande
ii) Mpangilio wa maneno
iii) Mpangilio wa vina
c) Chambua ubeti ya nne kiarudhi. (alama 3)
d) Bainisha vipengele vya kimtindo katika shairi hili. (alama 2)
e) Fafanua aina zozote tatu za urudiaji katika shairi hili. (alama 3)
f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 4)
g) Eleza toni katika shairi hili. (alama 1)
h) Fafanua maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi hili. (alama 2)
i) Zoma
ii) Tama

Cheo na madaraka haya ya umeneja yamaanisha kila siku nivae suti kamili na shati nyeupe pe, ambayo shingoni imeambatanishwa na kipande maalumu cha kitambaa kinacholewalewa kifuani. Nijiangaliapo kiooni hujifananisha na mtu ambaye amejitia kitanzi shingoni.

Nina kitambi ambacho labda ni **taashira** ya utajiri. Hata hivyo ingawa mimi si tajiri mwenye sauti kubwa kiuchumi, ninaweza kujivunia elimu yangu iliyoniwezesha kujimudu kidogo maishani. Sasa nina shamba-langu mwenyewe, nyumba yangu mwenyewe ambayo imejaa mali yangu mwenyewe. Nina redio yangu mwenyewe, rununu -yangu mwenyewe na wanyama wangu mwenyewe.

Lakini mwenzungu ambaye zilimwishia ukingoni katika shule za nasari, hana elimu, pesa wala anaahu kuzikiwa wakati mpira utakapomwia mwingi.

**Maswali**

a) Eleza imani ya mwandishi kuhusu elimu. (alama 3)
b) Taja dhiki zilizomkabili mwandishi alipokuwa shuleni. (alama 2)
c) Onyesha uhusiano uliopo kati ya elimu, kazi na ukwasi kwa mujibu wa habari hii. (alama 2)
d) Ukirejelea makala haya, fafanua msemo, "elimu ni bahari haina kikomo" (alama 3)
e) Hatima ya wale ambao hawakupata elimu ni ipi? (alama 2)
f) Badala ya maneno yafuatayo mwandishi angetumia msamiati gani? (alama 3)
i. Niliwahusudu ______________________________
ii. Ndaki ______________________________
iii. Taashira ______________________________

**SEHEMU B:**
**UFUPISHO** (ALAMA 15)

Sisi vijana wa Kenya inatupasa tuwajibike kufanya kazi kwa bidii, na kwa dhati ya mioyo yetu tuweze kupata ufanisi, na uwezekano wa kuinua nchi yetu changa katika kiwango cha juu. Tukumbuke, "Ajizi ni nyumba ya njaa." Kwa hivyo basi haifai kulaza damu ikiwa matatizo nchini mwetu yametuzonga. Lazima tufanye kazi kwa busara, adabu njema na jitihada kwa moyo mmoja. Sharti tutilie maanani zaidi elimu ya vijana na watu wazima, kilimo, uchumi na amani katika nchi yetu. Tunahitaji taifa lenye watu walioelimika, kwani bila elimu itakuwa vigumu sana kuweza kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo. Tupende tusipende lazima tuzidishe mazao mashambani, kwani kila kukicha idadi ya watu inaongezeka. Ni sharti tuweze kujitosheleza katika vyakula. Zaidi ya hayo pia lazima tujishughulishe na biashara ambapo kwa sasa ni Wakenya wachache sana ambao wanatambua umuhimu wa biashara. Wengi ni wale wenye mawazo ya kwamba, lazima kila mmoja aajiriwe maishani. Yatupasa tujitahidi kuleta uchumi katika; mikono ya wananchi wa Kenya badala ya kuwaachia wengine ambao hawahusiki.

Mafunzo tunayopata majumbani, shuleni na hata katika jamii, lazima yatuwezeshe kutambua mbinu za kupitia. Tunahitaji elimu tambuzi ambayo itamfanya Mwanakenya kujua wajibu wake katika jamii. Tumesinywa na elimu pumbao; inayotupumbaza na kutufanya tusione mbele. Sisi vijana tukiwa viongozi wa siku sijazo, "Utengano ni uvundo" Lugha ya taifa ndicho chombo cha pekee ambacho kinatuunganisha na kuweza kutuwasilishia mapendekezo, mawaidha na hisia zetu. Kukosa ndiko kibinadamu, wakati tunapokosea, lazima tukubali tumekosea na kufanya masahihisho mara moja kwani, "Usipoziba ufa, utajenga ukuta." Tusikasirike kwa sababu tumesahihishwa makosa yetu na wenzetu. Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi yetu tukiwa wazalendo halisi.

Sisi tukiwa vijana sharti tujishughulishe na kuyaangalia matatizo ya nchi, pia kutafuta njia za kutatua matatizo hayo. Siku zote tutekelezee nidhamu. Ni jambo la kusikitisha kwamba sisi vijana twashutumiwa mara kwa mara kwa kutokuwa na nidhamu shuleni na majumbani mwetu. Utamaduni wa asili unakariri sana kuwa tuwe na nidhamu shuleni na majumbani mwetu. Hi watu waweze kuishi maisha bora na kuwa na maendeleo, amani na upendo, lazima tuwe na bidii, ushirikiano mwema na kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo. Tukiwa viongozi ambao hawajishughulishi na maendeleo, basi tutabaki nyuma kama mkia siku zote. Bahati mbaya ni kwamba wananchi wengi siku hizi huchagua viongozi wao kwa kufuata ukoo ama kama kwa utajiri wake. Kwa hivyo basi ni vyema kuwachagua viongozi kutokana na ufanisi wanaoweza kuleta bali si kwa kutegemea utajiri au ukoo.

<u>**Maswali**</u>

a) Katika aya ya kwanza mwandishi anawahimiza vijana kufanya nini ili kuleta maendeleo? (maneno 50) (alama 6)

**Nakala chafu**

**Nakala safi**

b) Kwa mujibu wa taarifa ni mambo gani yaliyochangia kuzorota kwa maendeleo nchini Kenya? (Maneno sitini) (alama 6)

**Nakala chafu**

**Nakala safi**

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU C:**

**MATUMIZI YA LUGHA** (ALAMA 40)

a) Andika nomino moja ambayo inapatikana katika ngeli ya U-I (alama 1)

b) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo:
Bi. Kija anajiona. (alama 2)

c) Tunga sentensi ya neno moja yenye kiima, wakati, kitendewa / kitendwa na kitenzi. (alama 2)

d) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (alama 2)
Mwanamke huyo aliipiga ngoma hiyo mpya hadi ikapasuka.

e) Kamilisha jedwali lifuatalo ili kuonyesha jinsi irani zinavyotamkwa. (alama 2)

| Irabu | Hali ya ulimi | Hali ya midomo |
|---|---|---|
| e | | |
| u | | |

f) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya vishale. (alama 3)
Juma analima shambani lakini Asha anasoma.

g) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendeana. (alama 2)
i. La ______
ii. Pa ______

h) Pigia kistari kirai nomino katika sentensi ifuatayo: (alama 2)
Kuimba kwake kunapendeza ajabu.

i) Taja matumizi manne ya mshazari au mkwaju. (alama 2)

j) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia kiunganishi cha neno moja chenye maana sawa na kilichopigiwa mstari. (alama 2)
Sitafika shuleni kesho <u>kwa sababu</u> nina shughuli za dhamira.

k) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kutumia “O” rejeshi tamati. (alama 2)
Kipofu ambaye alishinda mbio alituzwa nishani ya dhahabu.

l) Onyesha aina za yambwa katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Yaya alimpa mtoto maziwa kwa chupa.

m) Huku ukitoa mifano ya sentensi, eleza matumizi mawili ya kiambiushi “po” (alama 4)

n) Kwa kuzingatia kiimbo eleza sentensi zifuatazo ni za aina gani. (alama 3)
i. Mama yuko jikoni
ii. Njoo hapa!
iii. Ameanguka vibaya sana, tafadhali njoo tumsaidie.

o) Tunga sentensi tatu ukitumia neno jasiri kama: (alama 3)
i. Kivumishi
ii. Kitenzi
iii. Nomino

p) Onyesha kishazi huru na tegemezi katika sentensi hii. (alama 2)
Aingiapo darasani mwambie asome kwa bidii.

q) Unda sentensi moja kutokana na sentensi sahihi zifuatazo. (alama 2)
i. Kijakazi alikuwa mgonjwa.
ii. Kijakazi alifanya kazi yote ya nyumba

r) Tumia nahau badala ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi.
Baba husema kwa <u>mafumbo</u> kila <u>anapolewa</u>. (alama 1)

**SEHEMU D:**

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

**Soma kifungu kifuatacho halafu ujibu maswali.**

“Baada ya mjadala mrefu kuhusu mswada huu na kuzingatia sheria za bunge hili tukufu, kifungu cha 4, kipengele cha 6, ibara ya 3 ndugu zangu ningetaka kutangaza kupitishwa kwa mswada huu na sasa utawasilishwa kwa rais kusubiri sahihi yake. Kupitishwa kwa mswada huu kwa kauli moja ni tukio la kihistoria kwa bunge hili. Tutaweza kufikia kwa two third rule….”

a) Tambua sajili hii. (alama 1)

b) Andika sifa zozote tano za sajili hii. (alama 4)

c) Fafanua vipengele vingine vitano vya mitindo ya mawasiliano ambayo mbunge angetumia katika kufanikisha mawasiliano yake. (alama 5)

www.freekcsepastpapers.com

**IMENTI SOUTH**
**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI LA TATU**
**FASIHI**
**MUDA: SAA 2 ½**
***MAAGIZO***

*a) Jibu maswali **manne** pekee*
*b) Swali la **kwanza** ni la lazima*
*c) Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki. Yaani: Tamthilia, Riwaya, hadithi fupi na ushairi.*
*d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu kimoja.*
*e) Kila swali lina alama ishirini.*

**SEHEMU YA A: SWALI LA LAZIMA**
**FASIHI SIMULIZI**

**1. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

A: Kumbe mambo yenyewe rahisi hivi?
B: Rahisi, lakini usije ukabakwa tena.
A: Hapana, safari hii itakuwa zamu yako. (Alimrudishia…. Huku akichekacheka)
C: Hapajaharibika mambo mama'ngu. Kwani la ajabu lipi? Sasa mie namsubiri Bakari mpya tu, hichi kikongwe nikipe takaka (Akitabasamu)
D: Haachwi mtu hapa. Tutabanana humo humo. Yeye atakuwa mke mdogo na mimi mkubwa.

i) Bainisha kipera cha utungo huu na uthibitishe kwa mfano. (alama 2)
ii) Kwa kutolea mifano eleza sifa nne za kipera hiki. (alama 8)
iii) Fafanua majukumu matano ya kipera hiki kwa jamii. (alama10)

**SEHEMU YA B:**
**TAMTHLIA (BEMBEA YA MAISHA)**

**2.** "Eti alama! My foot! (kimya) Eti ameshuka nafasi darasani lakini akapandisha alama.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza sifa za mnenaji. (alama 6)
c) Taja na utolee mfano mbinu mbili ambazo zinajitokeza katika dondoo hili. (alama 4)
d) Fafanua umuhimu wa mnenaji katika kujenga tamthlia ya Bembea. (alama 6)

**3.** a) Jadili maudhui ya utamaduni katika tamthilia ya Bembea. (alama10)
b) Eleza kwa kutolea mifano jinsi ya mbinu rejeshi ilivyotumiwa katika tamthilia ya Bembea ya maisha. (alama10)

**SEHEMU YA C:**
**RIWAYA YA CHOZI LA HERI**

**4. Jibu swali moja katika sehemu hii.**

Lakini…
Wewe hushangai?
Kwani wanawashwa
na pilipili iliyo
Kwenye uchago wa mwengine?
Kwani wasitake kukuli
Kilichotufanya mimi na wewe
Kwa marafiki wa kufa kuzikana
Kwani wasimulize
Alonirithisha huno mkaja?
Kwa utu kunipoka
Akanibakisha kaka
La!
Kiunzi cha mfupa?

www.freekcsepastpapers.com

Wali wakifanyani?
Alipokuja Bwana mabavu
Shamba la asili akatwaa
Ati ni yake milki
Alonunua
Si kurithishwa
Na mkoloni?
Wali wakifanyani
Alipotuonyesha hati miliki bandia
Nasi mithili ya vifaranga
Waliomuona mwewe,
Tukajikunyata kwa uoga
Tusitoe hata kauli moja
Kupinga ubahaimu huu?
Dhiki ya ukosefu ikatutuma
Kuwa vivarua
Katika "lake" shamba?

**<u>Maswali</u>**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Tambua mbinu sita za kimtindo zilizotumiwa katika utungo huu. (alama 6)
c) Kwa kurejelea utungo mzima fafanua umuhimu wa mnenaji katika kujenga riwaya ya chozi la Heri. (alama10)

**5.** a) Baba amewahi kumwona mtoto wa miaka hamsini ambaye hajasota….kwa kurejelea riwaya nzima dhibitisha kuwa mtoto anayerejelewa hajasota. (alama10)
b) Haki za watoto hazitiliwi maanani katika jamii za Kiafrika. Eleza ukweli wa kauli hii kwa kurejelea Riwaya ya chozi la Heri. (alama10)

**SEHEMU YA D:**
**DIWANI YA MAPAMBAZUKO YA MACHWEO**

**6.** Fafanua dhiki zinazowakumba raia katika hadithi ya "Msiba wa kujitakia". (alama20)

**7.** "Maajabu ya firauni ndiyo haya! Kumbe kazi ndio hii."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza sifa tatu mnenaji wa maneno haya. (alama 6)
c) Fafanua changamoto zinazowakumba vijana katika hadithi ya "mapambazuko ya machweo". (alama10)

**SEHEMU YA E: USHAIRI**

**8.** **SHAIRI A**

Wanangu pulikani, wangu mpate wosia
Kiwa humu duniani, muuepuke udhia
Msije nyie jutani, mawaidha kipilia
Zingateni uvumilivu, mpate kulani mbivu.

Papara ya mapenzini, hamtepuka zinaa
Mpate na wahibuni, sije wapata balaa
Yasije kuwadhuruni, msije nyie kulia
Zingateni uvumilivu, mpate kulani mbivu.

Mkiwa mna sihani, kazi fanya nawambia
Msije kuzua zani, magonjwa kusingizia
Mlahaka na kazini, mweze kuuzingatia
Zingateni uvumilivu, mpate kulani mbivu.

Vya bwerere sipendeni, sije nyie wasumbua
Mjifunge kibwebweni, kunguni msije kua
Kiwani nanyi kazini, daima muwe taa
Zingateni uvumilivu, mpate kulani mbivu.

www.freekcsepastpapers.com

Nataka mufahamuni, wengi moyo wataua
Wanangu la muhimuni, manenoyo puzilia
Pigeni na hatuani, kama wasoyasikia
Zingateni uvumilivu, mpate kulani mbivu.

Kama maji mtungini, nawaomba kutulia
Taepuka maovuni, kiwa mtavumilia
Ikiwa kuna mamboni, vigumu yatawawia
Zingateni uvumilivu, mpate kulani mbivu.

**Maswali**

a) Eleza nafsineni katika shairi hili. (alama 2)
b) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
c) Ainisha shairi hili katika bahari tofauti kwa kuzingatia: (alama 2)
a) Vipande
b) Vina
d) Kwa kutoa mfano, taja tamathali moja ya usemi inayojitokeza katika shairi hili. (alama 1)
e) Taja na uonyeshe idhini ya mshairi kama inavyojitokeza katika shairi hili. (alama 2)
f) Eleza umuhimu wa kibwagizo cha shairi hili. (alama 2)
g) Kwa kutumia hoja mbili, eleza ushauri anaotoa nafsineni kwa nafsinenewa. (alama 2)
h) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
i) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hili. (alama 3)
a) Pulikani
b) Zani
c) Kunguni msije kuwa

**SHAIRI B**

**9. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Vijana wetu hawa tumaini wamepungua
Wamebaki kujinwea vidawa
Na vinywa vyao havikosi
Mioshi kufuka.

Wamebaki kujinamia suruale zikidondoka
Kama kuku wa kidimu
Utadhani ndio waliowazaa wazee wao
Wamebaki kuiba na nyingi kuwacheka
Wamebaki kuomba na nyingi kuwacheka
Wamebaki walipokuwa jana na nyingi mbele mwaenda.
Mtakapofika ukingoni na pembeni kuitwa
Nahodha watakuwa hawakusalia
Taifa litagonga ule mwamba mkubwa
Akose kijana aliyejasirika kulikwamua!

**Maswali**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 2)
b) Shairi hili lina ujumbe gani kwa hadhira. (alama 2)
c) Fafanua kwa kutolea mifano mbinu ,mbili zilizojitokeza kwenye utungo. (alama 4)
d) Tolea mifano matumizi mawili ya mishata. (alama 2)
e) Tambua nafsi neni na nafsi nenewa katika shairi. (alama 2)
f) Fafanua toni ya malenga. (alama 2)
g) Tasnifu ya malenga ni ipi. (alama 2)
h) Eleza uhuru wa mshairi katika utungo. (alama 2)
i) Toa maana ya vifungu kama vilivyokusalia (alama 2)
   i) Nahodha watakuwa hawakusalia
   ii) Taifa litagonga mwamba mkubwa.

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA MWAKICAN**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**INSHA**
**MUDA: SAA 1¾**

**MAAGIZO**

1. *Andika insha mbili*
2. *Insha ya kwanza ni ya **Lazima***
3. *Chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia*
4. *Kila insha ina alama 20*
5. *Kila insha isipungue maneno 400*
6. *Kila insha iandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

1. Umetangazwa kuwa mwanafunzi bora katika mtihani wa kitaifa.Mwalimu mkuu wa Shule ya Upili ya Tangamano amekualika katika shule yake kuwahutubia wanafunzi kuhusu kilichochangia ufanisi wako. Andika hotuba utakayowatolea walimu, wazazi na wanafunzi wa shule hiyo.
2. Kumekuwa na ongezeko la visa vya ukeketaji wa wasichana. Pendekeza njia za kukabiliana na tatizo hili.
3. Andika insha itakayoafiki methali: maji yakimwagika hayazoleki.
4. Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo:
   Tulikuwa tukipata chajio, mara mama akapigiwa simu na alipoipokea………

---

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA MWAKICAN**
**102/2**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya pili**
**Lugha**
**MUDA: SAA 2½**

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**
   *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishanji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu;tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi,kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya kipindi cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mahali mwa kazi, washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano,

kwa wanajamii wanaoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri, uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoaukuta wauhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wamajirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na 'uhusiano wa chembe chembe.' Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachoshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea, nguo anazokufulia, ususi anokufanyia na kadhalika. Mahussiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiliwa, ameibiwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusiana vipi na jamaa zetu, marafiki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

(a) Taja kigezo cha kuzungumzia mahusiano. (alama 1)
(b) Eleza imani ya watu kuhusu mahusiano ya watu. (alama 1)
(c) Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. (alama 2)
(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. (alama 4)
(e) Taja sifa kuu za mahusiano ya muda mfupi. (alama2)
(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (alama2)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)
(h) (i) inasigana
(ii) yameghoshi
(iii) vighairi

www.freekcsepastpapers.com

2. **MUHTASARI /UFUPISHO (ALAMA 15)**

Kuna dhana nchini ambayo inazidi kuenezwa miongoni mwa vijana na usipochunga,tutakuja kujipata pabaya katika siku za usoni. Kwa kipindi cha miongo miwili hivi iliyopita, sekta ya sanaa nchini imekuwa ikiimarika kwa kasi. Kuna wasanii ambao wamefanikiwa kujiendeleza kimaisha kutokana na talanta zao lakini pia kuna wale ambao wamebaki katika hali ya uchochole, pengine kutokana na kuwa hawafahamu vyema jinsi ya kujisimamia na kutumia talanta zao kama mbinu ya kujipatia riziki. Kwa muda huo wote, vijana wengi Wamejikuta wakivutiwa mno na hali ya kimaisha ya wasanii waliobobea, hasa wanamuziki, na hivyo basi hujitosa kwenye sekta ya sanaa wakiwa na matumaini makubwa ya kuishi maisha ya kifahari.

Imefikia kiwango ambapo washikadau wa masuala ya kuendeleza maisha ya vijana, ikiwemo Wizara ya Michezo, Vijana na Utamaduni wanawekeza pakubwa kuendeleza sekta ya sanaa. Ni hapa ndipo wasiwasi unaibuka kwa kuwa huenda tukachukulia Kwamba juhudi za kuwezesha vijana kujikimu kimaisha zitafanikiwa tu iwapo sekta ya sanaa itaimarishwa. Dhana hii ni potovu na ni sharti washikadau wazinduke, waanze kupanua mawazo yao na kuwa na busara kwenye hatua wanazochukua ikiwa wana nia ya kuwezesha vijana kujikimu kimaisha na kuchangia ukuaji wa uchumi wa taifa.

Ukichunguza kwa makini, utapata kuwa ni asilimia ndogo mno ya wanaojitosa kwenye sanaa ambao wanaweza kusemekana wana ari na kipawa cha kutosha kuweza, kuchangia ipasavyo kwenye uchumi wa kitaifa kwa kutumia vipawa hivyo. Hivyo basi, suala ibuka ni je, asilimia kubwa iliyosalia huwa wanafanya nini, na ni jinsi gani wanavyoweza kuwezeshwa wajiendeleza zaidi kimaisha? Hapatakuwa na

**4. ISIMU JAMII**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

A: Sasa!
B: Fit!
A: Umepata ngapi?
B: Four twenty.
A: Utaitwa National School?
B: Sijui na wewe?
A: Nitaangalia yangu tomorrow.
B: Uta-come kunieleza?
A: Yes au nikuesemesie.
B: Okey nitakuremind.
A: Bye.
B: Sawa nisalimie buda.

a). Hii ni sajili gani? (alama 2)
Sajili ya lugha ya mtaani.

b). Unadhani wazungumzaji ni wa rika gani? Kwa nini? (alama 2)

c). Taja sifa bainifu za sajili hii (alama 6)

---

**MTIHANI WA PAMOJA WA MWAKICAN**
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya tatu**
**FASIHI**

***MAAGIZO***

1. *Jibu maswali manne*
2. *Swali la kwanza ni la LAZIMA*
3. *Maswali hayo mengine matatu, yachaguliwe kutoka maswali yaliyosalia*
4. *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
5. *Majibu yote LAZIMA yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**SEHEMU YA A:**
**SWALI LA LAZIMA:**
**USHAIRI**
**SABUNI YA ROHO**

Ewe tunu ya mtima, kwa nini wanikimbia?
Ndiwe suluhu za zama, waja wakukimbilia,
Waja wanakutazama, madeni wakalipia,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mafuta ya roho, walisema wa zamani,
Utanunua majoho, majumba na nyumbani,
Umezitakasa roho, umekuwa mhisani,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Matajiri wanakujua, wema wako wameonja,
Nguo zao umefua, wakupata kwa ujanja,
Sura zao - mefufua, wanazuru kila nyanja,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

www.freekcsepastpapers.com

Ndiwe mvunja mlima, onana na maskini,
Watazame mayatima, kwao kumekuwa duni,
Wabebe waliokuwa, wainue walio chini,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mvunja mlima, wapi kapata uwezo,
Umezua uhasama, waja kupata mizozo,
Ndiwe chanzo cha zahama, umewatia vikwazo,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Umevunja usuhuba, familia zazozana,
Waliokuwa mahabuba, kila mara wagombana,
Roho zao umekaba, majumbani wachinjana,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Nakutafuta kwa hamu, sabuni unirehemu,
Sinilipue ja bomu, sije kawa marehemu,
Niondoe jahanamu, ya ufukara wa simu,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Naondoka wangu moyo, nikuitapo itika,
Fulusi wacha uchoyo, tatua yalonifika,
Nichekeshe kibogoyo, nami nipate kuwika,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

**Maswali**

a) Taja nafsinenewa. Thibitisha. (alama 2)
b) Eleza toni ya nafsineni. (alama 1)
c) Eleza arudhi zozote nne zilizozingatiwa katika utunzi wa shairi hili. (alama 4)
d) Mshairi anawasilisha ujumbe gani katika mleo wa ubeti wa sita? (alama 1)
e) Ukitoa mfano eleza mbinu zozote tatu za lugha alizotumia mshairi. (alama 3)
f) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (alama 4)
g) Jadili jinsi mshairi ametumia idhini ya mshairi. (alama 2)
h) Kwa kurejelea mpangilio wa vina eleza bahari ambamo shairi hili linaweza kuainishwa. (alama 1)
i) Fafanua maana ya : (alama 2)
*i)* ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima
*ii)* jehanamu

**SEHEMU YA B:**
**TAMTHILIA:**
**BEMBEA YA MAISHA**

**2.** "Maisha ya sasa hayana fundi. Yanamwendesha kila mtu kama tawi lililosukumwa hadi likangóka kutoka tagaani na kupeperushwa na upepo"
a. Eleza muktadha wa dondoo hili (al4)
b. Tambua vipengele vya kimtindo katika dondoo hili (al2)
c. Eleza sifa nne za msemewa (al4)
d. Thibitisha kauli ya msemaji ukirejelea tamthilia nzima (al10)

**Au**

**3.** Timothy Arege amewajenga wanaume kwa njia hasi na chanya. Jadili kauli hii kwa kutolea mifano kutoka kwenye tamthilia (al20)

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA C:**
**HADITHI FUPI:**
**MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE**
***Msiba wa Kujitakia D.W.Lutomia***

**4.** ***a)*** *"Ndoto anayozidi kuiota akiwa mle kaburini! Ndoto iliyozikwa katika kaburi la sahau"*
*i)* *Eleza muktadha wa dondoo hili (al 4)*
*ii)* *Fafanua mbinu tatu zinazojitokeza katika dondoo (al 3)*
*iii)* *Eleza umuhimu wa anayerejelewa (al 3)*
b) Fafanua dhiki zinazowakumba raia katika hadithi ya Msiba wa Kujitakia (al 10)

**Au**

***Harubu ya Maisha Paul Nganga Mutua***

**5.** "Naja. Nakamilisha shughuli ndogo hapa kisha nianze safari…''
a. Weka dondoo hili katika muktadha wake (al 4)
b. Eleza sifa za msemaji wa kauli hii (al 4)
c. Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi hii (al 12)

**SEHEMU YA D: CHOZI LA HERI**

**6.** "Vijana hawapaswi kungojea kufanyiwa kila kitu. Tumewapa nyavu za kuvulia, nao wanaona wangoje kuletewa samaki!"
a. Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b. Fafanua maudhui yanayodhihirika katika dondoo hili (alama 2)
c. Tambua na ueleze mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili (alama 4)
d. Eleza maafa yaliyomwandama msemaji wa kauli hizi (alama 4)
e. Taja na ueleze sifa sita za msemewa (alama 6)

**Au**

**7.** Tathmini umuhimu wa usimulizi wa Pete katika kuijenga Riwaya Chozi la Heri. (alama 20)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

**8.** **Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

Hapo zamani za kale paliishi mtoto katika kisima kimoja. Siku moja mtoto huyu aliokota kijiwe karibu na soko kuu. Kijiwe kilikuwa kikimeremeta kwa rangi mbalimbali na kilizingirwa na pete ya dhahabu.

Mtoto huyu na wenzake walianza kurushiana kijiwe hicho. Baada ya muda kilianza kuongezeka umbo na kuonekana kama kiwiliwili cha binadamu. Kikaanza kuwakimbiza wale watoto. Kutokana na ukelele wao, watu walikuja kutazama nini kilikuwa cha mno. Walipofika walikutana ana kwa ana na dubwana hilo. Lilizidi kuongezeka umbo na likawameza wote pamoja na mifugo wao. Wachache waliojaribu kukimbia liliwashika kwa mikono yake mipana na mirefu. Kwa bahati njema alikuwepo mama mmoja aliyeona hayo yote. Alikuwa mbali kiasi na hapo. Aliteremka kutoka kilele cha mlima na kuwapata wakulima makondeni na sawia akawajuza kuhusu kitendo kilichomwogofya sana. Wote wakaacha shughuli zao na wakatwaa silaha zao wakaelekea soko kuu.

Dude sasa lilikuwa limejilaza baada ya shibe, wakulima wale walichagua watu sita ambao walijulikana kwa ushujaa wao. Pamoja walilinyemelea lile nyangarika na kulikata mara moja. Lilitoa mkoromo mkuu kabla halijakata kamba. Punde, wanakijiji kwa uangalifu mkubwa walitoboa tumbo lake wakitarajia kupata maiti za wapenzi wao pamoja na mifugo wao. Wote walijawa na furaha kuu walipoona wapenzi wao wakijichomoza kutoka tumboni, mmoja baada ya mwingine hadi akatoka yule wa mwisho. Mbuzi, kondoo na ng'ombe wote walitoka mmoja mmoja.

Siku hiyo kuliandaliwa sherehe ya kumshukuru Muumba kwa wema wake. Watoto walishauriwa wasithubutu kuchezea vitu wasivyovijua.

**Maswali**
a. Ainisha kipera hiki cha hadithi (alama1)
b. Fafanua mambo manne yanayodhihirisha kuwa kipera hiki ni sanaa. (alama 4)
c. Mwasilishaji bora wa kipera hiki anafaa kuwa na sifa gani? Eleza zozote nne. (alama 4)
d. Onyesha mifano miwili ya fantasia katika hadithi hii. (alama 2)
e. Eleza sifa nne za tungo hizi. (alama 4)
f. Eleza majukumu matano ya mtindo uliotumiwa kuanzisha hadithi hii. (alama 5)

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA GATUZI LA MUMIAS MAGHARIBI**
102/1
KISWAHILI
KARATASI YA KWANZA
INSHA
MUDA: SAA 1 ¾

***MAAGIZO:***
*i) Andika insha mbili; insha ya kwanza ni ya lazima.*
*ii) Chagua insha nyingine moja kutoka kwa hizo tatu zilizosalia.*
*iii) Kila insha isipungue maneno 400. Kila insha ina alama 20.*
*iv) Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**Maswali**
1. **Lazima**
Wewe ni naibu wa Mwalimu Mkuu katika shule ya Potoka. Hufurahishwi na matatizo ya kinidhamu ambayo yameongezeka shuleni humu. Andika **memo** kwa wakuu wa idara mbalimbali ukilalamikia visa mbalimbali na namna ya kukabiliana navyo
2. Fafanua umuhimu wa magazeti kwa mwanafunzi wa shule ya upili.
3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
Zimwi likujualo halikuli likakwisha.
4. Tunga kisa kitakachoanza kwa maneno yafuatayo:
"Dunia rangi rangile; analolitarajia mja halipati. Jamani maana ya methali hii, mgaa gaa na upwa hali wali mkavu ilibadilika?" Akajisemea Ridhaa huku machozi yakimtoka njia mbili mbili…..

---

**MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA GATUZI LA MUMIAS MAGHARIBI**
102/2
KISWAHILI
LUGHA
MUDA: SAA 2½

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**
***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Zaraa ndio uti wa mgongo wa taifa Ia Kenya. Viwanda vingi nchini hutegemea kilimo kama malighafi na kuwalisha wafanyakazi. Licha ya umuhimu wa sekta hii, mkulima ambaye ndiye nguzo ya zaraa anaendelea kukabiliwa na matatizo mbalimbali yanayokwamiza juhudi zake.

Mojawapo ya matatizo yanayomkabili mkulima ni ukosefu wa ushauri wa zaraa. Wataalamu wanaotarajiwa kumshauri mkulima kuhusu njia bora za kuzalisha na kuongeza pato lake ni haba ikilinganishwa na idadi ya wakulima wanaohitaji ushauri. Wachache walioko nao wanakwamizwa na mambo tofauti. Mathalani, utawapata hawaendi nyanjani ili kukutana na wakulima kwa kuwa hawana vyombo vya usafiri. Iwapo vipo, huenda petroli ikawa ni kizungumkuti. Halikadhalika, usisahau kuwa baadhi ya wataalamu hawa ni walazadamu au mafisadi. Kuna wale wanaofika ofisini na kushinda siku nzima wakisoma gazeti huku wakijaza miraba, wakicheza bao au karata. Kuna wale nao ambao hufika ofisini wakaangika koti au sweta kitini ili waonekane kuwa bado wapo na kisha kutokomea kwenda kushughulikia mambo yao ya kibinafsi yasiyohusu ndewe wala sikio kazi waliyoajiriwa kuifanya.

Ukosefu wa sera mwafaka kuhusu ardhi nalo ni tatizo jingine linalotatiza kilimo nchini. Serikali haijaweka sera mahususi kuhusu matumizi ya ardhi. Wananchi wengi huongozwa na taratibu za utamaduni za nasaba zao. Taratibu hizi hupendekeza ugawaji wa ardhi kwa minajili ya urithi kulingana na warithi waliopo. Si ajabu kuwa kote nchini, ardhi inayofaa kwa kilimo imekatwakakatwa vipande vidogovidogo ambavyo haviwezi kuwa na faida kwa zaraa.

Kushindwa kwa mkulima kuongeza virutubishi ardhini ni changamoto nyingine inayokabili kilimo nchini. Ulimaji wa kile kipande cha ardhi miaka nenda miaka rudi, bila kukipa nafasi ya kukipumzisha, huufanya mchanga kupoteza virutubishi muhimu vinavyohitajiwa na mimea. Hili nalo huchangia kupunguza uzalishaji wa mazao. Ili kutatua tatizo hili, wakulima wengi hukimbilia mbolea za kisasa ambazo badala ya kumsaidia, humwongezea madhila. Mbolea hizi zinatambulikana kuchangia uchafuzi wa mchanga na ardhi.

www.freekcsepastpapers.com

Mabadiliko ya hali ya anga nayo huongeza msururu wa madhila ya mkulima. Mabadiliko haya yamemfanya mkulima kushindwa kupanga wakati anaotakiwa kutayarisha shamba, kupanda, kupalilia, kunyunyizia dawa na kadhalika kwa sababu mvua imekuwa adimu. Badala yake panakuwa na vipindi virefu vya kiangazi ambavyo huathiri bidii za mkulima. Maji nayo yanaendelea kupungua na wakulima wengi hawawezi kukimu mahitaji ya unyunyizaji maji mashambani.

Maradhi pamoja na wadudu waharibifu kama vile viwavi, kupe na mbung'o ni changamoto nyingine inayotatiza juhudi za mkulima hapa nchini. Haya hupunguza uzalishaji wa mkulima au wakati mwingine kupunguza mifugo au mimea yake.

Kwa sadfa, iwapo mkulima ataweza kuzalisha mazao licha ya msururu huu wa vikwazo; ana tatizo jingine linalomngojea: ukosefu wa soko kwa mazao yake. Aghalabu, maeneo mengi yanayotoa mazao ya kilimo kwa wingi huwa na matatizo ya usafiri. Njia na barabara huwa mbovu na hazipitiki. Mazao mengi huwa hayafiki sokoni kwa wakati na huwa ni hasara kwa wakulima.

Fauka ya hayo, gharama ya uzalishaji wa mazao ya kilimo hapa nchini huwa ya juu zaidi kuliko faida anayopata mkulima. Watu wengi wameacha kutegemea kilimo kama njia ya ajira kwa kuwa hakilipi. Hii ni zaidi ya ushindani wa bidhaa za kilimo kutoka nje ya nchi ambao ni tatizo jingine linalomkabili mkulima. Mara nyingune wakulima wa kutoka nje ya nchi husaidiwa na serikabi zao kuzalisha mazao kwa kufidiwa au kupewa karadha. Mazao kama haya yaingiapo sokoni huuzwa kwa bei ya chini na hayawezi kushindana na yale ya wale wasiopata mchango wowote kutoka kwa serikali kama wakulima wa hapa nchini.

Mkulima wa Kenya anahitaji msaada wa dharura ili aweze kunyanyua kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa uchumi wetu. Lau haya hayatofanyika, uchumi wetu utaendelea kudidimia.

**Maswali**

(a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka . (ala.1)
(b) Kilimo kina umuhimu gani hapa nchini? (ala.2)
(c) Ni kwa nini wataalamu wa kilimo waliopo hawawafai wakulima nyanjani? (ala.4)
(d) Eleza sababu zozote **nne** zinazokinga mkulima kuzalisha mazao ya kutosha. (ala.4)
(e) Kwa nini watu wengi wameacha kutegemea kilimo kama njia ya ajira? (ala.2)
(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika taarifa. (ala.2)
    (i) Walazadamu
    (ii) Karadha

**2. UFUPISHO (ALAMA 15 )**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Mwana wa Adamu ni kiumbe cha ajabu! Ni kiumbe kilichopewa uwezo wa kuhodhi na kumiliki kila kitu; kiumbe kilichopewa akili na maarifa fuvu tele ili kuratibu shughuli na mambo; kiumbe kilichopewa uwezo wa kuwasiliana na kutumia sauti nasibu ili kuwa na urari na muwala; kiumbe kilichopewa uwezo wa kufaidi viumbe wengine kwa njia mbalimbali na jumla jamala; hiki ndicho kiumbe kilichopewa idhini maalumu ya kuzaana na kujaza dunia. Huyu ndiye mwana wa mama ambaye sasa amegeuka ndovu kumla mwanawe.

Kwa sababu ya bongo alizonazo, binadamu ana uwezo wa kutumia teknolojia kwa manufaa yake na ithibati zipo tele. Binadamu ametumia nyambizi kuzuru chini ya bahari; amefika mwezini; amevumbua mangala; amevumbua uyoka; amevumbua tarakilishi na sasa shughuli zake ni za kutandaridhi. Mwenyewe yuasema kuwa dunia yake imekuwa kitongoji katika muumano huu.Chambilecho wavyele, akili nyingi huondoa maarifa.Binadamu amekuwa dubwana linalojenga kushoto na kubomoa kulia na tuna sababu ya kulisoza dubwana hili kidole. Rabana ndiye msanii asiye mfanowe kwani aliisawiri dunia kwa kila lililo jema kwa siku sita mtawalia na kumpa binadamu mazingira murua. Rabuka akaona yote yalikuwa mema na mazuri; akamwambia binadamu, "Haya, twende kazi!"

Viwanda vya binadamu vinatiririsha maji-taka ovyo hadi mitoni, maziwani na baharini na matokeo yamekuwa ni vifo vya viumbe vya majini kama samaki ambavyo ni urithi aliopewa na Muumba. Hakuna kiumbe kinachoweza kustahimili maisha bila maji safi. Maji yote sasa yametiwa sumu na binadamu kwa sababu ya 'maendeleo' yake. Joshi kutoka katika viwanda vivyo hivyo nalo limehasiri ukanda wa ozoni ambao sasa umeruhusu jua kutuhasiri kwa joto kali mno. Siku hizi inasemekana kuwa kuna mvua ya asidi inayonyesha katika baadhi ya sehemu za dunia na kuleta madhara makubwa. Labda hata mabahari yamekasirika kwa sababu hivi majuzi katika kile kilichoitwa 'tsunami' bahari lilihamia nchi kavu na kusomba maelfu ya binadamu na kuwameza wazima wazima. Vimbunga navyo vimetokea kwa wingi. Wataalamu wanasema kuwa viwango vya miyeyuko vitazidi kwa sababu ya joto na kiwango cha maji kitazidi pia. Binadamu atatorokea wapi?

www.freekcsepastpapers.com

Idadi ya binadamu imezidi hadi kiasi asichoweza kukishughulikia kwa sababu anaijaza kiholela kwa sababu anadai kuwa aliruhusiwa kuijaza. Hii ni imani potovu. Anasahau kuwa alipewa ubongo wa kuwaza na kuwazua kabla ya kufanya chochote. Dhiki, maradhi na ufukara zimehamia kwa binadamu na kumtia kiwewe.

Binadamu amefyeka misitu kwa kutaka makao, mashamba, mbao, makaa, ujenzi wa nyumba na barabara na mahitaji mengine mengi. Wanyama wamefurushwa na wengi kuangamia kwa sababu ya ukosefu wa chakula na wengine kushindwa kuhimili mabadiliko katika mazingira. Chemichemi za maji zimekauka nalo jangwa limeanza kutuzuru kwa kasi inayotisha. Kazi ya binadamu imekuwa ya kusukia kamba motoni. Itambidi aanze kujenga kwa matofali ya barafu!

**Maswali**

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa taarifa, fupisha aya mbili za kwanza.
(Maneno 50-60) (alama 7)
Matayarisho/ Jibu

(b) Kwa kuzingatia aya tatu za mwisho, eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi.
(Maneno 85 – 95) (alama 8)
Matayarisho / Jibu

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40 )**

a) Taja mifano **miwili** ya sauti mwambatano. (alama 1)

b) Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (alama 1 )
Maseremala walilainisha mbao hizo wakatutengenezea meza.

c) Bainisha silabi zitakazowekwa shadda katika maneno yafuatayo: (alama 2)
i. miambakofi
ii. yatazoleka

d) Tumia neno **'hawa'** katika sentensi kama ; (alama 2)
Kiwakilishi
Kivumishi

e) Ainisha vihusishi katika sentensi ifuatayo; (alama 2)
Babu alifika mapema kuliko wote halafu akaondoka.

f) Andika sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 2)
KN (N+RH)+KT(TS+T)

g) Tumia kitenzi " Fa " katika sentensi kuonyesha mazoea (alama 1)

h) Andika neno lenye muundo ufuatao wa silabi. (alama 2)
i. irabu,konsonanti,konsonanti,irabu,konsonanti,irabu
ii. konsonanti,konsonanti,irabu,irabu

i) Weka maneno haya katika **ngeli** zake. (alama 2)
Miwani
vyanda

j) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo. (alama 3)
Aliyesamehewa

k) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia maneno yaliyopigiwa mstari ( alama 2)
Punde tu **alipouliza** swali hilo Halima **aliingia** darasani

l) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Viwanda vikianzishwa mashambani idadi ya wanaohamia mjini itapunguzwa.

m) Tambua yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Juma alimtunzia Kuta watoto hao kwa upendo.

n) Yakinisha sentensi ifuatayo (alama 2)
Badi huwa hapitii hapa , huenda usimpate.

o) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Viongozi wengine watasafiri ughaibuni kesho.

p) Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa (alama 1)
Mtu huyo alifuata njia iliyomwelekeza mjini.

q) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)
"Nitamwalika kesho jioni ." Fatuma akasema.

r) Changanua sentensi hii kwa kielelezo cha mstari (alama 2)
Mvua imepusa na watu wameanza kuondoka.

www.freekcsepastpapers.com

s) Kanusha ; (alama 2)
Mbao hizo zilihifadhiwa ili ziuzwe mjini.

t) Zito ni kwa jepesi, ___________ ni kwa choyo, na _____________kwa kali. (alama2)

(u) Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno: **zima** (alama 2)

**4. <u>ISIMU JAMII</u> (ALAMA 10)**

**<u>Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali</u>**

"Kwa mujibu wa ushahidi uliotolewa, mahakama hii imethibitisha bila chembe ya shaka kwamba wewe mshtakiwa, Bi. Mlachake Chauchau ndiye uliyepika pombe haramu ambayo ilisababisha vifo vya raia hamsini na kupofuka kwa wengine mia moja. Unahukumiwa kwa kosa la mauaji. "

a) Bainisha **sajili** ya makala haya kwa kutoa mifano **miwili** kutoka kwenye makala. (alama 2 )

b) Fafanua sifa nyingine **nane** za sajili hii ambazo zingejitokeza katika makala haya (alama.8 )

---

**<u>MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA GATUZI LA MUMIAS MAGHARIBI</u>**
**<u>102/3</u>**
**<u>KISWAHILI</u>**
**<u>KARATASI YA 3</u>**
**<u>FASIHI</u>**
**<u>MUDA: SAA 2½</u>**

**Maagizo**

(a) Jibu maswali **<u>Manne</u>** pekee
(b) Swali la **kwanza** ni **la <u>Lazima</u>**
(c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Tamthlia, Hadithi fupi na Fasihi simulizi
(d) Usijibu maswali **<u>Mawili</u>** kutoka **<u>Sehemu Moja</u>**

**LAZIMA SEHEMU A : SHAIRI**

**1. Soma shairi lifuatalo kwa makini, halafu ujibu maswali yanayofuatia**

Hakika yamekithiri, ni asoyajua?
Wazazi wayahubiri, na hivyo kutubagua
Hayana kamwe fahari, ila kweli yatua.
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

Mwanamke siyo huyo? Baba mtu anasema
Mwanamke kwani huyo? Anateta naye mama,
Sababu waitoayo, haina nguvu wima,
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

Kabila letu ni hili, sharuti uoe huko,
Unazomewa ukali, kuoa nje ni mwiko.
Hivyo twafanywa dhalili, viumbe tuso mashiko
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

Wanachunguza tabaka, ndipo wazushe wahaka
Wauliza kwa haraka, wajue lake tabaka,
Wasioridhika wafika, arudi alikotoka,
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

Waichuja yake dini, ndo ndoa ibarikiwe
Lazima yake imani, iwe sawa na yakuwe
Huu kweli ni uhuru, wataka uondolewe,
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

www.freekcsepastpapers.com

Japo mwanipa elimu, uhuru ninautaka,
Na mie muniheshimu, nipate nilomtaka
Kuoa kitu adhimu, so mchezo kwa hakika
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

Nawashauri wazazi, twahitaji kupumua,
Wawili ndo waamuzi, haa Mungu anajua,
Wasifu pasi ajizi, kwa yao njema hatua,
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

Ndoa akivunjikana, wawili wajisakeni
Isije kusemekana, wazazi ndio kiini,
Ndiposa hata Rabana, situtie lawamani,
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

Aliye na masikio, mesikia kwa makini,
Tusitamani kilio, mtihani tulo vitani,
Wakioa sema ndio, Mola asikulaani
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (al.1)
(b) Shairi hili laweza kuwekwa katika bahari mbili. Zitaje huku ukitoa mifano. (al.2)
(c) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (al.2)
(d) Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili. (al.4)
(e) Jadili muundo wa shairi hili. (al.4)
(f) Taja aina mbili za urudiaji katika shairi. (al.2)
(g) Ukizingatia shairi ulilopewa, eleza jinsi mshairi alivyotumia uhuru wake. (al.2)
(h) Taja toni ya shairi hili. (al.1)
(i) Eleza maaana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwa shairi. (al.2)
(i) Wahaka
(ii) Yamekithiri

**SEHEMU YA B : RIWAYA**

**A. Matei: chozi la heri**
**Jibu Swali la 2 Au la 3**

1. Alikuwa ameumwa na nyoka. Bafe hasa na bila shaka mwenyewe kuumwa na nyoka akiona ung'ongo hushtuka.
(a) Eleza muktadha wa kauli hii. (al.4)
(b) Fafanua sifa tatu za mrejelewa. (al.3)
(c) Thibitisha namna wahusika kadhaa walivyoumwa na nyoka katika riwaya. (al.13)

2. (a) Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo. (al.10)

Hata hivyo, tulijipa kuamini kwamba haya ndiyo yaliyokua majaliwa yetu, tuliikuwa wenye haja, maiti hasa na tangu hapo maiti hachagui sanda wala jeneza.

Tulivumilia tukidhani hali itatengenea, tukiamini kwamba tungerudi kwetu lakini, lo! Wanasema wajuao kuwa msitu ni mpya ila nyani ni wale wale uongozi mpya haukuleta ahueni yoyote katika maisha yetu! Kilicho badilika nikikwamba tulipwa ardhi zaidi ya kujengua mabanda zaidi ili kupunguza msongamano katika mabanda ya awali. Bado tu pale pale…sioni kama pana nyumbani pema zaidi ya pale kambini. Vumilia mwenzangu zingatia masomo yako kwani ndiyo yatakayokuvusha kutoka kwenye lindi hili la huzuni. Baada ya kusema haya, Kairu alitulia kwa muda kama mtu anayevuta fikra.

(b) Jadili jinsi maudhui ya ndoa yamejitokeza katika riwaya ya chozi la heri. (al.10)

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA**
**Bembea ya Maisha.**
**Jibu swali la 4 au 5.**

**4.** Basi usijipandishe presha mama!
(i) Eleza muktadha wa dondoo. (al.4)
(ii) Bainisha vipengele viwili vya kimtindo vinavyojitokeza katika dondoo. (al.2)
(iii) Eleza sifa za msemewa. (al.4)
(iv) Jadili jinsi maudhui ya utamaduni yanavyojitokeza katika tamthilia. (al.10)

**5.** Basi tu! Wenzenu ndio walioniingiza kwenye mkondo huu. Kama unakumbuka nilikuwa miongoni mwa vijana wa kwanza kuingia kwenye dini.
(i) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (al.4)
(ii) Eleza toni inayojitokeza katika dondoo. (al.2)
(iii) Jadili mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo. (al.4)
(iv) Jadili umuhimu wa mzungumzaji katika dondoo hili. (al.10)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**
**Mapambazuko ya machweo na hadithi nyingine**
**Jibu swali la 6 au 7.**

**6. Fadhila Za Punda**
Alimfungulia mlango akitetema kama unyasi upeo uvumapo. Mara akashika nywele karibu zing'ooke kisha akabururwa hadi kwenye chumba cha malazi. Si kipigo hicho, si makofi, si ngumi, si mateke tena ya mtu aliyevaa buti.
(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
(ii) Bainisha taswira zinazojitokeza katika dondoo hili. (al.2)
(iii) Eleza sifa nne za mrejelewa. (al.4)
(iv) Kwa kurejelea hadithi hii eleza jinsi maudhi ya nafasi ya mwanamke yalivyojitokeza. (al.10)

**7.** Ukombozi wa wanawake unakumbwa na vizingiti vingi sana. Jadili ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya Sabina. (al.20)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**
**8. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Zamani sana Paka na Mbwa waliishi peponi. Mungu alikuwa amewatunukia mapenzi si haba. Nyumba yao ilikuwa imepambwa kwa vyombo vya dhahabu na vito vingine. Bustani kubwa lilizunguka nyumba hiyo ya fahari. Matunda ya kila aina: si matikiti, si maembe, si matufaha, si machungwa; yote yalijaa kochokocho mitini. Alimuradi Paka na Mbwa hawakupungukiwa na lolote. Wanyama wengine hawakuisha kuwaonea kijicho wanyama hawa.

Siku moja, Malaika Mkuu mbinguni alikuwa na ujumbe kwa Mungu. Aliamka asubuhi na mapema na kuwaita Paka na Mbwa ambao walikuwa wamejipambanua kama watumishi waaminifu na kuwaambia, "Ndugu zangu, nina salamu muhimu ambazo ningependa kuwakabidhi mmpelekee Mungu. Kwa vile ujumbe wenyewe ni mrefu, nimeuandika na kuutia ndani ya bahasha hii. Basi nitakukabidhi ewe ndugu yangu Mbwa bahasha hii. Ni sharti uitunze isije ikakuponoka njiani". Mbwa akachukua bahasha na kuitia ndani ya mfuko wa shati lake.

Kabla ya Paka na Mbwa kupondoka, Malaika Mkuu aliwaambia, "Pana jambo ambalo ningependa kuwatahadharisha nalo. Msizungumze na yeyote wala chochote hadi mtakapofika kwenye kasri la Mungu."

Maneno haya ya mwisho yalimwia Mbwa vigumu. Alijua kuwa yeye hakuwa mzungumzaji kiasi hicho lakini kuambiwa asile chochote na hali safari hiyo ingewachukua kutwa mzima! Alichojua, kama alivyojiwazia, ni kwamba hata Malaika Mkuu asingeweza kuwa na stahamala wa kiwango hicho!

Safari ilianza saa moja asubuhi baada ya staftahi. Paka na Mbwa wakaandamana guu mosi guu pili. Jua la utosi liliwapata hata kabla ya kufika nusu ya safari. Njaa ilikuwa imeanza kuwauma, uchovu ukawa

www.freekcsepastpapers.com

unawang'ata kama nge. Hata hivyo, walijipa moyo, wakajiambia kuwa subira yao itavuta heri baada ya muda mfupi.

Ghafla kama ajali, sungura alitokea katika kichaka kilichokuwa karibu. Macho ya Mbwa ndiyo yaliyokuwa ya kwanza kumtua sungura huyo. Moyo wake ukamzaini kukitwaa kisungura hicho na kukonga roho yake. Mara alikumbuka onyo ambalo walikuwa wamepewa na Malaika Mkuu. Mvutano mkali ulizuka katika nafsi yake, "Bwana wewe una njaa, vipi utatakiacha kitoweo ambacho kwa kweli kinakunyooshea mkono?" kwa upande mwingine dhamiri yake ilimuasa na kumwambia, "Mwenye pupa hadiriki kula tamu, tuliza moyo wako, usikaidi amri ya mtumishi wa Mungu usije ukauma dole."

Basi mjukuuu wangu, Mbwa akawa hajifai kwa mgogoro huu wa nafasi. Mara uhayawani wake ulimvaa, akafyatuka kama mshale na kumhujumu Sungura. Akamla asimbakize chochote! Kwisha kumla, akamwambia Paka, "Ndugu, tuendelee na safari, huenda hata wewe ukabahatika kuambulia angaa buli la maziwa."

Hatua chache mbele, Panya alitokea. Akajishaua mbele ya marafiki zetu hawa kama kwamba alitarajia posa kutoka kwa mmoja wao. Moyo wa Paka ulimpapa kwa tamaa ya kutaka kulipiza kisasi kwa kiumbe huyu ambaye daima alizoea kuyahujumu maghala ya mahindi. Paka akamtazama Panya kwa jicho la hasidi, akatayarisha mafumba yake kwa vita. Lakini ghafla akakumbuka maneno ya Malaika Mkuu na kujiasa. Alimnyoshea Panya kidole na kumwambia, "Laiti Malaika Mkuu asingekuwa amenionya dhidi ya kula chochote, ningekufunza funzo la maisha." Basi Panya akanusurika.

Sasa walikuwa wakitazama kasri la Mungu. Kwa mbali, mbwa alikaza mboni zake zaidi na kumwona Swara akija kwa madaha. Ziraili akamwingia, "Kaka Mbwa, natumai unakumbuka walivyotwambia wahenga kuwa ngojangoja huumiza matumbo. Je, una hakika gani kuwa baada ya kufikisha ujumbe utapewa hata tone la maji? Hamadi kibindoni Bwana. Faida chajio ukionacho sasa. "bila nadhari, Mbwa alimtwaa Swara na kumla shibe yake.

Jua lilipozama Paka na Mbwa walijipata nje ya lango la kasri. Mungu akatoka kwenye chumba chake cha maongezi na kwenda kupokea salamu zake. Akamwuliza Mbwa, "Je, safari ilikuaje?" Mbwa akajibu, "Safari ilikuwa ndefu, lakini yenye mafanikio makubwa. Niliweza kuwashika sungura na Swara na kuwala. Njaa haikunidhili mno, ila bahasha niliyopewa ilipotea njiani. "Mungu akamjibu, "Subiri hapo nje ya lango. Nitakuita baada ya kuzungumza na Paka. "Paka alipoulizwa, alijibu kwa sauti hafifu, "Safari ilikuwa ndefu mno. Sikuweza kuzungumza na yeyote. Nilitaka kulipiza kisasi kwa Panya niliyekutana naye ila sikuweza kwani Malaika Mkuu alikuwa ametuonya dhidi ya hayo." Mungu alimpa pole kwa hayo. Akamkaribisha ndani ya kasri na kumpa sharubati kwanza. Mbwa akabaki nje akisubir. Tangu siku hiyo, Mbwa daima husubiri nje naye Paka huishi ndani ya nyumba. Hadithi yangu inaishia hapo.

www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Hiki ni kipera cha aina gani? Thibitisha. (al.2)

(b) Changanua mbinu za kimtindo katika utungo huu. (al.10)

(c) Eleza namna hadhira inavyoweza kushiriki katika uwasilishaji wa utungo huu. (al.4)

(d) Jadili jinsi jamii ya kisasa inavyojaribu kuendeleza Fasihi simulizi. (al.4)

**CHOGORIA - MURUGI ZONE**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1:**
**MUDA: SAA 1 ¾**

a) *Andika insha* ***mbili.*** *Insha ya kwanza ni ya* ***lazima.***
b) *Kisha chagua insha nyingine moja kato ya hizo tatu zilizobaki.*
c) *Kila insha isipungue maneno* ***400***
d) *Kila insha ina alama 20.*

1. Umealikwa kama mlumbi katika kata ndogo ya Matopeni kuhutubia wakaazi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira. Andika hotuba utakayoitoa.
2. Ukosefu wa ajira nchini ndicho chanzo kikuu cha utovu wa maadili nchini. Thibitisha.
3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi.
4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa………………………………………………… Baada ya kutafakari nilimshukuru Mola kwa kuniokoa.

---

**CHOGORIA MURUGI ZONE**
**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**MUDA: SAA 2½**

**MAAGIZO**
1. *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulioachiwa hapo juu.*
2. *Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.*
3. *Jibu maswali yote.*
4. *Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

www.freekcsepastpapers.com

**1. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia**

Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamii linalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanaoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofauti tofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochakaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulozi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto walioachwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hili husababisha dhana gande. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto, awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – ninawavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hili walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozurura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. <u>Inakera</u> zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimzaa mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi, aliyeachiwa ana jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa Jalali, kila anayeupuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama!

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ya chekechea had kidato cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa, ni kweli. Hata hivyo, wengi hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya chekechea, hivyo

kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21, asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa majukumu mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyishwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazazi wao waagapo nakuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya simba kumlilia swara! Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku mwanamkiwa yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata awaoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.

Baadhi ya waja walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale hushia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine hushia kutumiwa kama watumwa wa 'kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. Kujinasua kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali 'mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa' kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaidika wenyewe.

**Maswali**

**a)** Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alama 1)**

**b)** Eleza dhana ya mwanamkiwa kwa mujibu wa kifungu. **(alama 2)**

**c)** Eleza imani za kijadi kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 2)**

**d)** Jadili masaibu yanayowakumba wanawakiwa. **(alama 4)**

**e)** Eleza haki mbili za kikatiba zilizokiukwa kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 4)**

**f)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na kifungu. **(alama 2)**

**i)** Inakera

**ii)** Majukumu

2. **UFUPISHO: (Alama 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasiliano kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundishia. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkemu kwa mtu wa kila rika. Halikadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji wa stadi ya kujifundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu, huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemchemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo ya vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu huwa ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro tunayokabiliana nayo kila siku. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga huwa ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu, ubaya wa kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia, kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanaowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii. Ukilinganisha na vyombo vingine vya

www.freekcsepastpapers.com

burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake, tajriba ya televisheni huwa ya kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalani, baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa, n.k. Hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya dawa za kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaotumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya wawaelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

a) Fupisha aya tatu za kwanza (maneno 70 – 75) (alama 7, 2 za utiririko)
Matayarisho
Jibu

b) Eleza udhaifu wa runinga na video. (maneno 50 – 51) (alama 5, 1 ya utiririko)
Matayarisho
Jibu

3. **MATUMIZI YA LUGHA:** **(alama 40)**

**a)** Taja aina mbili kuu za ala za kutamkia sauti **(alama 2)**

**b)** Taja mfano mmoja mmoja wa sauti zifuatazo **(alama 2)**
Kimadende________________________________________
Kipasuo kwamizo____________________________________

**c)** Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi sahili **(alama 2)**

**d)** Ainisha mofimu katika neno lifuatalo; **(alama 3)**
Tulimpikia________________________________________

**e)** Ainisha vitenzi katika sentensi: Kitabu anachotaka kusoma ki mezani **(alama 3)**

**f)** Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi kiteuzi **(alama 2)**

**g)** Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama 2)**
a) Uzi____________________
b) Muda__________________

**h)** Tumia 'o' rejeshi ya kati katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**
Watu ambao walifika jana ni wale ambao walitoka mbali

**i)** Onyesha shamirisho kipozi na ala katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**
Mwindaji haramu alimuua ndovu kwa bunduki

**j)** Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale **(alama 3)**
Kilipikwa jana jioni

**k)** Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi **(alama 2)**
Msingesoma kwa bidii, msingepita

**l)** Tunga sentensi moja kudhihirisha dhamira/jukumu hili **(alama 2)**
Rai/ombi

**m)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**
Mtoto ambaye alianguka jana ana maumivu mengi

**n)** Onyesha matumizi yoyote mawili ya kiwakifishi: koma/kituo **(alama 2)**

**o)** Tumia neno 'Nairobi' kama **(alama 2)**
**a)** Nomino
**b)** Kielezi

**p)** Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya kuku na gugu **(alama 2)**

www.freekcsepastpapers.com

q) Onyesha matumizi ya kiambishi -ji- katika sentensi (alama 2)
Mwongeleaji stadi anajishaua sana.

r) Andika katika usemi wa taarifa (alama 2)
"Wageni wangu watafika saa ngapi? Mama aliuliza

s) Unda nomino kutokana na kitenzi (alama 1)
Safiri

4. **ISIMU JAMII:** **(alama 10)**
Nipe chai, andazi mbili na egg moja…………

a) Taja sajili inayorejelewa na maneno haya **(alama 2)**

b) Fafanua sifa nane zinazohusishwa na sajili hiyo **(alama 8)**

**CHOGORIA - MURUGI ZONE**
**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI**
**KARATASI YA 3**
**MUDA: SAA 2 ½**

**MAAGIZO**

*a) Jibu maswali manne pekee.*
*b) Swali la kwanza ni la lazima.*
*c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; tamthilia, riwaya, hadithi fupi na fasihi simulizi.*
*d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
*e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA A: USHAIRI**
**SWALI LA LAZIMA**
**MBELE YA SAFARI**

1. Ilipoanza safari , ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

2. Njaa ikawa dhabiti ,na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti, dhila na mingi mikiki
Tukajizatiti

3. Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari, utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari, juhudi iliyobaki
Tukajizatiti

4. Ile ilikuwa ndoto , mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto, sahala 'mekuwa dhiki
Wagombanio kipato, utashi haukatiki
Nakutabakari

5. Msafara ukasita , kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita, mlima haupandiki
Basi sote 'kijipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

6. Tukiwa migongo wazi ,tukainama kwa shaki
Tukawa'chia ukwezi, kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi, kuteremsha miliki
Wakaitapia

7. Wakafikia makazi, ya pumbao na ashiki
Huko wakajibirizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

8. Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema, kwa umati halaiki
Imezima nia yote, kiza hakitakasiki
Mbele ya safari

a) Eleza safari inayolejelewa katika shairi hili. (al 2)
b) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa. (al 6)
c) Taja na ueleze bahari mbili za shairi ukizingatia : (al 4)
i. Mizani ;
ii. Vina
d) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. (al 4)
e) Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita. (al 4)
f) Eleza umbo/ muundo wa shairi hili. (ala 2)

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA**
**Timothy Arege**
**BEMBEA YA MAISHA**

2. Hiyo ndio ajabu! Kizazi hili hakitaki kufanya kazi. Kinataka kuja kazini kwa sababu ya mshahara tu. Wachapa kazi hodari ni njozi iliyopotea.
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala 4)
b) Eleza sifa za msemaji wa dondoo hili. (ala 4)
c) Fafanua imuhimu wa msemewa katika kazi ya Bembea ya Maisha. (ala 4)
d) Taja na uonyeshe mbinu za uandishi zilizotumika katika dondoo. (ala 4)
e) Eleza maudhui yanayokuzwa katika muktadha wa dondoo. (ala 4)

3. Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha. (ala 20)

**SEHEMU YA C: Riwaya**
**Assumpta Matei**
**Riwaya ya Chozi la Heri**
**Jibu swali la 4 au 5**
4. "Siku moja nitakuwa mtetezi wa haki za kibinadamu, hususan haki za watoto."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)
b) Jadili sifa tano za mzungimzaji. (ala 5)
c) Kwa kutumia hoja kumi na moja. Onyesha jinsi jamii ya wahafidhina inavyokiuka haki za watoto. (al 11)

www.freekcsepastpapers.com

**Au**

5. Onyesha jinsi maudhui ya usaliti yanavyojitokeza katika riwaya ya Chozi la Heri. (al 20)

**HADITHI FUPI**

**D.W Lutomia na Phibbian Muthama:** ***Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine***

**Jibu swali la 6 au la 7**

6. "Isije ikawa mwenye nyumba kuja na yeye mpangaji akachelewa kumfungulia mlango; itakuwa balaa bin beluwa"

i. Eleza muktadha wa dondoo hili (ala 4)

ii. Jadili umuhimu wa mwenye nyumba anayerejelea (ala 6)

iii. Maisha yalikuwa balaa bin beluwa kwa mpangaji. Thibitisha (ala 10)

*7.*

***(a)*** Machoka alikumbuka kauli ya jirani yake, Zuhura, aliyeishi kumkumbusha, "wetu ni wetu, hata akiwa mbaya … wetu. Hatuna budi ila kumchagua yeye. Lisilobudi hubidi. Awe amesoma ama hajasoma, angali wetu." leo hii hata Zuhura mwenyewe alikuwa anajutia kumchagua huyo wetu.

Kwa muda mrefu, Machoka na Zuhura walikuwa kama fahali wawili hawakai katika zizi moja. Kisa na maana, ni wafuasi wa watu wawili tofauti. Leo hii kinachowaleta pamoja Machoka na Zuhura ni udhikinifu, hali ngumu ya maisha, mfumuko wa bei za bidhaa muhimu na kutozwa ushuru wa kiwango cha juu na serikali hiyo hiyo ya 'watu wao'. Zuhura alisuta nafsi yake. Alikuwa akiitazamia nchi nzuri na maisha bora baada ya uchaguzi. Alitazamia 'watu wake' wangezitimiza ahadi walizozitoa wakati wa kampeni zao. Leo hii imebakia kujuta. Kujuta ghya ya kujuta! Tayari alikuwa amekwishafanya kosa. Kosa ambalo alifahamu lilikuwa la kujitakia. Ulikuwa mwiba wa kujidunga usiokuwa na kilio wala kuambiwa pole. Maji yalikuwa yashamwagika, katu hayangeweza kuzoleka…"

Chambua maudhui katika dondoo hili. (ala 12)

(b) Eleza sababu nne zinazochangia jimbo la Matopeni kutoshuhudia maendeleo ya kisiasa tangu nchi kupata uhuru . (ala 8)

**SEHEMU YA E**

**FASIHI SIMULIZI**

8. i) Eleza maana ya misimu. (al 2)

ii) Taja mambo manne ya kimsingi yanayochangia kuchipuka kwa msimu. (al 4)

iii) Eleza umuhimu wa misimu katika jamii. (al 10

iv) Taja sifa nne za misimu. (al 4)

www.freekcsepastpapers.com

**KIGUMO 1**
***Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)***
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**INSHA**
**MUDA: SAA 1 ¾**

***Maagizo.***

***a)*** *Andika insha mbili: insha ya **kwanza** ni ya **lazima***
***b)*** *Kisha chagua Insha nyingine **moja** kutoka kwa zile zilizobaki*
***c)*** *Insha yako isipungue maneno **400***
d) *Kila insha ina alama **20**.*

**1. Lazima**
Wewe ni mhariri wa gazeti la *Mwanzo Mpya*. Andika tahariri kuhusu umuhimu wa vyama vya wanafunzi shuleni.
**2.** Asasi mbalimbali katika jamii zafaa kushughulikia kuwepo kwa mshikamano wa kitaifa. Fafanua.
**3.** Tunga kisa kinachodhihirisha maana ya methali ifuatayo;
Pang`okapo jino pana pengo.
4. Tunga kisa kitakachomalizika kwa maneno; ".....Kisa hiki kilinifundisha kwamba kuzaliwa maskini si hoja"

**KIGUMO 1**
***Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya***
**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**MUDA: SAA $2^1/_2$**

**1. UFAHAMU (Alama 15)**
***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.***

Kijiji cha Mulukoba kilikuwa na utulivu wa aina yake. Okolo alikuwa miongoni mwa wazaliwa wa eneo hilo. Katika miaka ya tisini alikuwa ameanza safari yake ya masomo katika shule ya msingi ya Magombe. Enzi hizo mshawasha na imani za watu zilihusu tu maswala ya elimu.

Okolo alifurahishwa na utangamano wa kijiji chao. Watu walishirikiana kazini, sherehe za arusi na matanga. Aghalabu shughuli ya mtu iligusa mwenzake. Anakumbuka vizuri ngoma zilizopigwa katika sherehe mbalimbali. Wanakikundi cha ``alaki'' wakiongoza ilikuwa burudani ya aina yake. Na je, baragumu lililopulizwa na Achwari kuwaita watu kununua nyama na kujuza watu kuwa fulani ameaga? Kwa kweli Mulukoba kilikuwa kijiji chenye ufanisi.

Kando na hayo, vyakula walivyokuwa navyo hasa samaki waliovuliwa mto Akanyo hususan kambare, walikuwa na ladha ya kupendeza. Okolo alifurahia sana samaki wa kukaushwa `kerewa' namna wanakijiji walivyoita. Huyu alikuwa chaguo lake. Mamake alipopika siku hiyo basi ukamilifu ulijaa moyoni mwake. Okolo alitumai kuwa atakapooa, basi mkewe ni sharti afahamu kuwa `kerewa' ndicho chakula chake. Mto huu pia ulikuwa kitovu cha michezo ya kitoto, ulikuwa na vivukio vitatu, kwa Alaki, kwa Nikola na Bobobo. Kidimbwi kizuri cha kupiga mbizi kilikuwa kivukio cha Nikola. Vivukio hivi viliitwa majina haya kutokana na mwenye ardhi palipo kivukio hicho. Mazingira ya pale pia yalimpendeza. Hili humfanya akumbuke hadithi aliyosoma chuo kikuu ya E. Kezilahabi kuhusu Mayai Waziri wa Maradhi wakiogelea mtoni. Enzi hizo za miaka ya tisini mwanzo mtu hakujisumbua na lazima ya sabuni. Mradi umeona maji, kilikuwa na mawe ya kusugua mguu pale mtoni, wengine wangetumia mchanga nayo sabuni ilikuwa harita au matawi ya mti walioita `sabuni ya wazee'. Yaani, wakati huo binadamu alitumia maliasili kwenye shughuli zake za kila siku. Leo hii, anapojitia marashi na hata mkewe kumkumbusha aina za sabuni nzuri, hucheka pasi yeyote kutambua kiini cha kicheko hicho.

Je, ukarimu nao wa wanakijiji. Enzi hizo watu walisaidiana. Anakumbuka babake akiwaalika wanakijiji katika sherehe tu za burudani. Atoka mchezo tiriri akiongoza burudani huku wengine wakila na kunywa. Bangaradesi mmoja wa wanakijiji angecheza wimbo wa Atoka kwa miondoko yote. Huo ndio ukamilifu uliokuwepo. Anakumbuka wagema wawili waliofahamika sana, Akong`o na Majimaji. Majimaji

www.freekcsepastpapers.com

Kwa muda mrefu, baa la njaa limekuwa likihusishwa na maeneo ya kaskazini mwa nchi yetu; lakini kama uchunguzi ulivyoonyesha, familia nyingi nchini zinaumia na wengi hawawezi kumudu bei ya bidhaa muhimu kama sukari, unga, mafuta ya kupikia na kadhalika.

Wakati umewadia kwa serikali kuchukua hatua madhubuti kwa kuwa kama ilivyo ni vigumu kumtawala mtu aliye na tumbo tupu na ambaye hajijui wala hajitambui kuhusu atakapopata lishe.

a) Ukizingatia taarifa uliyosoma fafanua athari za mfumko wa bei kwa wananchi.
(maneno 35-40) alama 6, 1 mtiririko
**Matayarisho /Nakala safi**

b) Eleza mambo muhimu anayoyazungumzia mwandishi katika aya za mwisho **tatu**
(maneno 60-65) alama 8,1 mtiririko
**Matayarisho / Nakala safi**

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

a) Andika neno lenye kikwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya mbele wastani, nazali ya midomo na irabu ya chini kati. al 1

b) Bainisha uamilifu wa viambishi katika neno lifuatalo: al 2
viliwavyo

c) Eleza muundo wa silabi katika neno **mbilikimo**. al 2

d) Tunga sentensi moja yenye kiwakilishi cha A-unganifu, kitenzi kishirikishi kipungufu na kijalizo. al 2

e) Kanusha sentensi ifuatayo katika wingi. al 2
Mwanafunzi huyo akisoma kwa bidii atapita

f) Ainisha vihusishi katika sentensi zifuatazo: al 2
a) Tunu ni mrembo kama mama yake.
b) Watawasili kufikia juma lijalo.

g) Tambua virai katika sentensi ifuatayo: al 2
Wenye bidii kazini wamesifiwa sana bungeni

h) Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha kulinganisha al 2

i) Andika katika usemi wa taarifa al 2
"Wanasiasa hawa wenu wakipigana hivi wataharibu nchi" Rais alisema

j) Changanua sentensi kwa kielelezo cha jedwali
Jirani mzuri aliyenisaidia juzi ataondoka mwaka ujao. al 4

k) Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo al 3
Alawi alifumiwa mkeka mzuri na shangaziye kwa miyaa.

l) Tambua aina za vishazi katika sentensi al 2
Lazima nile lishe bora ili niwe mwenye afya.

m) Ainisha sentensi ifuatayo ukitumia vigezo **<u>viwili</u>** vikuu al 2
Wanafunzi walikuwa wakiamka mapema.

n) Bainisha maana mbili za sentensi ifuatayo. al 2
Mapunda alisema kuwa mkewe amesafiri.

o) Andika sentensi ifuatayo katika wingi. al 1
Onyesha kivumishi katika sentensi ifuatayo.

p) Geuza sentensi zifuatazo katika nyakati na hali katika mabano. al 2
i) Wanafunzi wanafanya mtihani (ujao hali timilifu).
ii) Mtoto amekunywa maziwa (uliopita hali ya kuendelea)

q) Huku ukitoa mifano mwafaka, onyesha miundo miwili ya ngeli ya U-ZI al 2

r) Tunga sentensi yenye kitenzi halisi. al 1

s) Andika sentensi upya kulingana na maagizo al 2
<u>i)</u> <u>Miti</u> ilikatwa <u>Nairobi.</u> (Tumia viwakilishi vya maneno yaliyopigiwa mstari)
<u>ii)</u> Mtoto amekula wali. (Geuza katika kauli ya kutendwa)

t) Onyesha matumizi ya **ki** katika sentensi hizi: al 2
i) Hakijapikwa
ii) Alinunua kimeza hafifu

www.freekcsepastpapers.com

**4. ISIMU JAMII (Alama 10)**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali;***

MTU 1: Una shida gani?

MTU 2: Kichwa chaniwanga, tumbo lanisokota na ninahisi uchovu mwingi. Nisaidie tafadhali.

MTU 1: Pole, afya yako itakuwa shwari. Hizi tembe hapa zitakusaidia kupunguza maumivu. Unapaswa kuzitumia mara tatu kwa siku…

(a) (i) Tambua sajili hii al 1

(ii) Kwa kutolea mfano, andika sifa **nne** ambazo zinahusishwa na sajili hii. al 4

(b) Umepewa jukumu la kuendesha shughuli ya mazishi kijijini mwako. Fafanua sifa **tano** za lugha utakayotumia wewe na waombolezaji wengine. al 5

---

**KIGUMO 1**
***Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya***
**102/3**
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 3**
**FASIHI**

**Maagizo**

- ✓ Jibu maswali **manne** pekee.
- ✓ Swali la **kwanza** ni la **lazima.**
- ✓ Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.
- ✓ Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja.**
- ✓ Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**SEHEMU A; USHAIRI**

**1. LAZIMA**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Nazuka mtunga mambo, na watunzi watungao
**Wafungatao masombo**, kushika msu na ngao
Naipiga ya mgambo, sauti ifike kwao
Wawapi wajigambao, tungambiyane vigambo?

Ni siku nyingi kitambo, **ninyemele** naja leo
Kama kweli wana nyimbo, nawaje niimbe nao
Na sababu ni vingambo, vya wale wajitwazao
Wawapi wajigambao, tungambiyane vigambo?

Iwapo mu wana nyimbo, na ungoi upasao
Musingewaonya mambo, waoga mwatishao
Mungefungata masombo, kuteta na wawezao
Wawapi wajigambao, tugambiayane vigambo ?

Wawapi fundi wa nyinbo, malenga wajitwazao
Wasemao kulla jambo, kuwa walijua wao
Kuna kipambua pambo, chatafuta wapambao
Wawapi wajigambao, tugambiayane vigambo?

Musidhani ni msimbo, hayano nambano leo
Nawaeleza ni mambo, yamtaka atakao
Ajifungate msombo, mdudoateze nayo
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo ?

www.freekcsepastpapers.com

Imani wenya utambo, mutambao kwa matao
Muelewao mafumbo, na mbinu za wafumbao
Kuna 'tomvu za ulimbo, tengani muruke nao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Sasa tafunuwa wimbo, takasani masikio
Siimbi la mtu jambo, alojiweka kituo
Hili 'metunga no fumbo, n'nao niwatakao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Tamati enyi warembo, nasubiri matokeo
Hivi sasa sina jambo, ela naaga nendao
Ni mimi simba wa wimbo, marara ngurumao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

**Maswali**

**a)** Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 1)
b) Eleza muundo wa shari hili. (alama 4)
c) Taja na utoe mifano ya mbinu **nne** za kimtindo zilizotumika katika shairi hili (alama 4)
d) Fafanua uhuru wa kishairi katika ubeti wa **nne**. (alama 3)
e) Andika ubeti wa **pili** katika lugha ya nathari. (alama 4)
f) Tambua nafsinenewa katika shairi hili. (alama 1)
g) Taja toni la shairi hili. (alama 1)
h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama lilivyotumiwa katika ushairi. (alama 2)
i) wafungatao masombo
ii) ninyemele

**SEHEMU B: RIWAYA**

*A. Matei: Chozi la Heri*

*Jibu swali la 2 au la 3*

2. Watu wengi huko mashambani hutegemea mashamba, mvua haijakubali kunyesha kwa muda. Wengi wa wanaofanya kazi za ajira, hufanya kazi za kijungu jiko.

(a) Bainisha muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Bainisha mbinu **nne** za kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)
(c) Eleza nafasi ya msemaji katika kuendeleza maudhui riwayani. (alama 12)

Au

3. "………. Tulikuwa wenye haja, maiti hasa, na tangu hapo maiti hachagui Sanda wala jeneza….. lakini Lo! Wanasema wajuao kuwa msitu ni mpya, ila nyani ni wale wale"

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. ( alama 4)
b. Bainisha vipengele **vinne** vya kimtindo vilivyotumiwa katika dondoo hili ( alama 4)
c. Jadili mchango wa Wahafidhina katika kuivunja jamii yao. ( alama 12)

**SEHEMU C: TAMTHILIA**

Timothy M Arege: Bembea ya Maisha

*Jibu swali la 4 au la 5*

4. La! Kila mbegu ipandwayo haina budi kuzaa na izaapo mazao yake huvunwa. Mtu hutakasa sahani akijua itamfaa tena. <u>Kinacholelewa hakina budi kulea</u>

(a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
(b) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 3)
(c) Kauli iliyopigiwa mstari inaonyesha majukumu ya watoto kwa wazazi. Thibitisha kwa kuonyesha wazi alivyowajibika anayerejelewa na msemaji (alama 4)
(d) Fafanua umuhimu wa msemaji katika kujenga tamthilia ya *Bembea ya Maisha* (alama 4)
(e) Eleza sifa **tano** za msemewa . (alama 5)

www.freekcsepastpapers.com

Au

5. "Haidhuru. Umenirudisha nyuma kweli katika siku zile za ujana wangu. Asubuhi niko skuli majira ya alfajiri, kiboko mkononi. Anayekuja baada yangu hata kama hajachelewa alikuwa hana lake. Siku nzima kazi tu. Jioni darasani tena, kiboko mkononi. Siyo siku hizi. Huwezi tena kumnyoosha mtoto kwa kiboko. Vitabu navyo nilikuwa nikivifunga kwenye baiskeli kwenda kuvisahihisha wikendi."

a. Eleza umuhimu wa mbinu rejeshi ukirejelea makala haya. (alama 3)

b. Eleza hulka **tano** za msemaji wa maneno haya. (alama 5)

c. Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 4)

d. Eleza changamoto zinazokumba ndoa za kisasa kwa kurejelea tamthilia nzima. (alama 8)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE

**Jibu swali la 6 au la 7**

6. **Rachel Wangari :** ***Fadhila za Punda.***

"Rudi, nyumbani mwanamke wewe! Nitakuja jioni tuyamalize haya."

a) i. Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)

ii. Fafanua hulka ya msemaji wa kauli hii. (al. 4)

iii. Huku ukizingatia hadithi hii, jadili maudhui ya mabadiliko yanavyotjitokeza katika hadithi (alama 7)

b) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 5)

Alasiri ile, baada ya ibada mbili, mhubiri akawa hoi kwa mavune. Akatamani kufika nyumbani apumzike, kazi ya kuwalisha kondoo wa Mungu si kazi rahisi. Wamefika nusu safari, bintiye katulia kama maji mtungini. Akimtazama kipembe anamkumbusha marehemu mkewe. Miaka mitatu sasa na dhiki ya kuondokewa haijamwisha. Alihisi ukiwa, akatamani mwenziye. Sasa kazi kukilea kitoto chao, kibinti hiki kilichomlanda mamake kama shilingi kwa ya pili. Nyumba ilijaa kicheko alipokuwa hai mamake. Kama si bintiye ambaye ulimi wake hautulii, kihoro kingemvamia labda hata kumvuta kuelekea kaburini.

Au

7. **Winnie Nyaruri Ogenche; *Sabina.***

"Ninawaomba wazazi wenzangu muwape watoto wa kike elimu badala ya kuwaoza mapema. Hongera, mwanangu kwa kupata alama mia nne arubaini na saba."

(a) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza hadithi husika. (alama 5)

b) Tambua mbinu ya kimtindo iliyotumika katika dondoo hili. (alama 1)

c) Fafanua jinsi mbinu yenyewe ilivyotumika ili kufanikisha utunzi wa hadithi. (alama 6)

d) Fafanua changamoto zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi. (alama 8)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8. Niaje wazungu wanaweza kutunza vitu vikajaa kwenye friji. Yani nimeweka soda mbili tu kwenye friji lakini akili haitulii hadi nizinywe. Niko sebuleni nazunguka tu . Najaribu kuwaza vitu vingine lakini wapi akili inaniambia 'My friend, kunywa soda'

a) i) Bainisha kipera cha utungo (alama 1)

ii) Eleza maana ya kipera hiki. (alama 1)

b) Utanzu wa kipera hiki huweza kuchukua nafasi muhimu katika fasihi simulizi. Thibitisha kwa hoja zozote **sita**. . (alama 6)

c) Ufanisi wa uwasilishaji wa utanzu huu unategenea fanani. Tetea kauli hii. (alama 7)

d) Ni changamoto zipi zinaweza kumkabili mwanafasihi mtafiti nyanjani? ( alama5)

www.freekcsepastpapers.com

**IGAMBA NGOMBE**
**Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**INSHA**

**Maagizo**
a) *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima.***
b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
c) *Kila insha isipungue maneno **400.***
d) *Kila insha ni alama **20.***
e) *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

SWALI LA LAZIMA
1. Wewe ni kiranja mkuu shuleni mwenu. Andika memo ukiwaonya wanafunzi dhidi ya visa vya utovu wa nidhamu shuleni. (alama 20)
2. Ukiwa mhariri mkuu wa gazeti la Wosia. Andika tahariri kuhusu umuhimu wa mitandao ya kijamii nchini. (alama 20)
3. Tunga kisa kitakachoafiki maana ya methali ifuatayo.
   "Mpanda ngazi hushuka."
4. Tunga kisa kitakachoanza kwa maneno;
   Mwanzoni, mambo yalimwia magumu na majukumu mazito aliyopewa hadi alipokutana na ….

www.freekcsepastpapers.com

**IGAMBA NGOMBE**
**Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya**
**102/2**
**KISWAHILI (Lugha)**
**Karatasi ya 2**
**Muda: Saa 2½**

***Maagizo***
a) *Jibu maswali **yote**.*
b) *Maswali yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**1. UFAHAMU** **(ALAMA15)**
***Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata.***

''Makao ni hapa.'' Zawadi alisisitiza. ''Hapana haja ya kutafuta penginepo. ''Nataka tuishi pamoja sisi watatu.''

''Haiwezekani,'' nikajibu huku nasimama. Zawadi aliamka ghafla na kunishurutisha niketi. ''Eeh! Vipi tena.Keti tu. Watukimbia tumekukosea nini?''

''Hakuna kosa ni sera yangu ya maisha.'' Amina aliangua kicheko.akainuka na kumshika Zawadi begani. ''Dadangu Zawadi,''alimwambia. ''Wachoka bure huyu bwana hatetereki katu katika azimio lake. Hutaambua chochote hapa.''

''Hebu sikiza,'' Zawadi alisema kwa sauti ya kupembeja. ''Napenda tukae pamoja kama ndugu wa toka n`toke.''

Uchawi wa mwanamke ni ulimi wake.Na moyo wangu ulikuwa karibu kushawishika. Bali adabu ndiyo **hirizi iliyonihami** dhidi ya uchawi huo. ''Ni muhali kwangu,'' nilisema kwa mkataa. ''Kuishi katika nyumba moja na mtu wa jinsia tofauti asiye mahirimu kwangu wala mwenzi wangu wa ndoa.''Hilo lingalitokea tu iwapo hali isiyoweza kuepukika kama maradhi mabaya kunisibu.'' Zawadi machozi yalimpukutika pukuteee.

Lakini haramu ngapi zimekwisha halalishwa na kizazi hiki maluuni? Wanaadamu wamekaidi kila yenye manufaa kwao. Hauwapigi mshipa watendapo mambo yasiyo. Ndiposa yamkini ndoa hazidumu, magonjwa hatari husambazwa na mabinti tumbi nzima kuringwa.

Nilipitia kwa Abdul Mohamed .Akanionea imani sana. Nilikuwa na mavune na mbano za kizunguzungu. Likizo yangu ya majuma mawili aliyokuwa amenipa ilikuwa imekwisha. Akanikiza kwa

majuma mengine mawili .Sikumdokezea kuwa nilitaka kutafuta kazi kwa rafiki yangu Joel Papa.Niliona bora kumwambia wakati niwapo na hakika kuwa kazi yenyewe nimepata.

Nilipita katika barabara za mji wa Mombasa nikiwa hoi.Nilihisi kitefutefu.Nilikuwa taabani mbele kukawa hakwendeki na nyuma hakurudiki.Nikalala kingalingali chini, maumivu yalinisama kifuani na mgongoni.Kichwa kikaniwanga.

Nilikuwa kwa hali hii niliposikia rukwama lasimamishwa karibu nami.Nilipoinua kichwa nilimwona ghulamu mmoja amesimama tisti, mkono mmoja kaushika nyongani na mwingine kwenye rukwama.Aliponena nikamtambua. Alikuwa Jeremiah Kipruto hamali mwenzangu.Akanipandisha kwenye rukwama na kunirudisha Kisauni.

Amina na Zawadi walikuwa karibu kupasuka kwa furaha ya kuniona kutwa hiyo.Zawadi alinivaa mzimamzima na kunipiga pambaja. Hawakugundua mara moja dhiki niliokuwa nayo. Niliketi kitini uchungu wanidhurubu kweli kweli. Nilipojaribu kunena nikashindwa .Yaliyotokea sina mwao nayo. Nilipata fahamu nikiwa hospitalini.Amina na Zawadi wakija kuniona na kunitakia shufaa. Daktari alikuwa akikagua wagonjwa pindi kwa pindi. Asubuhi moja alipokuwa katika ziara yake ya ukaguzi alitua karibu na kitanda changu.

''Bwana mdogo,'' alisema kwa sauti ya kite.

''Naam daktari,'' nikajibu.

''Leo wasikiaje?''

''Nasikia nafuu kidogo.''

''Unafanya kazi gani?''

''Nasukuma rukwama.''

''Eeh! Bwana kama wataka kuishi acha hiyo kazi ya sulubu.Ushasikia?'' ''Leo,'' aliniambia daktari ''N`takuruhusu kwenda nyumbani. Wapaswa kupumzika pasi kufanya lolote zito.''

Alasiri hiyo Amina na Zawadi wakajikalifu kunitunza na kuniuguza. Wakawa haswa kama baba na mama kwangu. Walinivua, wakanikosha na kunivisha kama kitoto. Walinilisha kama ndege anavyorai kinda lake kiotani. Nilipata nafuu nikakoma kabisa kutenda kazi za sulubu. Nikapania sasa kuchora baada ya kupangisha chumba changu.

Sikuwa na mtaji wowote wa kuanzia uchoraji. Zawadi na Amina wakanifadhilia fedha za kununulia rangi, brashi, karatasi na ala nyingine zilizohitajika. Michoro yangu ilikuwa ya kupendeza machoni. Amina na Zawadi walipendezwa mno na sura zao, wakatia fremu na kutundika ukutani ukumbini.

Ingawa swala la ndoa halikunikaa sawa sawa akilini mwangu,liliniandama kama kivuli.Nakumbuka ilikuwa desturi ya Zawadi kwenda maziarani alikozikwa mchumba wake,Rashid.Aliwahi kwenda huko na Amina mara nyingi .Suku moja alipita kwangu chumbani wakati wa jioni na mafungu ya mchanga mkononi.Akanisihi tuandamane pamoja. Tulipofika maziarani akayaweka mafungu hayo kwenye kaburi la Rashid na kunyamaza kwa kitambo.Zawadi alinishika mkono ghafla na kunielekeza pembeni, hapo tukaketi kitako.

''Zilikuwa zimesalia siku tatu tu,'' Zawadi alisema. ''Baada ya hizo siku tatu ningeolewa.'' ''Halafu Rashid akanitupa mkono. Sikutaka tena kuolewa tena na mwingine.''

www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI**

a) Eleza usasa uliopo katika hadithi hii (alama 2)
b) Taja madhara **mawili** ya usasa kwa mujibu wa kifungu (alama 2)
c) Eleza namna utabiri wa msimulizi uavyotimia (alama 1)
d) Kifungu hiki kinahimiza uwajibikaji.Thibitisha kwa hoja **tano.** (alama 5)
e) Taja mambo **matatu** yanayodhibitisha kuwa Zawadi anamtamani msisimulizi (alama 3)
f) Eleza maana ya msamiati ufuatao jinsi ulivyotumika kweye kifungu. (alama 2)
i) Uchugu wanidhurubu
ii) Hirizi iliyonihami

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Mirundiko ya taka pamoja na utaratibu usiofaa wa uzoaji wake ni tishio kubwa kwa siha ya umma pamoja na mazingira. Hii ni kwa kuwa taka huwa ni makaazi ya wadudu na wanyama waharibifu kama nzi, mbu, kombamwiko na panya ambao hueneza magonjwa na kuharibu vitu vyenye thamani. Maji taka nayo, pamoja na mifuko ya sandarusi, huwa na mastakimu ya wadudu na virusi vinavyoleta magonjwa mbalimbali.

Mifuko ya sandarusi ina madhara zaidi kwa kuwa huziba mitaro ya maji na kuzuia upitaji wa maji. Madhara hutokeza wakati wa mvua za gharika. Maji hukosa njia yake ya kawaida ambayo huwa imezibwa

na mifuko hii. Maji haya husababisha mafuriko ambayo huleta hasara ya mali na wakati mwingine ya uhai. Fauka ya hayo, mifuko hii huwasakama tumboni wanyama sio wa nyumbani tu, bali wa porini na majini.

Kwa sababu ya hatari zitokanazo na taka, pana haja ya kutafuta njia na teknolojia ya kuweza kukabiliana na tatizo hili ili kuyatunza mazingira na siha ya umma. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kuelimisha na kuhimiza umma kuwa na uangalifu katika matumizi ya bidhaa na raslimali ili kupunguza uzalishaji wa taka. Matumizi ya bidhaa kwa njia ya ubadhirifu huwa chanzo cha uzalishaji wa taka kwa wingi. Kwa mfano, maji ni raslimali ambayo imeendelea kutumiwa kwa ubadhirifu na hiyo huzalisha maji taka kwa wingi. Raslimali hii inaweza ikatumiwa kwa njia endelevu. Kwa mfano, badala ya kutumia bafu ya manyunyu kuogea, mtu anaweza kutumia maji ya karai. Watu wengi huchukulia taka kuwa kitu kisicho na manufaa yoyote. Hawajui kuwa kwa kutumia teknolojia endelezi, taka nyingi zinaweza zikageuzwa na kuwa na manufaa mengi. Vijana wadogo sehemu za mashambani wanahitaji pongezi kwa kuwa na utambuzi na mifuko ya sandarusi kutengenezea mipira wanayoitumia kuchezea. Hii ni teknoloji endelezi ambapo taka hugeuzwa na kuwa na manufaa.

Baadhi ya wananchi wenye ubunifu nao wameanzisha miradi ya kuzoa takataka kutoka majumbani mwa watu kwa ada kisha huzipeleka taka hizi kule zitakakobadilishwa ili ziwe bidhaa za plastiki kama matangi, mitungi, sapatu na champali. Taka hizi huwa malighafi ya kutengenezea bidhaa nyingine. Taka za chupa na chuma nazo huuzwa katika viwanda vinavyozigeuza kuwa na manufaa tena. Taka za karatasi hutumiwa kutengenezea bidhaa kama vitabu, katoni, shashi za chooni na magazeti.

Taka zinaweza pia kugeuzwa kuwa zenye faida kuzitumia kufanyia mboji. Ni muhimu kutambua kuwa si kila aina ya taka inaweza kutumiwa hapa. Taka zinazoweza kufanyiwa mboji ni zile ambazo huoza kwa haraka kama vile mabaki ya vyakula, mboga na matunda. Kwa sadfa, hizi ndizo taka zinazozalishwa zaidi siku hizi na hasa sehemu za mijini na katika maeneo ya biashara kama mikahawa na hospitali. Mtu akiwa na nafasi anaweza kuchimba shimo ambalo atafukia taka hizi ili kutengeneza mbolea. Hii ni njia isiyodhuru mazingira na yenye manufaa kemkem. Kwanza, hugeuza taka ambayo inaweza kuwahatari na kuifanya iwe yenye manufaa kwa hivyo hutatua matatizo ya kiafya yanayoweza kutokana na mirundiko ya taka. Mchanga nao hufaidika kupata virutubishi. Mbolea kama hii inaweza ikatumika kukuzia mboga au maua katika bustani.

Maji taka, hasa yanayotumika kuoshea vyombo, nayo yanaweza kutumika kunyunyizia mashamba madogo ya mboga au bustani za maua. Maji taka haya yanahitaji kutayarishiwa njia mahususi ya kuyaelekeza katika mashamba haya baada ya kutumiwa. Aghalabu watu wengi wana mazoea ya kuchoma taka. Ni kawaida kupata matanuri ya kuchomea taka katika baadhi ya mitaa, shule na hospitali. Badala ya kupoteza moto huu bure bilashi, inawezekana pakawekwa baridi kubwa au tangi la chuma ambalo litatumia moto huo kuchemsha maji. Maji haya yanaweza yakatumiwa katika shughuli za nyumbani.

Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kuwa kuna baadhi ya taka ambazo ni hatari na huenda zisigeuzwe ili kutumika kwa njia yenye faida. Taka hizi ni kama vile mikebe au vifaa vingine vyenye kubeba sumu au dawa hatari. Ni bora kuvitupa vifaa hivi katika mashimo marefu au vyoo vya mashimo. Kwa vyovyote vile, si jambo muhali kwa watu popote wanapoishi kulinda siha yao pamoja na kutunza mazingira.

www.freekcsepastpapers.com

**<u>Maswali</u>**

a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa, fupisha aya za kwanza tatu kwa maneno 70 (alama 6, ut 1)
**Matayarisho / Jibu**

b) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 80, eleza manufaa ya taka kwa waja. (alama 9, ut 1)
**Matayarisho / Jibu**

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Andika maneno yenye miundo yafuatayo
i) Nazali ya kaakaa laini, irabu ya chini kati, kipasuo hafifu cha ufizi,irabu ya kati chini (alama 1)
ii) Kimadende, irabu ya chini kati, irabu ya nyuma juu, kipasuo hafifu cha kaakaa laini, irabu ya chini kati. (alama 1)
b) Ainishisha silabi katika neno **Amle** (alama 1)
c) Eleza maana ya ngeli (alama 1)
d) Tumia mifano **mitatu** kudhihirisha dhima tatu za viambishi tamati mbali na kiishio (alama 3)
e) Onyesha matumizi **mawili** tofauti ya 'kibainishi' (alama 2)
f) Badilisha sentensi katika wakati ujao hali ya masharti (alama 2)
Watoto watabarikiwa wasipowatelekeza wavyele wao uzeeni.
g) Geuza katika wingi: Mwanafunzi alileta unyoya shuleni. (alama 2)
h) Iandike sentesi ifuatayo upya ukibadilisha kivumishi cha sifa kiwe cha jina. (alama 1)

*i.)* Mwekahazina mrembo amewasili jijini.

*ii.)* Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hii: (alama 3)
<u>Huyu</u> alitembea <u>hadi</u> Kisumu <u>kisha</u> akapumzika

i) Tambua yambwa katika sentensi hii; Alipikiwa chai tamu sana (alama 2)

j) Tunga sentesi moja yenye kishazi tegemezi kinachofanya kazi ya kueleza (alama 2)

k) Tambua virai vinne katika sentesi ifuatayo (alama 2)
Wanamuziki hodari walikongamana mbele ya darasa asubuhi.

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa mstari (alama 2)
Mchezaji atakeyetuzwa ni yule mgeni.

m) Kwa kutolea mifano eleza majukumu **mawili** ya kiambishi '**e**' (alama 2)

n) i.) Paka alikunywa maziwa yote (anza kwa: maziwa …..) (alama 1)
ii) Tunga sentesi inayoonyesha hali ya vitu viwili kuwa pamoja kwa muda mrefu. (alama 1)

o) Andika upya sentensi ifuatayo ukizingatia maagizo kwenye mabano (alama 2)
<u>Kushauriana</u> kwao ndiko kuliwezesha <u>kuelewana</u> kwingi (tumia nomino nyingine yenye mzizi sawa na kila nomino iliyopigiwa mstari)

p) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo; (alama 2)
Baba alichoma mkuki ardhini na kuondoka

q) Mkuu wa kikosi alisema kwamba angezuru mtaa wa mabanda wa Sokomoko juma ambalo lingefuata (andika katika usemi halisi) (alama 2)

r) Tunga sentensi moja kutumia neno 'buibui' kudhihirisha maana mbili (alama 2)

s) Hasha ni kwa jambo, ……. ni kwa kujutia na …………………….. kwa kutaka nafasi . (alama 2)

t) Mwajuma ni mkaidi. Wazazi wake watamwonya kwa kutumia methali ipi? (alama 1)

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

a) Wewe ni mgeni, umealikwa kutoa hotuba kwa umma kuhusu uchumi. Eleza sifa za lugha utakayotumia kuafikia azma yako. (alama 5)

b) Jadili sababu **tano** zinaziwafanya watu kufanya makosa katika matumizi ya lugha (alama 5)

---

**<u>IGAMBA NGOMBE</u>**
**<u>Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya</u>**
**<u>102/3</u>**
**<u>KISWAHILI</u>**
**Karatasi ya 3**

**<u>Maagizo</u>**

*c) Jibu maswali **manne** pekee.*
*d) Swali la kwanza ni la **lazima**.*
*e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*
*f) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

**SEHEMU A: USHAIRI.**

1. **Lazima**
***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Haihitaji makini, kwa mwenye macho mazima
Utaona walakini, mradi ukitazama
Wanazini hadharani, wana kwa watu wazima
Yafanana na sodoma, miji yetu kwa yakini

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wanazini hadharani, wana kwa watu wazima
Wanatafuna maini, vijana na kina mama,
Hawana haya nyusoni, wameharamisha wema,
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini

www.freekcsepastpapers.com

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Hawana haya nyusoni, wameharamisha wema
Baba na binti ndani, wanacheza lelemama
Marijali wa mbioni, kujipagaza umama
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Marijali wa mbioni, kujipagaza umama
Wameikataa dini, toka tumboni mwa mama
Wadai Wataliani, watajirisha mapema
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wadai Wataliani, watajirisha mapema
Hivyo mambo ya kigeni, yametunukiwa dhima
Uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama,
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama
Watu hawana Imani, umezidi uhasama,
Na viongozi wa dini, kuabudu darahima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Na viongozi wa dini, kuabudu darahima
Wamekeuka yamini, kati yao na Rahima
Wamemuasi Manani, na kusahau kiyama
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wamemuasi manani, na kusahau kiyama,
Ya Illahi tuauni, tuwe watu maamuma
Tukue katika dini, siku zetu za uzima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini

***Maswali***

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)
b) Bainisha bahari ya shairi hili ukijikita katika ruwaza zifuatazo. (alama 3)
   i. Mishororo  ii. Maneno  iii. vina
c) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 5)
d) Bainisha aina tatu za taswira kama zinavyojitokeza kwenye shairi. (alama 3)
e) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
f) Bainisha nafsinenewa katika shairi hili. (alama 2)
g) Andika ubeti wa **tatu** kwa lugha nathari. (alama 4)

**SEHEMU B: RIWAYA**

**A. Matei:** *Chozi la Heri.*

*Jibu swali la 2 au la 3*

2. "Alikuwa wapi siku kiduka changu ambacho mimi na aila yangu tumekitegemea kwa miaka kumi kilipoporwa na kugeuzwa majivu?"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   Tathmini umuhimu **nne** wa msemaji katika kuijenga riwaya hii. (alama 4)
b) Jadili umuhimu wa mandhari katika kujenga riwaya ya *Chozi la Heri* kwa kurejelea Msitu wa Mamba. (alama 12)

3. (i) "Nina wazazi wawili, ila hawa ni wazazi tu, hawajadiriki kuwa walezi wangu, wala jina 'mlezi' haliwaafiki."Onyesha jinsi kauli iliyopigwa mstari inavyowaafiki baadhi ya wazazi katika Jumuiya ya Wahafidhina ukirejelea riwaya *Chozi la Heri.* (alama 12)

www.freekcsepastpapers.com

(ii) "Tumeendelea kuwakweza akina dada huku tukididimiza nguzo ya jamii yetu."
Kwa hoja **nane,** onyesha jinsi ambavyo nguzo ya jamii inadidimizwa kwa mujibu wa riwaya *Chozi la Heri.* (alama 8)

**SEHEMU C: TAMTHILIA**
**Bembea ya maisha; Timothy Arega**
*Jibu swali la 4 au la 5*

4. Mwandishi wa tamthilia hii ameshughulia sanasuala la Mabadiliko katika jamii. Fafanua. (alama 20)
5. "… anachukua vindonge vyake na kuvimeza kabla ya kuketi kwenye kochi mpya."

a) We dondoo hili katika muktadha wake.(alama4)
b) Tambua aina ya taswira kwenye dondoo hili. (alama 2)
c) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hii. (alama14)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**
FADHILA ZA PUNDA.

6. Jadili ufaafu wa anwani Fadhira za punda. (Alama 20)

KIFO CHA SULUHU -

**7.** ... iwapo penzi hili litatia doa, basi nirudishie mfuko huu kama ishara ya kulitupa penzi langu kama jongoo na mti wake..."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
c) Fafanua mbinu mbili ambazo zimetumika katika dondoo hili. (alama 4)
d) Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)
d) Eleza umuhimu wa msemewa wa hadithi hii katika kujenga ploti. (alama 6)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

*4.* ***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Ewe Mainga wa Ndumi
Siwe uloambia akina mama
Siku tulopiga foleni
Chakula cha msaada kupata
Turudishe vifaranga kwenye miji
Wageuke vijusi tena
Njaa isiwaangamize?
Siwe ulopita
Matusi ukitema
Chumvi na sukari kuturushia ja samadi?
Uhitaji wetu ukatutuma
Kuokota vihela ulotuurushia
Ukatununua,kura ukapata?
Sasa miaka mitano imetimia
Waja tulaghai tena
Mainga wa Ndumi huna lolote safari hii
Ubunge umekudondoka ukitazama

***Maswali***

a) Huu ni wimbo wa aina gani? (alama 2)
b) Taja shughuli **mojamoja** ya kijamii na kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utungo huu. (alama 2 )
c) Wewe ni mwasilishaji wa kipera hiki jukwani, eleza mambo **sita** ambayo utazingatia katika uwasilishaji wako. (alama 6)
d) Jadili jinsi jamii ya kisasa inavyojaribu kuendeleza fasihi simulizi. (alama 5)
e) Maandishi ni mojawepo ya vifaa vya kukusanya na kuhifadhi fasihi simulizi. Tathmini udhaifu wa kutumia kifaa hiki. (alama 5)

www.freekcsepastpapers.com

r) Tunga mfano mmoja wa sentensi kuzingatia muundo ufuatao (alama2)
S - (RH + RH + t + N + V )

s) Neema amekuwa kiduchu toka utotoni lakini mwenye akili nyingi akitazama unaona kama anayezisoma a akili zako (tumia methali mwafaka kuafiki maelezo hayo) (alama1)

t) Jaza pengo (alama2)

i) Mtu ni kwa mja, ukongo ni kwa ...................................... na kiate ni kwa ...................................

ii) Tunapotaka kuomba radhi kabla ya kutamka jambo ambalo linaweza kumuudhi mtu tunasema .......................... ilhali tunapotamka kuonyesha mshtuko au jambo la hatari tunasema .........................

**4. <u>ISIMU JAMII</u> (alama10)**

Jambo Kenya! Nachukua fursa hii kumkaribisha mheshimiwa Profesa Chan kutoka jamhuri ya watu wa Uchina. Kufikia hapo kila kitu ki barabara tunapoendelea kujadiliana kuhusu swala hili la mabadiliko ya hali ya anga ulimwenguni. Suala hili linaendelea kupunguza idadi ya watu duniani. Nawaomba tusimame kuwaheshimu walioondoka.
(anawaashiria wasimame)
Asanteni sana!

a. (i) Tambua sajili hii (alama1)
ii) Eleza sifa za sajili uliotaja hapo juu ukizingatia kifungu (alama4)

b) Order! Lazima kutii mpangilio! Katili hauruhusiwi kuongea bila ruhusa. Polisi, mpelekeni nje.
i) Tambua sajili hii (alama1)
ii) Fafanua sifa zozote nne ambazo zingejitokeza iwapo mazungumzo yangeendelea (alama4)

---

**<u>MTIHANI WA CEKENAS (2)</u>**

*<u>Hati ya kuhitimu Elimu ya Sekondari Nchini Kenya</u>*

**<u>102/3</u>**

**<u>KISWAHILI</u>**

**<u>KARATASI YA TATU</u>**

**<u>(FASIHI)</u>**

**<u>MUDA: SAA 2½</u>**

**<u>MAAGIZO</u>**

- *Jibu maswali <u>manne</u> pekee*
- *Swali la <u>kwanza</u> ni la <u>lazima</u>*
- *Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobakia yaani : Riwaya, hadithi fupi,ushairi na fasihi simulizi*
- *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*
- *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**SEHEMU A: TAMTHILIA**

**Timothy M.Arege :Bembea ya Maisha**

1. **LAZIMA**

La! Kila mbegu ipandwayo haina budi kuzaa na izaapo mazao yake huvunwa. Mtu hutakasa sahani akijua itamfaa tena<u>. Kinacholelewa hakina budi kulea.</u>

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)

b) Changanua mtindo katika dondoo hili (alama3)

c) Kauli iliyopigiwa mstari inaonyesha majukumu ya watoto kwa wazazi. Thibitisha kwa kuonyesha wazi alivyowajibika anayerejelewa na msemaji (alama4)

d) Fafanua umuhimu wa msemaji katika kujenga tamthilia ya Bembea ya Maisha (alama4)

e) Eleza sifa tano za msemewa (alama5)

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU B: RIWAYA**

**A. Matei: Chozi la Heri**

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. "Vipi, binadamu anavyoweza kuyazoa maji yaliyomwagika?"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)

b) Tambua mbinu ya lugha iliyotumika (alama2)

c) Jadili sifa tatu za msemaji (alama3)

d) Hakiki jinsi binadamu alivyomwagikiwa na maji katika riwaya (alama1)

3. "Nilipojaribu kuukata mkono niliostahili kuubusu yalinifika ya kunifika.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)

b) Fafanua mambo mbalimbali yaliyomfika anayesema maneno katika dondoo hili (alama4)

c) Kwa kurejelea hoja kumi na mbili kutoka kwenye riwaya, onyesha jinsi udhaifu wa uongozi umebainika katika Jumuiya ya Chozi la Heri (alama12)

**SEHEMU C: HADITHI FUPI**

**MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE**

**Jibu swali la 4 au la 5**

4. Racheal Wangare: Fadhili za Punda

"Rudi, nyumbani mwanamke wewe! Nitakuja jioni tuyamalize haya."

a) i) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)

ii) Fafanua hulka ya msemaji wa kauli hii (alama4)

iii) Huku ukizingatia hadithi hii, jadili maudhui ya mabadiliko yanavyojitokeza katika hadithi. (alama7)

b) Changanua mtindo katika dondoo hili (alama 5)

Alasiri ile, baada ya ibada mbili, mhubiri akawa hoi kwa mavune. Akatamani kufika nyumbani apumzike, kazi ya kuwalisha kondoo wa Mungu si kazi rahisi. Wamefika nusu safari, bintiye katulia kama maji ya mtungi. Akimtazama kipembe anamkumbusha marehemu mkewe. Miaka mitatu sasa na dhiki ya kuondokewa haijamwisha. Alihisi ukiwa, akatamani mwenziye. Sasa kazi kukilea kitoto chao, kibinti hiiki kilicho mlanda mamake kama shilingi kwa ya pili. Nyuma ilijaa kicheko alipokua hai mamake. Kama si bintiye ambaye ulimi wake hautulii, kiroho kingemvamia labda hata kumvuta kuelekea kaburini .

AU

5. Winnie Nyaruri Ogenche; Sabina

"Ninaomba wazazi wenzangu muwape watoto wa kike elimu badala ya kuwaoza mapema. Hongera, mwanangu kwa kupata alama mia nne arubaini na saba"

a) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza hadithi husika (alama5)

b) Tambua mbinu ya kimtindo iliyotumika katika dondoo hili (alama1)

c) Fafanua jinsi mbinu yenyewe ilivyotumika ili kufanikisha utunzi wa hadithi (alama6)

d) Fafanua changamoto zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi (alama8)

**SEHEMU D :USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au la 7**

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Nazuka mtunga mambo, na watunzi watungao
**Wafungatao masombo,** kushika msu na ngao
Naipiga ya ngambo, sauti ifike kwao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Ni siku nyingi kitambo, **ninyemele** naja leo
Kama kweli wana nyimbo, nawaje niimbe nao
Na sababu ni vigambo, vya wale wajitwazao
Wawapi wajigambao,tugambiyane vigambo?

www.freekcsepastpapers.com

Iwapo mu wana nyimbo, na ungoi upasao
Musingewaonya mambo, waoga mwatishao
Mungefungata masombo, kuteta na wawezao
Wawapi wajigamboa, tugambiayane vigambo?

Wawapi fundi wa nyimbo, malengo wajitwazao
Wasemao kula jambo, kuwa walijua wao
Kuna kipambua pambo, chatafuta wapambao
Wawapi wajigambao,tugambiyane vigambo?

Musidhani ni msimbo, hayano nambano leo
Nawaeleza ni mambo, yamtaka atakao
Ajifungate msombo,mdudoateze nayo
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Imani wenya utambo, mutambao kwa matao
Muelewao mafumbo, na mbinu za wafumbao
Kuna 'tomvu za ulimbo, tengani muruke nao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Sasa tafunuwa wimbo, takasani masikio
Siimbi la mtu jambo, alojiweka kituo
Hili' metunga no fumbo, n' nao niwatakao
Wawapi wajigambao, tugambiyane vigambo?

Tamati enyi warembo, nasubiri matokeo
Hivi sasa sina jambo, ela naaga nendao
Ni mimi simba wa wimbo,marara ningurumao
Wawapi wajingambao, tugambiyane vigambo?

**Maswali**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama1)
b) Eleza muundo wa shairi hili (alama4)
c) Taja na utoe mifano ya mbinu nne za kimtindo zilizotumika katika shairi hili (alama4)
d) Fafanua uhuru wa kishairi katika ubeti wa nne (alama3)
e) Andika ubeti wa pili katika lugha ya nathari (alama4)
f) Tambua nafsi nenewa katika shairi hili (alama1)
g) Taja toni la shairi hili (alama1)
h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika ushairi (alama2)
    i) Wafungatao masombo
    ii) Ninyemele

7. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakazifuata nyago,
Hadi kwenye wako ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

www.freekcsepastpapers.com

Pindi kinunua kitu, hafurahi Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanuna mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake 'Subutu' Kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani,ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliyejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sadawi, aibatili rohoyo,
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza kuvunja kaninyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Ninacho changu kilio, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa matatizo kuambiwa,
Ama nitumie mbio, fuadini ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

**Maswali:**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama1)

b) Fafanua mambo **manne** mabayo nafsineni analalamikia (alama4)

c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: (alama3)
 (i) Idadi ya vipande katika kila mshororo
 (ii) Mpangilio wa vina katika kila ubeti
 (iii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti

d) Andika ubeti wa **nne** katika lugha nathari (alama3)

e) Bainisha tamathali **mbili** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili (alama2)

f) Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu **mbili** alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi (alama2)

g) Andika aina **mbili** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili (alama2)

h) Fafanua muundo wa ubeti wa **tano** na **sita** (alama3)

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI**

8. Niaje wazungu wanaweza kutunza vitu vikajaa kwenye friji. Yani nimeweka soda mbili tu kweye friji lakini akili haitulii hadi nizinywe. Niko sebuleni nazunguka tu. Najaribu kuwaza vitu vingine lakini wapi akili inaniambia 'My friend, kunywa soda.'

a) Bainisha kipera cha utungo huu (alama1)

b) Fafanua aina tatu za taswira zilizotumika katika kifungu hiki (alama3)

c) Utanzu wa kipera hiki huweza kuchukua nafasi muhimu katika fasihi simulizi. Thibitisha kwa hoja zozote sita (alama6)

d) Ufanisi wa uwasilishaji wa utanzu huu unategemea fanani. Teteta kauli hii. (alama5)

e) Ni changamoto zipi zinaweza kumkabili mwanafasihi mtafiti nyanjani? (alama5)

**MURANG'A SOUTH**
**102/1**
**KISWAHILI**
**INSHA**
**KARATASI YA 1**
**MUDA: 1$^3/_4$**

**Maagizo**

a. *Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima.***
b. *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
c. *Kila insha isipungue maneno 400.*
d. *Kila insha ina alama 20.*
e. *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

1. Kumekuwa na tatizo sugu la uharibufu wa mazingira nchini.
Wewe ndiye mhariri mkuu wa gazeti la Tushauriane. Andika tahariri kuhusu aina za uharibifu wa mazingira na jinsi ya kusuluhisha janga hili.

2. Maendeleo ya kiteknolojia yana umuhimu na madhara. Jadili.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali:
Mchumia juani hulia kivulini.

4. Tunga kisa kitakochomalizika kwa maneno yafuatayo:
…Nilipopiga darubini nilianza kujuta. Maovu niliyomtendea mke wangu yalikuwa yameleta madhila tele. Tayari amepatwa na shinikizo la damu. Nilitamani nimtake radhi. Nilikata shauri kuchukua mkondo mwingine wa maisha.

---

**MURANG'A SOUTH**
**102/2**
**KISWAHILI LUGHA**
**KARTASI YA 2**
**Muda: Saa 2 ½**

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

Nchi ya Kenya inaibukia kuwa kitovu cha mitandao ambayo imekuwa ikijihusisha na ulanguzi wa wasichana wachanga kutoka wilaya ya Moroto, eneo la Karamoja, nchini Uganda. Naibu Kamishina wa Leba, Bonaya Kase, alisema kuwa watu hao wamekuwa wakitumia mipaka na kiwango cha juu cha umaskini cha jamii zinazoishi katika eneo hilo kuendesha biashara hiyo haramu.

"Wasichana wengi huwa wanasafirishwa hadi mtaa wa Eastleigh, jijini Nairobi, ambako huwa wanaajiriwa kama wajakazi. Ni huko ambako huwa wanafanyiwa ukatili wa kila aina ambapo baadaye wengi wao hupata mimba wakiwa bado wachanga," akasema. Akihutubu katika Kaunti ya Bungoma wakati wa maadhimisho ya *Siku ya Kitaifa Dhidi ya Kazi ya Lazima kwa Watoto*, Bwana Kase aliwaonya Wakenya dhidi ya kuwaajiri na kuwanyima watoto haki, uhuru na furaha yao ya utotoni.

Meneja wa Miradi katika Shirika la Kimataifa kuhusu Leba (ILO), Grace Banya, alisikitika kwamba wazazi wanatumia watoto kama wafanyakazi. Alisema kuwa wanashirikiana na wadau muhimu, wakiwemo polisi, Afisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ya Umma (ODPP), maafisa wa Idara ya Mahakama na wale wa idara ya uhamiaji kumaliza ulanguzi wa watoto nchini. "Kenya ni kitovu kinachotumika katika ulanguzi wa watoto ili kuwafanyisha kazi za lazima. Tunahatarisha nafasi ya nchi hii ikiwa hatutachukua hatua za dharura kukabili hali hiyo," akasema.

Hapa nchini, kaunti ya Bungoma inatajwa kuwa miongoni mwa zile zilizoadhiriwa zaidi na hali hiyo, kwani iliibuka kuwa jumla ya wanafunzi elfu kumi na tano, mia sita themanini waliacha shule. Naibu gavana wa kaunti hiyo Bi Jeniffer Mbatiany, alisema kuwa visa hivyo vinatokea kwa wingi katika maeneo ya mlima Elgon, Bumula, Tongaren, Kimilili na Chwele, kwani watoto wa kati ya umri wa miaka minane

www.freekcsepastpapers.com

na kumi na tano huwa wanaajiriwa kama vibarua katika mashamba ya miwa na viazi, kuchunga mifugo, kutafuta kuni kati ya kazi nyingine.

"Kwa upande mwingine, kuna ongozeko la visa vya watoto wanaoingizwa katika ukahaba katika barabara ya Bungoma hadi Malaba, katika eneo la Kanduyi, ambako madereva wa matrela huwa wanaegesha matrela yao nyakati za jioni," akasema. Bi Mbatiany alisema kuwa wanabuni Rasimu ya Sera ya Kuwalinda Watoto katika Kaunti ya Bungoma, ili kuwalinda watoto dhidi ya kutumiwa vibaya.Watoto wengi huwa wanaingizwa katika kazi wasizofaa kutokana na ukosefu wa taasisi maalum ya kuafuatilia maslahi yao. Ukosefu wa taasisi hiyo ndio unatajwa kuchangia ongezeko la visa hivyo.

Baraza la Kitaifa la Huduma za Watoto (NCCS) linakisia kuwa karibu Wakenya elfu kumi na saba na mia tano huwa wanasafirishwa kila mwaka kufanya kazi za ujakazi, kazi za lazima na ukahaba, ambapo nusu yao huwa watoto.

**Maswali**

a) Eleza jinsi dhuluma dhidi ya watoto inavyojitokeza katika kifungu ulichosoma. (alama 2)
b) Bainisha maudhui manne ambayo Bw Bonaya Kase anadokeza katika mazungumzo yake. (alama 4)
c) Tambua suluhisho kwa matatizo yanayowakumba watoto kwa mujibu wa kifungu. (alama 2)
d) Nchi inahatarishwa ikiwa hatua za dharura hazitachukuliwa kukabiliana na ulanguzi wa watoto. Taja washikadau wanaoweza kushirikishwa ili kumaliza tatizo hili. (alama 2)
e) Kipe kifungu hiki anwani mwafaka. (alama 1)
f) Eleza mchango wa wazazi katika kukiuka haki za watoto. (alama 2)
g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika kifungu. (alama 2)
i. kitovu
ii. ulanguzi

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

Kati ya mwaka wa 1888 hadi 1963 Kenya ilikuwa koloni ya Uingereza. Wakati huo nchi ilishuhudia mapambano ya muda mrefu ya uhuru huku watu wakipigana na wakoloni kuikomboa nchi yao. Wengi wa waliohusika katika vita hivyo walikuwa wanaume kwani wanawake walibaki nyuma kutunza nyumba, kulea watoto wao na kufanya kazi kwenye mashamba na masoko. Chini ya utawala wa kikoloni, wanawake walizidi kuchukuliwa kama wasio na umuhimu kwa mfumo wa kiuchumi na mamlaka na ushawishi wao ulififia haraka miongoni mwa umma.

Licha ya ushawishi wao kififia katika kipindi hiki, hata hivyo, baadhi ya wanawake walisimama kidete na kuchukua jukumu kubwa katika safari ya uhuru wa Kenya. Wao, ni miongoni mwa wananchi wengine waliotunga na kuimba nyimbo zilizokejeli serikali ya kikoloni na kuwatia moyo wapiganaji wa uhuru katika mapambano hayo.

Wengine walifanya kazi kama majasusi wa wapiganaji uhuru wa Mau Mau kwa kuwapa taarifa muhimu ambazo hatimaye ziliwasaidia kuwashinda wakoloni. Hawa ni baadhi ya wanawake ambao jukumu lao katika mapambano lilijitokeza dhahiri.

Mekatilili wa Menza alikuwa mpiganiaji uhuru wa kike wa Kenya ambaye aliwaongoza watu wa pwani wa jamii ya Wagiriama kupinga utawala wa kikoloni wa Uingereza mwanzo mwa karne ya ishirini. Wakati utawala huu ulipojaribu kulazimisha sera na sheria zao kwa Wagiriama, Mekatilili alisimama na kuwapinga kwa ujasiri. Aliamini katika mila za watu wake wala hakutaka kuziona zikichafuliwa au kukomeshwa na Waingereza. Baada ya kuwa mjane, aliongoza watu Wagiriama kuasi Waingereza ambao walitishia uhuru wao kupitia kazi za kulazimishwa na kutozwa ushuru. Uongozi wake ulichangia katika maasi mwaka wa 1913 hadi 1914 na licha ya kukamatwa mara nyingi na kufungwa gerezani alifaulu. Kilichofuatia ni uasi wa Wagiriama ambao ulisababisha Mekatilili kukamatwa. Alifungwa jela katika eneo la Mumias kwa miaka mitano. Waingereza hatimaye walilegeza udhibiti wa eneo hilo, na kukubali matakwa ya watu wa Menza wa jamii ya Giriama.

Muthoni Kirima alikuwa kiungo muhimu katika vita vya Mau Mau na alipigana na wanaume wakati wa mapambano ya uhuru. Yeye alikuwa mpiganaji wa ngazi ya juu wa kike aliyestaafu katika Jeshi la Ardhi na Uhuru la Kenya la Mau Mau katika miaka ya 1950. Wanawake wachache wa Mau Mau walikuwa wapiganaji wenye bidii, na Muthoni ndiye mwanamke wa pekee aliyepata cheo cha Mau Mau cha *field-marshal.* Akiwa na umri wa miaka ishirini pekee, Muthoni alijiunga na Mau Mau kama jasusi. Pia alisaidia kuwapa wapiganaji chakula na maji. Mwanzoni mwa Maasi ya Mau Mau (1952-1960), kwanza alifanya kazi kama jasusi, kabla ya kujiunga na wapiganaji msituni. Alipanda daraja haraka kutokana na talanta yake ya kuzaliwa kama mtaalamu wa kijeshi. Kwanza alipata cheo cha Jenerali kisha *Field Marshal.* Hakuwahi kutekwa wakati wa mapambano ya uhuru. Ilibidi akabiliane na hali mbaya ambayo ilikumba

www.freekcsepastpapers.com

Mau Mau waliokuwa wakiishi msituni ikiwa ni pamoja na hali mbya ya hewa, hatari ya wanyamapori bila kusahau kupambana na wakoloni.

Wambui Otieno alipewa jina la Virginia Wambui Waiyaki alipozaliwa. Akiwa na umri wa miaka kumi na sita, alitoroka nyumbani na kujiunga na Mau Mau jijini Nairobi wakati wa hali ya hatari kuwafanyia kazi ya upelelezi. Kutoroka nyumbani katika umri mdogo kuliashiria mwanzo wa maisha yake yote kama mwanaharakati na mpiganaji. Alikiuka mipaka ya utabaka na jinsia alipojiunga na vuguvugu hilo licha ya kwamba hakuwa mwajiriwa wa kawaida wa Mau Mau. Katika vuguvugu la Mau Mau, Wambui alihudumu kama wakala wa ujasusi kwa kupeleleza, kuwasiliana na kusaidia katika ununuzi wa silaha. Mnamo 1952, akiwa shule ya upili, Wambui alikula kiapo cha kutii kilichokuwa sehemu ya kanuni za Mau Mau.

Baada ya vikosi vya Mau Mau kushindwa, alijihusisha na shughuli za vyama vya wafanyakazi na kufanya kazi kwa karibu na Tom Mboya na wanaharakati wengine wa vyama vya wafanyakazi. Alikamatwa Julai 1960 kwa kuhamasisha wanawake kugoma na kufanya ghasia dhidi ya utawala wa Waingereza na alizuiliwa katika kambi ya Lamu hadi Januari 1961.

Mukami Kimathi alikuwa mke wa marehemu mpiganaji wa uhuru Field Marshal Dedan Kimathi. Mbali na kuwa mke wa mpiganaji uhuru maarufu pia alishiriki kikamilifu katika harakati za kupigania uhuru wa nchi. Mukami alikuwa miongoni mwa wapiganaji wa Mau Mau waliozuiliwa katika Gereza Kuu la Kamiti Maximum wakati wa harakati za kupigania uhuru. Mukami alikuwa mtu muhimu katika kupigania uhuru wa Kenya, akichangia uungaji mkono usioyumba kwa mumewe alipokuwa kiongozi wa waasi wa Mau Mau. Alivumilia magumu mengi, yakiwemo kufungwa jela na kuteswa lakini hakuyumba.

***Maswali***

a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 55. (alama 6, 1 mtiririko)

**Matayarisho /Nakala Safi**

b) Tambua mchango wa wanawake mahsusi katika mapambano ya ukombozi. (maneno 105-110). (alama 9, 1 mtiririko)

**Matayarisho / Nakala Safi**

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Andika **neno** lenye mpangilio wa sauti zifuatazo. (alama 1)
Kipasuo kwaruzo, irabu ya juu nyuma, kimadende, irabu ya kati chini.

b) Onyesha **matumizi ya -li-** katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Tunda lilipatikana sokoni.

c) **Ainisha vielezi** katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Wakulima hupalilia mimea, mara kwa mara shambani.

d) Andika miundo ya nomino katika ngeli ya U-ZI huku ukitoa mifano. (alama 2)

e) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo.

i. Baba aliyenunuliwa gari na bintiye amefurahi. (**Anza kwa kipozi**). (alama 2)

ii. Kipkeino alikimbia mbio mjini London. (Geuza **chagizo** cha mahali kuwa chagizo cha wakati).(alama 2)

iii. Mwalimu alituzwa vizuri. (Badilisha kielezi kilichopigiwa mstari kuwa kivumishi). (alama 2)

f) Tambua aina ya **vishazi** katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Ajaye shuleni ni mzazi wake.

g) Andika katika **udogo**. (alama 2)
Vitabu vilivyokuwa vimebebwa na mwanamke vimeuzwa.

h) Kwa kutoa mifano katika sentensi, onyesha matumizi mawili ya **mkwaju**. (alama 2)

i) Andika katika **usemi halisi.** (alama 3)
Mama alimuamrisha mtoto alale.

j) Tunga sentensi ukitumia mzizi **-ch-** katika kauli ya kutendea. (alama 1)

k) Tambua **hali** iliyotumika katika sentensi ifuatayo. (alama 1)
Kidege chapaa angani.

l) Ainisha **virai** katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Jumba hili limejengwa na fundi hodari mno.

m) **Changanua** sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mishale. (alama 4)
Wale walifika mapema lakini hawa wangu walichelewa.

n) Unda **nomino** kutokana na **kitenzi**: **tubu**. (alama 1)

o) **Kanusha** sentensi ifuatayo kwa wakati ujao hali timilifu. (alama 2)
Meza hiyo ilinunuliwa kwa ajili yake.

p) **Tunga** sentensi ukitumia **kuhusishi cha mtenda.** (alama 1)

www.freekcsepastpapers.com

q) Andika **kinyume** cha sentensi ifuatayo. (alama 2)
Mwizi alikimbia haraka aliposahau njia.

r) **Andika neno** lenye mofimu zifuatazo. (alama 3)
Kikanushi, ngeli, wakati kanushi uliopita, mzizi, kauli ya kutendeka, hali ya kutenda.

s) Amrisha katika nafsi ya tatu wingi. (alama 1)

t) Jepesi ni kwa rahisi, ukuta ni kwa _________ na rabsha ni kwa ___________ (alama 2)

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

*Soma makala yafuatayo halafu ujibu maswali.*

Napiga kura upande wa la, Bwana Spika, kwani kupitisha mswada huu jinsi ulivyo utakuwa mzigo kwa raia wazalendo wa nchi hii waliotuchagua.

***Maswali***

a) Bainisha sajili inayorejelewa na makala haya. (alama 1)

b) Fafanua sifa tano za matumizi ya lugha katika muktadha huu. (alama 5)

c) Jadili changamoto nne zinazokumba kuimarika kwa Kiswahili katika jamii ya sasa. (alama 4)

---

**MURANG'A SOUTH**
102/3
KISWAHILI (FASIHI)
Karatasi ya 3
Muda: Saa 2½

*Maagizo*

a) Jibu maswali **manne** pekee.
b) Swali la **kwanza** ni la lazima.
c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani Tamthilia, Riwaya, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.
d) Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.

**USHAIRI**

**1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki,
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakizifuata nyago,
Hadi kwenye wako ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Pindi kinunua kitu, hafurahi Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanuna mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake "Subutu!" kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Aliye na **taraghani,** taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Haina faida nyumbani, ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliyejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sodawi, aibatili rohoyo,
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza kuvunja kaniyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

www.freekcsepastpapers.com

Ninacho changu kilio, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa mazito kuambiwa,
Ama nitumue mbio, fuadini ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

a) Shairi hili ni la aina gani? (alama 1)
b) Eleza sababu za mtungaji kulalamika katika shairi hili. (alama 3)
c) Andika umbo la shairi hili. (alama 4)
d) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari. (alama 4)
e) Taja na utoe mifano ya aina mbili za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)
f) Toa mifano miwili tofauti ya uhuru wa kishairi katika shairi hili. (alama 2)
g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi.
i) zani
ii) taraghani (alama 2)

**TAMTHILIA: KIGOGO- PAULINE KEA**

*Jibu swali la 2 au la 3.*

2. a) "Mamangu wee! Sikuwa nimeyasoma haya! Eti asilimia zaidi ya sitini iko tayari kumpigia kura ikiwa atasimama?"
   i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   ii) Taja tamathali mbili za usemi zilizotumika katika donddo hili. (alama 2)
   iii) Eleza sifa za msemaji (alama 4)
   b) Eleza namna mbinu ya ishara ilivyotumiwa katika Tamthilia ya Kigogo. (alama 10)

3. Ukiukaji wa haki na uvunjaji wa sheria ni mambo yaliyokithiri katika jimbo la sagamoyo. Thibitisha. (alama 20)

**RIWAYA: CHOZI LA HERI-ASSUMPTA MATEI**

*Jibu swali la 4 au la 5.*

4. "Kama ningeusikiliza ushauri wa Tausi wangu labda ningeweza kuiokoa aila hii …"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Tambua mbinu ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
c) Eleza ni kwa nini msemaji hakuweza kuiokoa aila yake. (alama 2)
d) Eleza athari za ukosefu wa usalama katika nchi ya wahafidhina. (alama 12)

5. Fafanua namna mbinu zifuatazo zimetumika katika Riwaya ya Chozi la Heri. (alama 20)
i) Jazanda
ii) Sadfa

**HADITHI FUPI:**
**TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

6. "Kipi kipya kilichotokea? Matone mangapi ya machozi amekwishajirovya? Kitu gani kimebadilika?"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Andika vipengele viwili vya kimtindo vilivyo katika dondoo hili na uvitolee mifano. (alama 4)
c) Eleza uamuzi aliofikia msemaji baada ya mjadala huu. (alama 2)
d) Fafanua changamoto zinazoikabili jinsia ya kike katika hadithi hii. (alama 10)

**FASIHI SIMULIZI**

7 a) Maigizo ni nini? (alama 2)
   b) Taja sifa nne za maigizo. (alama 4)
   c) Eleza mambo manne anayopaswa kufanya mwigizaji ili kufanikisha uigizaji wake. (alama 4)
   d) Kushiriki ni mbinu moja ya kukusanya data katika utafiti wa kazi za fasihi simulizi.
   i) Eleza hoja tano kuhusu umuhimu wa mbinu ya kushiriki. (alama 5)
   ii) Eleza udhaifu wa mbinu ya kushiriki. (alama 5)

www.freekcsepastpapers.com

**MURANG'A SOUTH**
102/1
KISWAHILI
Karatasi ya 1
**INSHA**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. **Hii ni insha ya mahojiano .Vipengele muhimu vya insha ya aina hii viweze kujitokeza. Yafuatayo yazingatiwe**:

**a) Muundo**
Sura ya mahojiano idhihirike.

i. Kichwa au anwani
Kichwa kionyeshe wahusika na mada inayoshugulikiwa

ii. Utangulizi
Haya ni maelezo mafupi kwenye mabano ambayo hufafanua mazingira ambapo mahojiano yanaendelea. Huweza pia kutaja majina ya wahusika.

iii. Mwili
Sehemu hii hujumuisha ujumbe au maudhui yanayoshughulikiwa.
Huchukua mtindo wa kitamthilia.
Majina ya mhoji na mhojiwa huandikwa kushoto mwa pambizo yakifuatwa na koloni kisha kauli zao.
Maelezo ya ziada huandikwa kwenye mabano.

iv. Hitimisho
Huhitimishwa na mhoji kwa kutoa shukrani kwa mhojiwa.

**b) Maudhui**
Baadhi ya hoja ni :

i) Uhasama wa makabila tofautitofauti unakosesha amani.
ii) Ukosefu wa ajira unafanya watu wengine kuwa wahalifu.
iii) Tamaa ya kutajirika inawafanya wengine kuibiana.
iv) Tofauti za kitabaka.
v) Ufisadi. Wenye pesa huhongana na kufanya vitendo viovu.
vi) Idara ya mahakama kutotoa adhabu kali kwa wahalifu.
vii) Vijana kujiunga na makundi haramu.

Suluhisho

i) Watu kuelimishwa kuhusu uzuri wa kuishi kwa amani.
ii) Kupanuliwa kwa nafasi za ajira.
iii) Watu kuhimizwa kutosheka na kile Mungu amewajalia.
iv) Adhabu kali kutolewa kwa wahalifu.

**Tanbihi**
Mtahiniwa awe na hoja tano au zaidi ili aweze kujitosheleza kimaudhui.
Mtahiniwa akikosa muundo wa mahojiano aadhibiwe kwa kutolewa alama nne za sura (4s)

**2. Hii ni insha ya mjadala. Makala yaonyeshe faida na hasara za mitandao ya kijamii.**

Faida za mitandao ya kijamii:

i) Kuboresha mahusiano
ii) Kuboresha mawasiliano.
iii) Hutumika katika kutafuta kazi.
iv) Hutumika kupunguza misongo ya mawazo.
v) Huburudisha.

Hasara za mitandao.

i) Kutumia muda mwingi mtandaoni na kuwafanya watu kuwa wazembe.
ii) Wafanyikazi huiba muda wa wajiri wao.
iii) Kuathiri watu kimaadili.
iv) Kupenyezwa kwa utamaduni wa nje.
v) Kueneza umbeya.
vi) Wizi wa mawazo na fedha.

Mtahiniwa awe na hoja tano na zaidi ili kujitosheleza kimaudhui.

www.freekcsepastpapers.com

3. **Hii ni insha ya methali**
Kisa kidhihirishe maana ya methali.
Maana ya methali hii ni kuwa jambo linaloenda tenge linafaa kurekebishwa kabla halijaharibika kabisa. Mtu anafaa kufanya jambo mapema, baadaye haitawezekana.

4. **Hii ni insha ya mdokezo. Mtahiniwa anafaa atunge kisa kinachooana na mdokezo aliopewa**.
Msimulizi anaweza kutumia mbinu rejeshi na kusimulia kisa kuhusu jinsi mhusika alisaidiwa na familia yao.
Mtahiniwa akikosa kuandika mdokezo atakuwa amepungukiwa kimtindo.
Mtahiniwa akitunga kisa kisichooana na mdokezo atakuwa amepotoka kimaudhui.

---

**MURANG'A SOUTH**
102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

***1.* UFAHAMU (ALAMA 15)** ***MAJIBU***

a)
i) Huwa makaazi ya wanyama waharibifu waletao magonjwa
ii) Taka huziba mitaro ya maji na kuzuia maji kupita
iii) Madhara huwa ni mafuriko wakati wa mvua za gharika
iv) Mafuriko husababisha hasara ya mali
v) Vifo hutokea kupitia mafuriko/ kupoteza uhai
*vi)* Taka huwasakama tumboni wanyama wa nyumbani, porini na majini (alama 5)
**** sahihisha hoja tano za kwanza***

b)
i) Karatasi za sandarusi hutumiwa kutengeneza mpira
ii) Taka hutumika kama malighafi ya kutengeneza bidhaa zingine, kama vile, bidhaa za plastiki
iii) Taka za karatasi hutengeneza bidhaa kama katoni, vitabu, shashi na magazeti.
iv) Taka ya vyakula hutengeneza mboji au mbolea isiyohatarisha mazingira
v) Maji taka hasa ya kuoshea vyombo yanaweza kutumika kunyunyuzia mimea
*vi)* Moto wa kuchoma takataka waweza kutumika kuchemsha maji ya kutumiwa nyumbani
(alama 4) **** hoja zozote nne***

c)
i) Kuelimisha na kuhimiza umma kuwa na uangalifu katika matumizi ya bidhaa ili kupunguza uzalishaji wake.
ii) Kutumia teknojia endelezi au endelevu ili kugeuza taka kuwa ya manufaa.
(alama 2) *** hoja mbili za kwanza**

d)
i) Hutupwa katika mashimo marefu au vyoo vya mashimo. (alama 2)

e)
i) Maskakimu – Makaazi (alama 2)
ii) Muhali - muhimu

www.freekcsepastpapers.com

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

a)

i) Wanaume wapo hatarini ya kupatwa na kansa kuliko wanawake.

ii) Tofauti za kimaumbile husababisha hali hii.

iii) Wanaume hujihusisha na mitindo hatari na huwa na lishe duni.

iv) Wanawake wana homoni mbili za X zilizo na uwezo wa kuzuia saratani ikilinganishwa na wanaume ambao wana homoni moja ya X.

v) Kulingana na WHO, kuna aina nyingi za kansa zinazowahangaisha wanaume.

vi) Kansa ya koo na mapafu husababishwa na uvutaji sigara na ya ini ubugiaji wa pombe.

vii) Wizara ya afya Kenya inakadiria kuwa kansa ya tezi dume huua wanaume 1292 kila mwaka.

***viii)*** Asilimia 7 ya vifo vyote huchangiwa na kansa ***(alama7)(1 ut)***

b)

i) Wagonjwa wengi wa kansa huenda wakapata afueni.

ii) Hii ni baada ya jopokazi kupendekeza kupunguzwa kwa gharama ya matibabu ya kansa.

iii) Ripoti ilisema kuwa gharama ya matibabu ya kansa ni Ghali sana

iv) Nchi ina uhaba wa dawa na vifaa muhimu.

v) Gharama ya matibabu hutofautiana kulingana na kiwango cha saratani.

vi) Gharama ya tiba kemia na upasuaji hutofautiana.

vii) Matibabu ya saratani ya matiti na saratani ya mlango wa uzazi ni Ghali pia.

viii) Wanaougua kansa awamu ya tatu huwa hatarini. ***(alama 8)(1 ut)***

www.freekcsepastpapers.com

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) aibu ****kadiria jibu la mwanafunzi*** 1/0 (alama 1)

b) **Magari yale** yalipakwa rangi 1/0 (alama 1)

c) Nilichokipikia 2/0 (alama 2)

d) ni-kitenzi kishirikishi kipungufu
aliyekuwa – kitenzi kisaidizi
akizawadiwa – kitenzi kikuu 1x3 (alama 3)

e)

a) lika

b) pewa

c ) toa

d) fungama ½ x4 (alama 2)

f) sana – kielezi halisi
vizuri – kielezi cha hali
jana jioni – kielezi cha wakati zozote mbili1x2 (al 2)

g) Kile kimeraruka – kiwakilishi
Kitabu kile kimeraruka – kivumishi 1x2(alama 2)

h) Juma **na** Zainabu walinunuliwa viatu **na** baba. **kadiria jibu la mwanafunzi* 2/0 (ala 2)

i) **Kutangazwa** kwake kuwa mshindi kulimpa **furaha** na kuwapa wengi **mshangao**. (ala 3)

j) Viongozi wengi – kirai nomino (RN)
Walikuwa wakakamavu sana – kirai tenzi (RT)
Kabla ya uchaguzi – kirai husisi (RH) 1x3 (alama 3)

k) Baba na Martha wamepewa cheti na mwenyekiti wa kamati. (alama 4)

| S | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KN | | | KT | | | | | |
| N | U | N | T | N | H | N | H | N |
| Baba | na | Martha | walipewa | cheti | na | mwenyekiti | wa | kamati |

l) Kura- shamirisho kipozi
Wananchi- shamirisho kitondo
Ndege- shamirisho ala 1x3 (alama 3)

m) Jambazi sugu sana lilishikwa jana asubuhi. 2/0 (alama 2)

***n)*** Mnyama adhoofikaye ndiye atunzwaye vizuri**.** 1/0 (alama 1)

**** 'o' rejeshi iwe tamati kuleta dhana ya mazoea.***

o) a – nafsi ya tatu umoja
me – hali timilifu
ni – yambwa tendewa
w – mzizi
i – kauli ya kutendea
a – kiishio ½ x6 (alama 3)

p) **Walipachua** na **kufungua** mizigo **aliyopakua** juu ya lori. 1x3 (alama 3)

q) Wanafunzi **waliokuwa wametia bidii** walitunzwa zawadi. 2/0 (alama 2)

r) Finyo kwa chumvi
Suke, shuke,, chane, kipeto, shazi, kwa mtama. ½ x2 (alama 1)

**4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

*a)* Muktadha wa siasa – msamiati maalum umetumika, kwa mfano, *next general election.*

b) Istiara – mimi ni simba
Kuchanganya ndimi – Wangoje mpaka *next general election*.

c) Huwa ni lugha ya propaganda
Ni lugha ya ucheshi
Hutumia chuku
Lugha yenye ushawishi
Yaweza kuwa na majibizano
Ni yenye udanganyifu
Imejaa ahadi
Ina kudunisha
Yaweza kuwa na matusi/bezo
Ina majisifu/ majigambo
Ina kauli fupi fupi
****Mifano inaweza kutolewa kwa kifungu au nje ya kifungu, kadiria***

www.freekcsepastpapers.com

**KIGUMO - 2**

***Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)***

**102/1**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 1**

**INSHA**

**MUDA : SAA 1¾**

***Maagizo.***

***a)*** *Andika insha mbili: insha ya **kwanza** ni ya **lazima***

***b)*** *Kisha chagua insha nyingine **moja** kutoka kwa zile zilizobaki*

***c)*** *Insha yako isipungue maneno **400***

d) *Kila insha na alama* **20**.

e) *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**1. Lazima**

Kumekuwa na visa vingi vya utovu wa nidhamu shuleni mwenu. Ukiwa katibu wa viranja, andika kumbukumbu za mkutano uliojadili vyanzo vya utovu huo na suluhisho lake.

2. Baadhi ya wanafunzi shuleni mwenu wanatumia dawa za kulevya. Ukiwa kiongozi wa washauri marika, andika hotuba kuwaelezea madhara ya mazoea haya**.**

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti

4. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno yafuatayo:
… Nilijitolea mhanga na msaada wangu ukazaa natija kwa wengi.

---

**KIGUMO - 2**

***Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)***

**102/2**

**KISWAHILI**

**LUGHA**

**Maagizo**

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapojuu.

b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwahapo juu.

c) Jibu maswali **yote**.

d) Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki chamaswali.

e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**1. UFAHAMU: (Alama 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Mimi na Mwamba tulijiunga na shule ya upili ya Maarifa wakati mmoja.Tangu wakatihuo nimemtambua Mwamba kama rafiki wa kuaminika, Tulisoma pamoja, tukacheza pamoja na kushirikiana katika mambo mengi. Alikuwa mmakinifu, msikivu na mchangamfu. **Unadhifu** wake uliwavutia wengi. Hata mimi aliniathiri nikamuiga. Walimu na wanafunzi walimshabikia nakumthamini hata wakamchagua kuwa kiongozi. Vipawa vya Mwamba vilianza kuchipuka mapema.Naye Mwamba alijitahidi kuvipalilia.

Bidii ya Mwamba inaweza kumithilishwa na ile ya mchwa kujenga kichuguu kwa mate.Mwamba alifahamu fika kuwa mja yeyote kujaliwa ni yeye mwenyewe kujipa uvumilivu, kutia bidi na kushirikiana na wenzake. Alifanya juu chini kuelewa yote tuliyofundishwa na walimu wetu. Ingawaakili yake ilikuwa

www.freekcsepastpapers.com

kama sumaku, pale ambapo alitatizika kuelewa hakufa moyo. Alikuwa tayari wakatiwote kujadiliana na wenzake katika vikundi. Alitambua kuwa jifya moja haliinjiki chungu. Pamoja nahayo, Mwamba alijaliwa moyo wa kusaidia. Wakati mwingine katika kundi letu alitufafanulia madaambazo hatukuzielewa vizuri. Aliwafaa hata wale waliokuwa na changamoto ya kuelewa yaliyofunzwana walimu. Ama kwa hakika, tulishangazwa na subira na unyenyekevu wake.

Mimi na rafiki yangu Mwamba tulijiunga na timu ya soka ya shule yetu. Alichukua nafasi yamshambulizi nami nikawa mlinda lango. Kila tuliposhiriki kwenye mashindano, Mwamba aliifungiatimu yetu mabao mengi. Mara nyingi, tuliibuka washindi na kuwaacha wapinzani wetu vinywa wazi.Nyota ya Mwamba ilianza kung'aa michezoni. Alipokea tuzo ya mwanasoka bora zaidi katika gatuziletu. Nayo timu yetu ilinyakua kombe la ushindi na sare kamili za kandanda. Shule yetu ilisifika nakutambulika kama kitovu cha wachezaji kandanda chipukizi. Hata baadhi yetu tulichaguliwa kujiungana timu ya kitaifa ya vijana.

Mwaka huu, Mwamba amegundua kipawa chake kingine katika rubaa ya muziki baada yakujiunga na bendi ya muziki shuleni. Wakati wa gwaride na pia sherehe mbalimbali shuleni amewezakupata nafasi ya kututumbuiza. Sauti yake ya kinanda na nyimbo zake zimevuma kotekote. Kuvumakwa nyimbo hizo kunatokana na ujumbe wa nyimbo zake. Nyimbo hizo huwahimiza watu kukuzamaadili na bidii kila uchao. Hakika, zinatuliza mioyo, zinahimiza, zinachochea watu kuwa na upendo,amani na ushirikiano. Katika siku za hivi majuzi, bendi yao imetunga nyimbo ambazo zimevutiawafuasi wengi mitandaoni. Baadhi ya vituo vya mawasiliano vimetuma maombi kualika bendi hiyokwenye studio zao. Azma yao ni kurekodi baadhi ya nyimbo zao ili zitumike kama milio kwenye simu zinapopigwa au kukiriza. Aidha, nyimbo zao huchezwa kwenye vituo mbalimbali vya redio na runinga. Chini ya uongozi wa mwalimu wao, ambaye ni mlezi wa bendi yao, wameweza kujipatia hela ambazozimetumika kununulia vyombo zaidi vya muziki. Mwalimu huyu wao huhakikisha kuwa bendi hiyoina nidhamu ya hali ya juu.

Juma lililopita, mwalimu wa zamu aliwapa nafasi wanafunzi kadha kutoa nasaha kuhusunamna ya kufanikiwa masomoni. Mwamba alikuwa miongoni mwao. Hotuba yake ililenga ndipo.Alisema, "Wanafunzi wenzangu, kufaulu kwetu masomoni na pia maishani hakutegemei kuletulikotoka bali nidhamu ya mtu mwenyewe". Alituambia kuwa **achanikaye kwenye mpini hafi njaa**.Kwa hivyo, tujitahidi masomoni. Aliongezea kusema kuwa, kila mtu amejaliwa muda wa saa ishirini na nne kila siku. Alituhimiza tuuratibu muda wetu vyema. Katika kuhitimisha hotuba yake, alisisitizatuwaheshimu wakubwa wetu ili tuweze kufanikiwa maishani. Hotuba yake **hupigiwa debe** shuleni hadi leo.

a) Kwa kurejelea kifungu, fafanua manufaa **matano** ya kukipalilia kipawa. (Alama. 5)

b) Onyesha mambo **manne** yanayo onyesha umaarufu wa Mwamba. (Alama 4)

c) "Nyimbo zina majukumu tele katika jamii." Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea kifungu. (Alama 3)

d) Kauli "achanikaye kwenye mpini hafi njaa" imetumia tamathali gani ya usemi? (Alama 1)

e) Eleza maana ya:

i) **hupigiwa debe**, kwa mujibu wa kifungu.

ii) Andika kisawe cha **unadhifu,** kwa mujibu wa kifungu.

**2. UFUPISHO: (Alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Kuna aina mbili kuu za misitu. Ipo ile ya kiasili kama vile Msitu wa Karura na Msitu waMau. Hali kadhalika, ipo misitu ya kupandwa kama ile ya Kinale na Webuye. Misitu nihazina kubwa kwa jamii yoyote ile. Kila mwanajamii anapaswa kujivunia msitu.

Misitu husheheni miti ya aina nyingi ambayo pamoja na kuwa makazi ya wanyama,hutoa vyakula kama vile matunda na majani ambayo huwafaidi binadamu na viumbewengine. Bila misitu binadamu na wanyama wangeangamia.

Misitu ni kivutio cha watalii. Watalii kutoka ndani na nje ya nchi huzuru misitu nambuga mbalimbali za wanyama kuajabia uzuri wake. Watalii hawa hulipa fedha zakigeni ambazo hutumiwa kuanzishia miradi ya kiuchumi kama vile kustawishamiundomsingi.

www.freekcsepastpapers.com

Fauka ya hayo, misitu husafisha hewa na kurembesha mandhari wanamoishi binadamu.Rangi ya kijani kibichi na maua yenye rangi tofautitofauti huyafanya mazingirakupendeza hata yakitazamwa kwa mbali. Mandhari yasiyo na miti hayakosi urembo tu,bali huwa wazi kiasi kwamba hata mapaa ya majengo yaliyo hapo wakati mwinginehupeperushwa na upepo mkali.

Vipindi virefu vya jua huwanyima viumbe starehe na huweza kusababisha saratani yangozi kwa binadamu. Miti hufanya vivuli ambavyo huwakinga watu na wanyama dhidiya miale ya jua. Isitoshe, si ajabu kuwa mahali ambapo pana miti mingi kwa kawaidahupata mvua hata wakati usio wa majira ya mvua kwingineko.

Sekta ya tiba imefaidika si haba kutokana na miti. Matabibu wa kienyeji na hata wakisasa hutumia mizizi, majani na magome ya miti kutengenezea dawa. Miti kama vilemwarubaini hutibu magonjwa mengi. Hivi sasa magonjwa kama vile bolisukari,shinikizo la damu na ugonjwa wa figo yameweza kudhibitiwa kwa kutumia dawazinazotokana na miti. Inasemekana kuwa hata nyoka humtibu nyoka mwenzake kwamajani!

Miti hutumiwa viwandani kutengenezea bidhaa kama vile karatasi na samani. Viwandahivi hutoa ajira kwa maelfu ya raia, hivyo kupunguza makali ya uhaba wa nafasi za kazinchini.

Ni wazi kuwa uhifadhi wa misitu una manufaa tumbi nzima kwa binadamu. Hata hivyo, binadamu mwenyewe ndiye anayeiangamiza misitu yenyewe. Watu wenye mate ya fisiwamekata miti kiholela kwa ajili ya kupata kuni na kuchomea makaa ya kuuza. Lakusikitisha ni kwamba watu hawa hawadiriki kupanda miti mingine kufidia ilewaliyoikata. Wengine, kwa kutojua wanajipalia makaa, hupanda miti ambayo inakaushaVyanzo vya maji na kúchangia kuenea kwa kasi kwa jangwa. Hali kadhalika, wapowarina asali ambao katika juhudi zao za kurina husababisha kuteketea kwa misitu.

Kifungu cha katiba kinachohusu mazingira na mali ya asili kinasisitiza suala la uhifadhiwa mazingira. Kila mwanajamii basi ana jukumu la kuilinda misitu na kuepuka mazoeaambayo yanaiangamiza, la sivyo tutakuwa tunajichimbia kaburi.

a) Fupisha ujumbe wa aya **sita** za kwanza kwa maneno 85 (Alama 9, mtiririko ala 1)
**Matayarisho**
**Nakala safi**

b) Fafanua masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya **tatu** za mwisho.(Maneno50, Alama 6, 1 mtiririko)
**Matayarisho**
**Nakala safi**

**3. MATUMIZI YA LUGHA: (Alama 40)**

a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo: ( Alama 2)
(i) Kikwamizo ghuna cha kaakaa laini. ……………………………………
(ii) Kiyeyusho ghuna cha kaakaa gumu. ……………………………………
(iii) Irabu yanyuma wastani. ……………………………………
(iv) Kipasuo kwamizo sighuna cha kaakaa gumu …………………………………..

b) Bainisha dhamira/ jukumu ya kauli zifuatazo kwa kuzingatia kiimbo: ( Alama 2)
(i) Nisaidie na daftari lako. ………………………………………………………
(ii) Umemwona Rajabu leo? …………………………………………………….....

c) Andika maneno yenye miundo ifuatayo: ( Alama 2)
(i) Kiambishi nafsi, wakati uliopo, mzizi, kauli tendeshwa, kauli tenda/kiishio.
(ii) Kiambishi cha umoja, mzizi.

d) Nomino ifautayo, imo katika ngeli **mbili** tofauti ziandike: ( Alama 2)
ua
i) ……………………………………………………………………………………..
ii) ……………………………………………………………………………………..

www.freekcsepastpapers.com

e) Unganisha sentensi zifuatazo kuunda sentensi changamano. ( Alama 2)
Uhalifu ulidhibitiwa. Kulikuwa na doria za kutosha.

f) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali. ( Alama 3)
Lake lilipoporwa hatukujua.

g) Bainisha virai vilivyopigwa mstari katika sentensi ifuatayo: ( Alama 3)
Wanafunzi wengi walikuwa waadilifu mnokabla ya kuathiriwa na shinikizo za marika.

h) Ainisha kiima, kiarifu na chagizo katika: ( Alama 3)
Yeye mwenyewe alinipenda sana.

i) Andika upya katika hali ya udogo: ( Alama 2)
Nguo ambazo zinauzwa kwenye duka hili zinavutia.

j) Tunga sentensi iliyo muungano wa vishazi **viwili** huru. ( Alama 2)

k) Andika upya sentensi ifuatayo kulingana na maagizo. ( Alama 2)
Maria aliwachapa watoto wa Ali.
Anza kwa: Watoto wa Ali ……………………………………………………………………

l) Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali ya kuendelea. ( Alama 2)
Nyumba nyingi zinajengwa.

m) Andika maana **mbili** zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo. (Alama 2)
Maria alisema atafika kwao.

n) Andika upya sentensi ifuatayo katika usemi halisi. ( Alama 2)
Mtahini alisema kuwa kujibu maswali kwa usahihi kungewahakikishia matokeo bora katika mtihani huo wao.

o) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo. ( Alama 2)
Habiba alimnunulia mpenzi wake mkufu wa dhahabu.

p) Mkwaju hutumika kuleta maana ya **au** tunapoandika visawe. Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mengine **mawili** ya mkwaju/ mshazari. ( Alama 2)

q) Tumia kwa' katika sentensi kuleta dhana zifuatazo: ( Alama 2)
i) Pamoja na
ii) Sababu ya kutenda jambo

r) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya: ( Alama 2)
gari na ghali

s) Tunga sentensi **moja** ukitumia nomino ya makundi/jamii na uibainishe.(Alama 1)

**4. ISIMU JAMII: ( Alama 10)**

Unawahudumia wagonjwa katika kituo cha afya cha Sihabora. Fafanua sifa **kumi** za lugha ambayo utaitumia. (Alama 10)

www.freekcsepastpapers.com

**KIGUMO - 2**

***Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)***

**102/3**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA2½**

**SEHEMU YA A:USHAIRI**.

**1. Lazima**

*Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali*

Mwanadamu mambo yake, kueleweka muhali Ubavuni umuweke, umtowe kule mbali
Maskani ni afike, umtindie fahali
Utamu anufaike, sima badaa uwali
Hatimaye ateuke, kwa viliwa vya samli
Mwanadamu simuamini, afadhali nyamalumbwi.

Mwanadamu umjenge, awe mwenye kutajika
Mambo yake uyapange, ukawa wahangaika
Uwashe wake muwenge, uhakikishe wawaka
Nao mkono umuunge, vyake viwe vyaungika Dhorubani umkinge, asipate kudhurika
Mara atakusahau, wema wako kafukia.

Mwanadamu mpe cheo, kuwa akutumikie
Amani yako umpeo, fanaka uirajue
Kwake iwe kimbilio, wamini akukwamue
Mwisho takuwa kilio,shika sikio ujue
Ndio wake mwelekeo, yu aumaavuvie
Mwanadamu mgeuze, pande zote umtizame.

Mwanadamu mfadhili, kwa kila lililojema
Pasiwe hata dalili, ya kwake kukosa wema
Viteko siwe akali, kumbizo zikaterema
Binadamu takudhili, dhili zako kuzitema
Licha ya zote jamili, mwanadamu si muema
Mwanadamu ni mtu, lakini nusu mnyama

a) Onyesha **kinaya** cha mwanadamu anayezungumziwa (Alama 3)

b) Fafanua toni ya shairi hili (Alama 2)

c) Taja na ueleze bahari **tatu** za shairi hili (Alama 3)

d) Tambua aina **mbili** za urudiaji katika shairi hili (Alama 2)

e) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. (Alama 2)

f) Onyesha mbinu **nne** alizotumia malenga ili kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. (Alama 4)

g) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari ( Alama 4)

www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMUB : RIWAYA**

**Assumpta *Matei :*** *Chozi la Heri*

*Jibu swali la 2 au 3*

2. "Nitapigana kwa jino na ukucha kuulinda utu wangu, Nitatafuta haki ilikojificha."

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

b. Kwa kutolea mifano, tambua mbinu **mbili** za kimtindo zilizotumika katika dondoo (Alama4)

c. Elezau muhimu wamsemaji wa dondoo hili. (Alama4)

d. Eleza toni iliyotumika katika dondoo hili (Alama2)

e. Huku ukitumia hoja kumi na mbili. Fafanua jinsi haki za watoto zilivyokiukwa katika riwaya hii. (Alama 6)

3. Fafanua umuhimu wa matumizi ya barua katika kuendeleza maudhui riwayani. (alama 20)

**SEHEMU C: TAMTHILIA**

**TimothyArege:** *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 4 au 5*

4. "Dunia hii ya sasa tunaishi katika hofu. Tunahofu hata tusichokifahamu"

a. Eleza muktadha katika dondoo hili. (Alama 4)

b. Tambua **tamathali mbili** za usemi zilizotumika katika dondoo hili (Alama 2)

c. Fafanua sifa **nne** za msemaji wa maneno haya. (Alama 4)

d. Eleza jinsi hofu imejitokeza katika tamthilia. (Alama 10)

5 "…wakati mwingine mwindaji huwa mwindwa. Hata kijijini wanaishi watu. Watu hao hawakumbwinadhikikiasihiki. Ya nini kung'ang'ana kuyatafuta maisha kama kwamba hayapiti? Maisha ni mshumaa usomkesha! Ukijiachia sana peupe hata upepo unaweza kuuzima kabla ya kulika hadi nchani."

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)

b. Bainisha toni katika kifungu hiki (Alama 2)

c. Eleza vipengele **vine** vya kimtindo vinavyojitokeza (Alama 4)

d. Eleza umuhimu wamsemaji katika tamthilia hii. (Alama 10)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI-**

**D.W. Lutomia na P Muthama**: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 6 au 7*

**D.M. Oigo:** *Kifo cha Suluhu*

6. "Mumewangu, hebu zivute fikra zako miaka kumi na mitano iliyopita tulipoingia katika mkataba wa ndoa. Kwanini unataka kujitia hamnazo kuhusu ahadi ulizozitoa? Umesahau namna tulivyohangaika, tukachekwa na watu, tukakosa hata marafiki na hatimaye tukabandikwa majina ya ajabu? Umesahau, mumewangu? Umesahau namna kazi yako yakuuza makaa ilivyofikia hatima ya ghafla baada ya serikali kupiga marufuku ukataji wa miti katika eneo la Dafrau? Naomba ukumbuke. Ninaamini huenda umesahau! Ama cheo chako cha ubunge ulichokipata kwa mbinu nizijuazo mimi kimekulevya nakukufanya uisahau familia yako?"

a. Fafanua mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili (Alama 6)

b. Tambua toni zilizotumika katika dondoo hili. (Alama 2)

c. Fafanua umuhimu wa ujumbe alitoa mnenaji wa maneno haya. Tumia hoja nane. (Alama 8)

www.freekcsepastpapers.com

**R. Wangari**; *Fadhila za Punda* na **P. Muthama**: *Nilitamani*

7. (a) Kwakurejelea hadithi *Fadhila za Punda* katika mapambazuko yamachweo na hadithi nyingine, jadili maudhui yafuatayo;

i) Nafasi ya mwanamke katika jamii. (Alama 8)

ii) Ndoa. (Alama 8)

b) "Wakati anaongea kwa simu, nikawa najifungua mkanda. Nikafaulu.
Nikajaribu kufungua mlango. Duh! Ulikuwa ushatiwa *loki*. Sijui nilipata wapi nguvu za kupitia juu yake! Nikaponyoka pyu! Nikakimbia nisijue niendako. Nikakimbia. Sitaki kuangalia nyuma kwa kushtukia yaliyonikuta. Nilikata katikati ya misitu sijui nielekeako ila mbali na Romeo na pepo yake. Nimekaza mwendo huku na hema, pumzi si zangu!"

i) Fafanua aina za taswira zinazojitokeza katika dondoo hili. (Alama 4)

**8. SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

***Jibu swali la 8***

***Soma utungo ufuatao kasha ujibu maswali***

Angole Angole mwanangu
Mwanangu nakuchombeza
Nakuchombeza ulale
Ulale ukiamka
Nikupikie ubwabwa
Na mchuzi wa papa
Ukilia waniliza wanikumbusha
Ukiwawa baba na mama

Baba na mama watende
Ilimukunikatizia
Ng'ombe mbuzi kupokea
Kunioza dumukongwe
Hali ukinahalende
Kazi kupiga matonge

Likiingia mvunguni
Lavunjavunja vikombe
Likilala kitandani
Languruma kama ng'ombe.

a) Bainisha kipera hiki na utoe thibitisho (Alama 2)

b) Eleza ujumbe unaofumbwa katika utungo huu. (Alama 5)

c) Tambua mitindo ya lugha iliyotumika katika kifungu hiki. (Alama 3)

d) Eleza shughuli **mojamoja** ya kijamii na ya kiuchumi inayoendelezwa katika jamii ya utungo huu (Alama 2)

e) Unakusudia kukusanya data kuhusu kipera hiki. Eleza udhaifu wa mbinu ya mahojiano. (Alama 4)

f) Kipera hiki kinazidi kufifika katika jamii yako. Fafanua njia ambazo jamii ya kisasa inaweza kutumia kukifufua. (Alama 4)

www.freekcsepastpapers.com

**KAPSABET**
**Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
**102/1**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**(Insha)**
**MUDA: SAA 1¾**

**MAAGIZO**
- ✓ *Karatasi hii ina maswali manne.*
- ✓ *Jibu maswali mawili pekee*
- ✓ *Swali la kwanza ni la lazima.*
- ✓ *Chagua swali moja kwa yale matatu yaliyobaki.*
- ✓ *Kila insha isipungue maneno 400.*
- ✓ *Kila insha ina alama 20.*

1. Ndugu yako ameamua kuasi ukapera. Andika ratiba itakayotumiwa siku ya arusi yake.
2. Eleza mikakati ambayo serikali ya Kenya imeweka kukabiliana na mashambulizi ya mara kwa mara ya Kigaidi nchini.
3. Andika insha kuonyesha busara iliyomo katika methali “Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe”.
4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya:
   ……………Nilikumbuka ushauri niliopewa na mama mazazi mara kwa mara. Uchungu usiomithilika ulinichoma moyoni, laiti ningalijua.

---

**KAPSABET**
**Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
102/2
KISWAHILI
KARATASI YA PILI
LUGHA
MUDA: SAA MBILI NA NUSU

1. **UFAHAMU**

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata:***

Miaka michache iliyopita, kila aliyekuwa amesoma alikuwa na bahati ya kupata kazi katika ofisi za humu nchini. Wote waliofika darasa la saba au pengine kidato cha pili na zaidi wale waliofuzu mtihani wa kidato cha nne, walinyakuliwa juu kwa juu na wizara mbalimbali za serikali au pengine waliandikwa kazi na makampuni. Kwa vile kila moja wao alipata kazi ya kuajiriwa, hakuna aliyejishughulisha na kazi za mtu binafsi kama useremala, uashi, ukulima, uvuvi na kadhalika- kazi kama hizo ziliachiwa wale tu ambao hawakupata fursa ya kuenda shule.

Siku hizi mambo yamebadilika. Licha ya kuwa na elimu ya darasa la saba au kidato cha pili na pengine cha nne, hata wale wenye shahada za vyuo vikuu nao pia wamezifungia shahada hizo mashubakani zikiota ukungu huku wenyewe wakijipurukusha kulima au kufuga; na wale ambao bado hawajakata shauri kama hili, wako barabarani wakipiga lami.

Wakoloni walifanya kosa moja kubwa sana ambalo tumeligundua tu baada ya kunyakua uhuru wetu. Kosa lenyewe ni lile la kuwafanya wananchi waliopata elimu wasipende kushika kazi zinazochafua mikono.Walijua tu kwamba mashamba yao na hata mitambo yao ingalifilisiwa na ile ya waafrika; kwa hivyo ingaliwabidi hata wao waje wawatumikie wenyeji. Ndipo walipokata shauri kutowaamsha waliolala ili wasije wakalala wao.

Katika karne hii, wataalamu wameshawishika kuitumia elimu yao kufanya kazi za mashamba, ujenzi na ufundi wa mitambo. Ijapokuwa baada ya kazi kama hizo mikono huwa imejaa tope au masizi, pato lake ni kubwa ajabu. Jambo la kuvutia zaidi katika makazi kama haya ni kwamba mwananchi huwa ni ‘bwana’ mwenyewe, hujitegemea mwenyewe bila kochokocho.

Kila moja wetu yuaelewa kinaganaga kwamba kazi kama ya ukulima huleta donge kubwa zaidi ya kazi zote; kwani kila mfanyikazi humwelekea mkulima baada ya kumaliza kazi yake. Mkulima naye hutoa

www.freekcsepastpapers.com

jasho jingi wakati wa kulima shamba. Baadaye atapekua magugu na visiki aviweke katika matita ili aviteketeze moto. Baada ya muda kidogo atapanda na angoje hadi mbengu zake ziaanze kuchipuza. Mara maua huchanua na mazao kujionyesha. Baada ya kuvuna, kazi yake kubwa huwa ni kuanika na kuanua nafaka zake. Wakati huo, mazao yake huwa yatanga, mara yuapanga mara yuapangua mipango juu ya uuzaji. Mazao yafikapo nyumbani, pengine mkulima huipamba nyumba yake na akawaita marafiki zake ili awakirimu kwa vyakula na vinywaji. Karamu ikiisha hana budi kupambua mapambo yote. Huyoo, aenda kuuza bidhaa zake; akirudi yuakaa raha mstarehe akila na kuburudika pamoja na familia yake. Je kuna kazi yenye raha zaidi ya ukulima?

Watu wengi hufikiria maana ya neno 'kulima' ni kushika jembe tu. Hiyo si kweli kwani kuna ukulima namna nyingi, kama vile ufugaji wa ng'ombe, mbuzi au kuku. Hata ufugaji wa samaki au utunzaji wa nyuki pia waweza kuitwa ukulima. Dhamira ya taifa letu changa ni kuwapatia mwangaza wananchi wake waliomo mashuleni, kwamba wangojewa kwa hamu wajiunge na wenzao katika kulijenga taifa lenye nguvu, ili katika kujisaidia wenyewe pia waongeze pishi katika kulipa taifa maongozi mema yasiyokinai kazi zilizokuwa zikiitwa 'chafu' lakini ambazo ndizo hasa kiini cha maendeleo na kujitegemea.

a) Kulingana na habari uliyosoma, ni mambo gani hasa yaliyochangia kupuuzwa kwa kazi za mtu binafsi? (alama 3)

b) Wakoloni walikuwa na lengo gani kwa kufanya waafrika waliosoma kuchukia kazi za mikono? (alama 2)

c) Unafikiri mwandishi wa taarifa hii alikuwa na dhamira gani kwa wasomaji wake? (alama 1)

d) ..'Wamezifungia shahada hizo mashubakani zikiota ukungu huku wenyewe wakijipurukusha kulima au kufuga' Mwandishi anamaanisha nini katika kauli hii? (alama 2)

e) Kwa nini wasomaji wa kisasa wameanza kufanya kazi ya ukulima? (alama 3)

f) Eleza maana ya semi hizi kama zilivyotumiwa katika taarifa: (alama 4)

i) Kata shauri…………………………………………………………………

ii) Kuwa bwana ………………………………………………………………

**2. UFUPISHO**

**Soma taarifa ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata kulingana na maagizo.**

Inaaminika kuwa majeruhi wengi katika mikasa ya ajali huaga au huathirika vibaya zaidi kutokana na hali mbaya ya uokoaji.Watu wengi ambao hujitolea kutoa majeruhi baada ya ajali kama za barabarani, maporomoko ya ardhi au nyumba huwa hawang'amui hata chembe jinsi ya kukabiliana na uokoaji. Hatima ya juhudi zao ambazo hulenga kutenda mema ni kuathirika zaidi kwa majeruhi.

Hali ya ukoaji inaweza kurekebishwa kwa kutoa elimu ya huduma ya kwanza kwa umma. Elimu hii yahitajika na kila Mkenya kwani mikasa ya ajali za barabarani na nyinginezo inaendelea kutokea kila siku.

Ajali zinazotokea, si ajabu kuona makundi ya waokoaji wakibeba majeruhi hobelahobela bila kuzingatia madhara wanayoweza kuwaongezea kutokana na ubebaji wao. Kutojua namna ya kumbeba majeruhi kunaweza kumhatarisha na hata kusababisha kifo.

Kuna mambo mbalimbali ambayo makundi ya waokoaji yanatakiwa kuzingatia wakati yanatoa huduma ya kuokoa. Kwanza ni muhimu kuchunguza kama kuna hatari yoyote inayoweza ikatokea na kuwatia majeruhi na waokoaji hatarini zaidi. Makundi ya waokoaji yameweza kwa kuliingilia eneo la ajali mbumbumbu kama mzungu wa reli.

Hatua ya pili ni kutafuta idadi ya majeruhi. Pana uwezekano wa majeruhi kutupwa mbali na eneo Ia ajali. Vivyo hivyo, kuna majeruhi ambao huweweseka baada ya ajali na kuanza kutembea wasijue wanakoelekea. Wengi wao huaanguka karibu na eneo la ajali au wakaenda mbali.

Hatua ya tatu ni kuchunguza kama majeruhi amezimia, moyo unapiga na jinsi anavyopumua. Ili kuhakikisha kuwa majeruhi anapumua, mwokoaji atazame kama kifua kinapanda na kushuka. Halikadhalika, mwokoaji anaweza kusikiliza au kuguza kifua na kuona kama kuna ishara za kupumua. Iwapo majeruhi anapumua, mwokoaji amweke katika hali ambayo itaimarisha kupumua kwake. Anaweza akamlaza chali au kumgeuza kwa pamoja na kichwa chake ili kufungua mkondo wa hewa. Pia mwokoaji ahakikishe hamna chochote kinywani kinachoweza kumsakama. Ikiwa hapumui, mwokoaji anaweza kujaribu kumfanya apumue kwa kupuliza hewa mdomoni mwake.

www.freekcsepastpapers.com

Fauka ya hayo, Upulizaji wa hewa utahakikisha kuwa damu inazunguka mwilini vizuri.
Hatua nyingine ni kuchunguza vile amejeruhiwa. Chunguza kama majeraha ni vidonda tu au kuna kuvunjika kwa mfupa na kubainisha ni mfupa upi. Haya yatamwezesha mwokoaji kujua jinsi ya kumbeba majeruhi. Pakiwa na kuvunjika kwa mfupa, ni muhimu kutotumia kiungo kilichovunjika anapobebwa.

Pia kuchunguza vile majeruhi amejeruhiwa, humwezesha mwokoaji kujua huduma ya dharura atakayotumia. Majeruhi akiwa anavuja damu sana, ni muhimu kuzuia uvujaji huu. Iwapo ni kidonda kidogo, kinahitaji kufungwa ili kuzuia uambukizaji. Mwokoaji anaweza kutumia kifaa chochote kilicho karibu kutolea huduma hizi. Kwa mfano, anaweza kupasua nguo ya majeruhi iii apate kitambaa cha kusaidia kuzuia kuvuja kwa damu au kumfunga kidonda.

Hatua inayofuata ni kumhamisha majeruhi toka eneo la ajali hadi hospitalini. Mwokoaji anaweza kuwatumia watu wengine kutafuta msaada. Wanaweza kupiga simu wakitumia nambari za simu za dharura kama zile za polisi, wazimamoto au makundi ya wataalamu wa shughuli za ukoaji. Nambari hii ya simu huwa 999 popote na huwa haina malipo. Wanaopiga simu ni vyema kutoa maelezo ya mahali ambapo ajali imetokea, ama ya ajali na huduma za dharura zinazohitajika pamoja na idadi ya majeruhi. Iwapo makundi haya ya ukoaji yameahidi kufika, ni bora kuwasubiri.

Ikiwa makundi ya wataalamu wa ukoaji hayakupatikana, ni jukumu Ia mwokoaji kuhakikisha majeruhi wamehamishwa na kupelekwa hospitalini. Majeruhi wakiwa wengi, ni bora kuanza na wale waliozimia au wenye matatizo ya kupumua kisha kuwaendea wanaovuja damu sana. Baadaye mwokoaji awasaidie waliovunjika mifupa huku akimalizia na wenye majeraha yasiyohatarisha maisha. Ni muhimu kuwabeba majeruhi kwa kutumia machela. Hii hupunguza kuathirika zaidi kwa majeruhi. Iwapo hamna machela karibu, mwokoaji anaweza kuunda moja kwa kutumia vipande viwili vya mbao, blanketi, shuka au makoti.

Ujuzi wa huduma ya kwanza ni mojawapo ya mambo muhimu ambayo kila mtu anapaswa kuwa nayo.

**Maswali**:

(a) Fupisha aya tatu za kwanza kwa maneno 50-60. (alama 5) ut.1

**NAKALA CHAFU**

**NAKALA SAFI**

(b) Eleza kwa kutumia maneno 90 — 100, hatua zinazotakiwa kufuatwa wakati wa uokoaji. (alama 7) Ut.2

**NAKALA CHAFU**

**NAKALA SAFI**

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

**a)** (i) Taja sauti mbili ambazo ni irabu na wakati huo huo konsonanti. (alama 2)

(ii) Tambua sauti hafifu kati ya zifuatazo: (alama 1)
/K/, /r/, /gh/,/ sh/, /w/

b) Onyesha yambwa tendwa na yambwa tendewa katika sentensi hii. (alama 2)
Mbunge wa Mtondo Kaskazini atawajengea wanakijiji josho kisha aghurie mjini. …………

c) Andika kwa msemo taarifa (alama 3)
"Sitakwenda sokoni leo ila nitakwenda kesho," nikamjibu

d) Eleza matumizi ya neno wale katika sentensi hii. (alama 3)
Wale walioiba ni mabanati wale ambao waliambiwa wale kabla ya kitendo hicho.

e) Yakinisha sentensi hii. (alama 1)
Hapa napo sipo ninapotaka

f) Changanua kwa vielelezo vya mistari / vishale. (alama 3)
Mwanafunzi anapohepa shuleni huadhibiwa kikondoo.

g) Andika kwa udogo (alama 2)
Mtoto wa mzee yule aligongwa kwa nyundo alipofukuzwa na mbwa.

h) Tumia kiunganishi <u>alakulihali</u> katika sentensi ili kubainisha matumizi yake. (alama 1)

i) Akifisha sentensi hii (alama 3)
mtafanya kazi hii mpaka lini mzee alisema nataka ikamilike leo kesho mtaanza nyingine

j) Tunga sentensi ukitumia 'A'unganifu mwafaka pamoja na nomino ulizopewa (alama 2)

(i) Teo

(ii) Liwali

www.freekcsepastpapers.com

k) Eleza matumizi ya ni katika sentensi ifuatayo: (alama 3)
Rudi**ni** haraka! Amina **<u>ni</u>** mgeni hapa kwetu, nitamtembeza mji**ni**

l) Vitumie vihisishi vifuatavyo katika sentensi. (alama 2)
(i) Ebo!
(ii) Kefule!

m) Sentensi hizi zinaashiria nyakati gani? (alama 2)
(i) Ninapokimbia huchoka sana
(ii) Aendapo msikitini hujitia tohara

n) (i) Imekuwa vigumu mwananchi kuelewa katiba
(andika katika kauli ya kutendea) (alama 1)
(ii) Andika sentensi katika kauli ya kutendewa ukitumia kitenzi 'cha' (alama 1)

o) Tumia vivumishi vya pekee kutunga sentensi zenye maana ifuatayo. (alama 2)
(i) bila kubagua
(ii) bila kubakisha

p) Eleza maana mbili za sentensi hii (alama 2)
Alinichezea na Baniani

q) Tunga sentensi mbili tofauti kubainisha maana tofauti kati ya: (alama 2)
(i) Pamba
(ii) Bamba

r) Mwalimu huyu atawatahini wanafunzi wote watakaofanya mtihani. (alama1)
Anza: Wanafunzi wote

s) Unda kitenzi kutokana na nomino hii (alama 1)

| ***Nomino*** | ***kitenzi*** |
|---|---|
| Ufisadi | ………………………………… |

**4. ISIMU JAMII**

(Mdundo wa muziki) Kina mama mpo ……………! Kina siste nanyi ………. Are you there? Kampuni ya Platinium imewaletea mafuta mpya ya Silk. Mafuta hayo yana vitamin C, Sunscreen na yana marashi ya kupendeza. Ukiyatumia kwa wiki moja tu, ngozi yako itakuwa laini na nyororo kama ya kitoto kichanga. Nayo macho ya wote, Waaa! Yatakuwa kwako 24/7. Jinunulie! Jinunulie! Mafuta ya silk. Mafuta ya wanawake wa kisasa.

(a) Taja sajili iliyotumiwa hapa. (alama 1 )
(b) Taja sifa nne za sajili hii. (alama 4)
(c) Kwa nini Wakenya wengi hupenda kuchanganya na kubadili msimbo? (alama 5)

www.freekcsepastpapers.com

**KAPSABET**
**Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari**
**102/3**
**KISWAHILI**
Karatasi ya 3
**Muda: SAA $2^{1}/_{2}$**

**SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI**

**1. Lazima**

a) "Mwanangu nakuomba uzingatie uadilifu maishani.Uongofu ni nuru ya mustakabali wa kila mtu…"

i) Tambua kipera na utanzu wa tungo hili (alama 2)

ii) Kwa kutumia hoja **mbili** eleza muundo wa kipera hiki (alama 2)

iii) a) Fafanua sifa **nane** za kipera hiki (alama 8)

b) Eleza vikwazo **vinane** vya ukuaji wa fasihi simulizi. (alama 8)

**SEHEMU B: RIWAYA**
**Matei:** ***Chozi la Heri***
**Jibu swali la 2 au 3**
**Assumpta K. Matei: Chozi la heri**

2. "Hili lilimtia ………… uchungu, akajiona kama aliyedhalilishwa na mwanamke."

(a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake (alama 4)

(b) Taja maudhui linalodokezwa katika dondoo hili (alama 1)

(c) Kwa kutumia hoja kumi na tano, eleza namna maudhui uliyotaja hapo juu 1 (b) linalijitokeza (alama 15)

3. a) "Siasa mbaya maisha mabaya."Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri. (alama.10).

b) Fafanua athari za umaskini katika jamii ukirejelea Riwaya ya Chozi la Heri. (alama.10)

**SEHEMU C**
**TAMTHILIA:** Timothy Arege: BEMBEA YA MAISHA
Jibu swali la 4 au la 5

4. "Nyinyi mmebahatika kuwa mbegu nzuri istahiliyo kupandwa. Japo wapaliliaji ni haba, shikeni usukani muwe marubani wa kweli ili ndege ipae angani"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Tambua tamathali mbili za usemi katika dondoo hili. (alama 2)

c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa dondoo hili katika kuijenga tamthilia ya Bembea ya Maisha. (alama 4)

d) Thibitisha kuwa walengwa wamekuwa mbegu nzuri istahiliyo kupandwa. (alama 10)

5. "…wakati huo sikuona, sasa ninaona. Wanasema mwenye macho haambiwi tazama. Kweli ilioje! Japo hutokea wakati tukalalamika, nafikiri… ni zawadi nzuri katika kuleta mshikamano wa kijamii.
Onyesha jinsi wahusika kwenye tamthilia ya Bembea wamekuwa zawadi nzuri katika kuleta mshikamano wa kijamii. (alama 20)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

***6.*** **Uliza wanaojua**

Wako wapi waliokuwa viongozi zamani
Waliokitoa hotuba ujamaa kuupigania?
Sasa wamestaafu ndio wafuga kuku
Ndio wenye majumba ubepari kurithisha!
Kama wewe hujui, uliza wanaojua
Ukweli watakwambia.

Au hujaona makabaila wenye mashamba.
Matrekta yanafukuta na vumbi kutimuliwa!
Zungumza juu ya vijiji watakuonyesha kidole
"Pilipili usiyoila yakuwashiani!"
Basi, kama wewe hujui, uliza wanaojua
Ukweli watakwambia.

www.freekcsepastpapers.com

Lakini Darubini la Serikali ni kubwa sana
Tena lina nguvu sana na lina sumaku.
Linawavuta wakapimwa
Chote walichokwisha kula kikaonekana
Rafiki, kama wewe hujui, basi uliza Wanaojua.
Ukweli watakwambia.

Hata dawa ya kutapisha Serikali inayo
Mabepari na Makabaila wametapishwa hadharani
Wakaona na aibu mbele ya wake zao.
Wananchi tuliwazomea tena tukacheka sana.
Ndugu, kama wewe hujui, basi usinyamaze.
Uliza wanaojua. Ukweli watakwambia.

**Maswali:**

(a) Thibitisha kwamba hili ni shairi. (alama 3)
(b) Jadili matumizi ya kinaya katika shairi hili. (alama 4)
(c) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (alama 4)
(d) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
(e) Eleza matumizi yoyote mawili ya mishata. (alama 2)
(f) Bainisha nafsi-nenwa katika shairi hili. (alama 1)
(g) Thibitisha kuwa mabadiliko hayaishi duniani kwa kurejelea shairi hili. (alama 4)

**7. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata**

Ndege mwema na muruwa, katu haishi tunduni
Hataki kufadhiliwa, muda yumo utumwani
Japo mnyonyoe mbawa,mwisho wake atahuni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa.

Ndege ataka yoyoma, nasiyahi msituni
Apite akisimama, shinani na mitawini
Haridhiki kwa mtama, na maji ya kikombeni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mwema wa hishima, mwema mno wa kughani
Tundu huliona chama, japo liwe la thamani
Huporomosha yakwe kima, na kufanya faraghani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mpambe kwa zari, na lulu na marijani
Upambe yake suduri, kwa almasi kidani
Tunduni atahajiri, ili awe huriani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mwema wa busara, hatoishi kifungoni
Anayo kubwa hasara, kukosa nyumba ya mani
Lamkera lamkera, tundu la dhahabu kwani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege maumbile yake, na waja hayalingani
Yeye hutaka wenzake wafukuzane hewani
Jambo la kuishi mpweke, kamwe humridhiani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Baiti zangu ni haba, nakonea kituoni
Ndege huficha mahaba, kama yumo kifungoni
Hali ndege akashaba, kwani yumo adhabuni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Lipe shairi anwani mwafaka (alama 1)
(b) Fumbua maana ya ndege anayerejelewa (alama 1)
(c) Shairi hii ni la mkondo gani? (alama 3)
(d) Eleza muundo wa ubeti wa nne (alama 3)
(e) Fafanua uhuru aliotumia mshairi (alama 4)
(f) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (alama 4)
(g) Jadili dhamira ya mshairi (alama 2)
(h) Fafanua maana ya msamiati ufuatao kama ilivyotumiwa na mshairi (alama 2)
i) Atahuni
ii) Baiti

**SEHEMU E: Hadithi Fupi**

D. W. Lutomia na Phibian Muthama:

Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine.

Jibu swali la 8 au la 9

**D.W. Lutomia:** *Msiba wa Kujitakia*

**8.** Jioni Machoka ameketi kitako kochini.Amerejea akiwa amechoka zaidi ya kuchoka. Pilkapilka zake za kutafuta kibarua mchana kutwa zimegonga mwamba.Hajui la kufanya. Matumbo yake yanateta kwa kushindwa kuhimili makali ya njaa.Hajatia chochote kinywani tangu asubuhi.Taswira ya chumba chake ingeweza kumliza kipofu! Anawaza juu ya maisha yake. Maisha ya wasakatoge. Maisha ya wanaojiita 'pangu pakavu'. Maisha ya wapiga kura. Maisha ambayo ni tofauti sana na maisha ya waliopigia kura, yametengana kama mbingu na ardhi. Machoka anabaki kukondoa macho huku maonevu yakiihukumu nafsi yake. Anasimama pale kama kigingi. Hasongi wala kufurukuta.

a) Onyesha mbinu **sita** za kimtindo zilizotumika katika kifungu hiki. (alama 6)
b) Onyesha hali ya maisha ya wanaojiita 'pangu pakavu' ilivyo katika Jimbo la Matopeni. (alama 10)
c) Jadili maudhui ya usaliti kama yanavyojitokeza katika hadithi husika. (alama 4)

**9. Sabina (Winnie Nyaruri Ogenche)**

a) **"**Siwezi kususia jukumu hata moja kwa sababu nikifanya hivyo nitakuwa najipalia makaa''
  i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  ii) Tambua mbinu iliyotumiwa katika dondoo. (alama 1)
  iii) Jadili masaibu yaliyompata msemaji wa maneno haya kwa kurejelea hadithi nzima. (alama 5)

b) **"**Kumbe kucheza na pombe ni sawa na kucheza na moto!"
Jadili ukweli na kauli hii kwa kurejelea hadithi ya "**Kila Mchezea Wembe"** (alama 10)

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA MWIGO WA MATHIRA WEST**
**102/1**
**KISWAHILI**
**INSHA**
**KARTASI YA 1**
**MUDA: 1¾**

**MAAGIZO**
(a) *Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima*
(b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobaki*
(c) *Kila insha isipungue maneno 400*
(d) *Kila insha ina alama 20*
(e) *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya kiswahili*

1. Suala la Afya ya akili ni suala telezi na telezi na ambalo halijapewa umakini ufaao na wanajamii kutokana na unyanyapaa unaohusishwa nalo.
   Ukiwa mhariri wa Gazeti la mzalendo, andika tahariri kuangazia vyanzo vya changamoto hii na kupendekeza suluhu mwafaka.
2. Wewe ni kiranja mkuu shuleni mwenu. Andika memo ukiwaonya wanafunzi dhidi ya visa vya utovu wa nidhamu shuleni
3. Tunga kisa kitakachoafiki maana ya methali ifuatayo; "Mpanda ngazi hushuka."
4. Tunga kisa kitakachokamilika kwa maneno yafuatayo: Kweli nimetambua kuwa, familia ni nguzo muhimu katika ujenzi wa jamii.

---

**MTIHANI WA MWIGO WA MATHIRA WEST**
**102/2**
**KISWAHILI**
**LUGHA**
**MUDA: 2½**

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali*

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo ulimwenguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malighafi inayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji viwanda vinavyoimarika ni vile vidogo. Hivi ni viwanda ambavyo huhusisha amali za mikono. Kuimarika kwa viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu sana kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa na bidhaa za viwanda. Katika msingi huu viwanda vikubwa vitawiwa ugumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vidogo pia vinao uwezo wa kuwaajiri wafanyikazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine. Uajiri huu wa wafanyikazi wengi ni muhimu katika maeneo mengi ambako tatizo la ajira ni mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasmia (yenye viwanda vingi) mataifa mengi yanayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo hakuhitaji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Sambamba na suala hili ni kuwa ni rahisi kujarisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo. Ikiwa mzalishaji yeyote atazalisha bidhaa mpya kwa mapanu, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hiyo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa yenyewe. Majaribio mazuri huwa ni kwa kiwango kidogo.

Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa chocheo kubwa la usambazi wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikisha kuwa nafasi za ajira zimezambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huo wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa

www.freekcsepastpapers.com

kiununuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo. Upanuzi ueneaji wa viwanda vidogo vidogo ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa msingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

(a) Eleza dhina ya viwanda al3
(b) Fafanua vyanzo vya matatizo ya uuzaji wa bidhaa katika nchi zinazoendelea al2
(c) Viwanda vidogovidogo ni muhimu katika uendeleaji wa nchi zinazoendelea. Thibitisha al5
(d) Linganua nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea al5

**2. UFUPISHO (ALAMA 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Kila mwaka, watoto milioni 10 hufariki katika mataifa yanayoendelea kabla ya kufikisha umri wa miaka mitano. Hii mara nyingi hutokana na magonjwa yanayoweza kuzuiliwa ama kutibiwa. Kulingana na ripoti ya hivi punde kabisa ya shirika la watoto la umoja wa kimataifa UNICEF, watoto milioni 2.2 wnaweza kuokolewa ikiwa wazazi wao watahudhuria kliniki inavyohitajika baada ya kujifungua hadi miaka mitano. Huu ndio wakati watoto hupewa huduma muhimu kama chanjo. Vile vile mzazi hupokea mawaidha muhimu kuhusu jinsi anavyoweza kumlea mwanawe katika hali nzuri, na hatua anazohitajika kuchukua shida zinapotokea.

Kliniki hizi ni muhimu sana haswa kwa kutoa mwongozojinsi yakumtunza mtoto na mama mwenyewe baada ya kujifungua. Huduma anazopata katika kliniki humwezesha kutambua ikiwa mwanawe anakua ipasavyo na hatua atakazochukua tatizo linapotokea. Sababu kuu ni kwamba miaka mitano ya kwanza katika maisha ya mtoto ni kipindi kinachohitaji mzazi kuwa muangalifu sana.

Kipindi hiki ambacho wataalamu hukiita 'pre-schoolhealth' ni muhimu mno kwani mtoto hukaguliwa namna anavyokua na hali yake ya afya. Hakuna mwingine anayefahamu afya ya mwanao vizuri muda wote huu ila muuguzi anayekuhudumia katika kliniki baada ya kujifungua.
Hata hivyo wataalamu wanasisitiza kwamba kliniki si kwa kina mama pekee bali kwa wazazi wa kiume. Kina baba wanahimizwa wahudhurie kliniki hizi kwani jukumu la kumlea mtoto ni wazazi wote wawili.

Katika kliniki hizi mzazi hupewa habari kuhusu maradhi yanayojitokeza katika miezi ya kwanza kama homa ya macho, vipele vya ngozi, uvimbe wa ndani, kuhara, kulia ovyoovyo na msokoto wa tumbo. Lakini si hayo tu utapata ufahamu wa magonjwa sugu ambayo UNICEF inaorodhesha kama sababu kuu zinazopelekea watoto wengi katika nchi zinazoendelea kufariki wakiwa chini ya miaka mitano. Virus vya HIV na Ukimwi, surua, malaria, kuharisha na nimonia husababisha asilimia 3,4,8,17 na 19 mtawalia vya vifo hivi. Hata hivyo maradhi yanayotokana na hali mbaya ya mama anapomtunza mwanawe, au mazingira machafu husababisha vifo asilimia 36 ama milioni 4 katika mwezi wa kwanza baada ya kuzaliwa. Nao ugonjwa wa utapiamlo huwaua watoto milioni sita au asilimia 53 kila mwaka. Mzazi anapaswa kujihami na ufahamu wa maradhi haya ambayo mengi hupuuzwa kama maambukizi rahisi. Wale wanaopuuza kliniki hizi baada ya kujifungua huwa, wanajihatarisha kando na kujionyesha kama wazazi wapumbavu ihali wanaelewa majukumu yao.

Nchini Kenya, changamoto kuu katika miaka kuhakikisha watoto wanakua na kufikisha miaka mitano wakiwa wenye afya bora ni kutolewa kwa huduma za kimsingi kwa watoto wote kokote kule. Serikali inajitahidi kuimarisha kampeni za kuwasihi kina mama kuhudhuria kliniki baada ya kujifungua. Utawapata wahudumu wa afya tayari kukupa mawaidha jinsi ya kuzuia magonjwa kadha ambayo huwatatiza kina mama na hata kutoa matibabu ya kwanza kwa yale maradhi mwanao atapata.

Kumekua na matangazo ya mara kwa mara katika vyombo kuhusu chanjo za bure zikitolewa mle mashinani na maafisa wa afya wa serikali. Katika mataifa kadha serikali zimengoeza uwezekano wa kufikia na kupokea huduma za afya kwa kuondoa ama kupunguza gharama za huduma msingi katika vituo vya umma. Aidha serikali zimeimarisha ubora wahuduma zinazotolea kwa kuwapa mafunzo maafisa wa afya. Pia, zinawapa mafunzo watu kutoka jamii hizi waliojitolea kufikia jamii zilizo mbali na kliniki. Hivyo wanaweza kutoa ushauri kuhusu jinsi ya huduma ya kwanza kutibu magonjwa haya watu huwa wa kujitolea huwa muhimu sana katika kuripoti visa vya mkurupuko wa maradhi kwa maasifa wa afya kwenye kliniki za kina mama na watoto.
Njia ya pili inayotumika kwa wingi ni kampeni za chanjo zinazoendelezwa na serikali kwa usaidizi wa wakaazi wa maeneno hayo ili kuhakikisha kila mtoto mchanga anapata chanjo. Hizi huwa kampeni za nyumba ama kliniki spesheli za chanjo huwekwa katika jamii nzima.

www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) Kwa maneno 40-45 dondoa hoja kuu katika aya tatu za kwanza (al 8 )
Nakala chafu / Nakala safi

b) Fupisha aya tatu za mwisho (Maneno 80) (alama 7)
Nakala chafu / Nakala safi

**3. <u>LUGHA (ALAMA 40)</u>**

A) Ainisha nomino katika sentensi (alama 1)
Wewe wake ulimsaidia katika kupata maji ya ziada

B) Fananisha sauti /m/ na /n/ kwa njia mbili (alama 1)

C) Andika maneno yenye miundo ifuatayo ya silabi (alama 2)
I) KKII II) KKIKI

D) Andika katika udogo.
Maguu ya majibwa yametibiwa na jana hilo (alama 2)

E) Bainisha mofimu katika neno lifuatalo
Atamnywea (alama 3

F) Ainisha mofimu katika sentensi ifuatayo
Huyu ndiye aliyetukomboa (alama 2)

G) Eleza matumizi ya 'na' katika (alama 2
Nina na Tina wanaandikiana barua na Mina

H) Unda upya sentensi hii ukigenza maneno yaliyopigwa mstari kuwa nomino (alama 2)
Watu hao <u>walifungua</u> mlango baada ya <u>kutafakari</u> kwingi.

I) Weka shadda katika maneno yafuatayo
i) Miambakofi (alama 1)
ii) Baiskeli

J) Ainisha yambwa katika sentensi ifuatayo (alama 3)
Kaka alimwandikia nyanya barua kwa pensili

K) Andika kinyume
Akina mama wameombwa waanike nguo (alama 2)

L) Tunga sentensi zilizo na vivumishi vifuatavyo (alama 2)
I) Kivumishi cha pekee kilicho na dhana ya kutobagua
II) Kivumishi cha nomino

M) Tunga sentensi ya kuonyesha rai (alama 1)

N) Binisha vishazi katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Ikiwa unataka kufaulu lazima utie bidii shuleni

O) Unganisha sentensi hizi kuunda sentensi ambatano (alama 1)
I) Wnajamii wanaishi karibu na msitu
II) Wanajamii hawa huharibu msitu

P) Kwa kutumia sentensi moja, onyesha matumizi mawili ya kibainishi (alama 2)

Q) Andika sentensi hii upya kwa urejeshi tamati;
Mwanafunzi ambaye hufaulu ni yule ambaye anajitahidi (alama 2)

R) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao;
KN (W) + KT (Ts + T + E) (alama 2)

S) Andika sentensi hii katika usemi halisi; (alama 2)
Mwalimu alitwambia tungeifanya kazi hiyo mpaka tuchoke

T) Kamilisha;
Mama ni kwa nina; ila ……….. ni kwa baba na …………. ni kwa ndovu (alama 2)

U) Changanua sentensi hii kwa matawi (alama 3)
Wote waliokuwa wameitwa walipewa ajira nzuri

**4. <u>ISIMU JAMII (ALAMA 10)</u>**

Wewe ni kiongozi wa chama cha wafanyikazi, umepewa jukumu la kuwahutubia wafanyikazi wa kampuniya jitihada.
Fafanua sifa kumi, za lugha utakayotumia (alama 10)

www.freekcsepastpapers.com

**MTIHANI WA MWIGO WA MATHIRA WEST**
**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI**
**MUDA: SAA 2½**

**MAAGIZO**

a) *Jibu maswali manne pekee*
b) *Swali la kwanza ni la lazima*
c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani Riwaya, Tamthilia, ushairi na hadithi fupi*
d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*

**SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI**

**1.** *(Lazima)*

*Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali*

Heri ujue mapema
Nasaba yetu haina woga
Woga haumei kwetu, humea kwa kina mamako
Tulichinja jogoo na fahali ili uwe mwanaume

Ah! Kisu cha ngariba ni kikali ajali
Iwapo utatikisa kichwacho,
Uhamie kwa wasiotahiri,
Aa tukwite njeku.

Mpwangu kumbuka hili,
Wanaume wa mlango wetu
Si waoga wa kisu
Wao hukatwa mchana hadi usiku
Wala hawalalamiki.

Siku nilipokatwa
Nilisimama tisti
Nikacheka ngariba kwa tashtiti
Halikunitoka chozi.

Iwapo utapepesa kope
Wasichana wa kwetu na wa mbali
Wote watakucheka
Ubaki ukinuna

Sembe umepokea
Na supu ya makongoro ukabugia
Seria unachotaka
Usije kunitia aibu

www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha (alama 2)
(b) Eleza shughuli mbili za kiuchumi za jamii hii (alama 2)
(c) Bainisha nafsineni ya utungo huu (alama 1)
(d) Eleza mambo ambayo nafsineni itazingatia katika kufanikisha uwasilishaji wake (alama 5)
(e) Fafanua mambo ambayo yatapotea wimbo huu ukiandikwa (alama 6)
(f) Ingawa nyimbo zina faida katika jamii, zina madhara yake. Yaeleze madhara <u>manne</u> (alama 4)

**SEHEMU B: RIWAYA** **(A MATEI; CHOZI LA HERI)**

**Jibu swali la 2 au la 3.**

**2.** Jadili jinsi haki za wafanyakazi zilivyokiukwa kwa kurejelea riwaya ya 'Chozi la Heri.' (alama 20)

**3.** Basi Mwamu wangu Ridhaa, muda haukuipita kabla ya kusikia mlio wa bunduki, mitutu yake ilitema risasi jinsi bafe atemavyo mate. Vilio vya kite vilihanikiza hewani, vita vikaanza kati ya kundi lililounga mkono uongozi wa Mwekevu na lile lililounga mkono mpinazi ambao awali waliishi katika zizi moja, wakishiriki kazi pamoja, wakishiriki pamoja vunoni, sas wakawa hawapikiki katika chungu kimoja! Mara, "Tangu lini mwanamke akashinda katika uchanguzi? Kama mamataifa huyu mwanagenzi ambaye hatat kushika mgwisho sisi ndio tulimfunza?"

a) Changanua mtindo katika dondoo hili (alama 7)

b) Fafanua umuhimu wa msimulizi wa dondoo hili katika kujenga

i) Msuko/ploti (alama 5)

ii) Maudhui (alama 5)

iii) Wahusika (alama 3)

**SEHEMU C: TAMTHILIA** **(TIMOTHY M. AREGE: BEMBEA YA MAISHA)**

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** Haidhuru. Umenirudisha nyuma kweli katika siku zile za ujana wangu. Asubuhi niko skuli majira ya alfajiri, kiboko mkononi. Anayekuja baada yangu hata kama hajachelewa alikuwa hana lake. Siku nzima kazi tu. Jioni darasani tena, kiboko mkononi. Siyo siku hizi. Huwezi tena kumyoasha mtoto kwa kiboko. Vitabu navyo nilikuwa nikivifunga kwenye baiskeli kwenda kuvisahihisha wikendi.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Fafanua mbinu nne za kimtindo katika kifungu hiki (alama 4)

**5.** "Lakini katika vicheko vyetu, zimezikwa kero zetu. Wanavyosema, muungwana hununa moyoni, siyo usoni."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Bainisha toni ya dondoo hili (alama 2)

c) Fafanua sifa sita za msemaji wa dondoo hili (alama 6)

d) Kwa kutolea mifano tamthiliani, thibitisha ukweli kuwa waungwana wengi wamenuna moyoni bali si usoni (alama 8)

**SEHEMU D: USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6.** Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

**FUJO TUMBONI**

Siku moja, miongoni mwa wengi
Virago vyetu migongoni
Tulianza safari
Kuhama janga la jangwa
Kutafuta bonde la rutuba
Na mvua nzitinzito
Kulima kwa nyoyo imara
Kuzima moto tumboni.

Miaka imepita
Na kupita
Bali, tuzo kutoka ardhi
Kwa wale ambao
Wamekauka kama kuni
Kutokana na nyimbo
Za kuishi ardhi
Ni moto tele tumboni.

www.freekcsepastpapers.com

Lo! Maisha haya!
Ukweli mchungu!
Hii ng'ambo tunayolimia
Kwa kalamko zamisuli
Siyo tuliyoona
Kwa macho ya ndoto
Tulipoanza safari.

Aka! Maisha haya!
Maisha yanadondoka njama!
Njama za malaika wa machozi
Za kuiba matunda ya udongo
Baada ya wakulima
Kugofuka kama mahame
Kutokana na makofi
Ya jua
Na mateke
Ya njaa

**<u>Maswali</u>**

a) Shairi hili ni la aina gani? Thibitisha (alama 2)
b) Eleza ujumbe wa shairi hili (alama 6)
c) Kwa kutolea mfano kwenye shairi, eleza maana ya mshororo mshata (alama 2)
d) Bainisha toni ya shairi hili (alama 3)
e) Eleza mbinu tatu za kimtindo zilizotumika katika shairi hili (alama 2)
f) Eleza dhima ya aina tatu za urudiaji katika shairi hili (alama 3)
g) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari (alama 2)

**7.** ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Pana haja ya kupima, neno tuzowele-angu
Tusizowee kusema, hili ni teuo langu
Huenda huji mapema, -angu huja kuwa tungu
Ikaja kukusakama, na kukuposha kwa Mungu
Pana haja ya kupima.

Neno huwa ni la kwako, likiwa ndani moyoni
Lakini katu si lako, likishavuka menoni
Kwa hivyo likutokako, liweke kwenye mizani
Linaweza kuwa cheko, ama tusi kwa wendani
Pana haja ya kupima.

Mwana ujuwe ni wako, punje ukiimezele
Lakini katu si wako, nde ukimuletele
Akiwa yu ndani yako, ni wa duniya vivile
Ukishishilia ni wako, muavye takakuole
Pana haja ya kupima.

Maisha nayo si wako, utabaradi milele
Ungayaishi ja yako, ni tunu ya maumbile
Mgawa si kufu yako, mshindane hili lile
Akupapo akupoko, utaishi palepale
Pana haja ya kupima.

www.freekcsepastpapers.com